

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 23 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika(Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 129

Mafao Kwa Wastaafu Wanachama Wa NSSF

MHE. AMINA D. HASSAN aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaondoa tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya mafao kwa wastaafu wanachama wa *NSSF*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Daud Hassan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikihakikisha kuwa wastaafu wote wanalipwa mafao yao ya pensheni kwa mujibu wa Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini pindi wanapostaafu. Aidha, ili mstaafu aweze kulipwa mafao ya pensheni ni lazima awe amekidhi vigezo vifuatavyo:-

Mosi, awe ametimiza umri wa kustaafu kwa mujibu wa sheria, ambapo ni miaka 55 hadi 59 kwa hiari na miaka 60 kwa lazima.

Pili, awe amechangia kwenye Mfuko kwa kipindi kisichopungua miezi 180 au miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yaani *NSSF* wastaafu wote wanaokidhi vigezo na kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika hulipwa mafao ya pensheni kwa wakati pasipo kuchelewa. Mwanachama akiwasilisha maombi ya kuomba kulipwa mafao na akawasilisha nyaraka husika, mwanachama atalipwa mafao yake ndani ya siku 30. Aidha, malipo ya pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu hulipwa tarehe 25 ya kila mwezi moja kwa moja

kwenye akaunti za wastaafu na hadi sasa hakuna malimbikizo yoyote ya mafao ya pensheni kwa wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2020 – Machi, 2021, jumla ya wanachama 93,861 wamelipwa mafao mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 377.8. Aidha, tunawasihi waajiri kuwasilisha michango ya watumishi wao kila mwezi kwa wakati na ninawasihi wastaafu kuhakikisha wanawasilisha nyaraka zote zinazotakiwa kwa mwanachama ili kuwezeshwa kulipwa mafao na kuondoa ucheleweshaji unaoweza kujitokeza katika kuanda mafao ya wastaafu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Daud Hassan, swal la nyongeza.

MHE. AMINA D. HASSAN: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; pamoja na majibu yake mazuri Naibu Waziri aliyonipa, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini hasa Serikali itaanza kulipa mafao ya wanachama ambao wana miaka zaidi ya mitatu wanafuatilia masuala yao hawajafanikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili je, Serikali inamkakati gani kuhakikisha kwamba wastaafu wanalipwa kwa wakati ili islathiri dhamani ya fedha ambayo wanalipwa? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Amina Daud Hassan kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni lini Serikali itakamilisha ulipaji wa Wawanachama ambao wana miaka mitatu sasa ambapo hawajaweza kulipwa mafao yao. Nimakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza nimpongeze kwa

kufuatilia hasa kuhusu wananchi wake katika matatizo hayo ambayo wanayapata labda pengine ya kuwacheleweshea malipo. Lakini zaidi niweze kumuambia Mheshimiwa Mbunge mpaka sasa mfuko wetu hauna madeni kwa maana ya kwamba wastaa fu wote ambao wamewasilisha nyaraka zao zenye usahihi ndani ya siku 30 anakuwa ameshalipwa malipo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa kama kuna mwananchi wake ambao amewasema zaidi ya miaka mitatu pengine hawajaweza kulipwa mafao yao niombe tu niwasiliane naye, nipate hizo *details* ili niweze kushughulikia waweze kulipwa kwa sababu ni haki yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu mkakati wa Serikali wa kuhakikisha malipo haya yanalipwa kwa wakati. Tayari Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa maelekezo yake, tumekwisha kuanza kufanya kazi ya kuchunguza madai, lakini pia kuweza kuangalia kwa undani tija ya fedha ambazo zinapatikana katika mfuko, zaidi ya hapo uwekezaji unaofanywa pia na mfuko na tatu tunaenda katika kufanya uchunguzi wa madai yote ambayo yalikuwa ya awali kama yapo kuweza kujhakikishia kwamba yanafanyiwa uchunguzi na baada ya kujiridhisha tuweze kuwalipa madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika huo mkakati ambao upo mkubwa kwa sasa tunasubiri *actuarial report* ambao Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu amekua akiisimamia kwa kipindi chote na *actuarial report* itatoa taarifa kwa ujumla jinsi *status* ya mifuko hii na namna gani ambavyo itajiendesa kwa faida zaidi kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais jana katika hotuba yake aligusia na kuweza kueleza namna gani ambavyo mashirika ya umma, lakini taasisi na mifuko iweze kujijendesa kwa faida. Kwa hiyo hili Mheshimiwa Mbunge, tunakuakikishia kwamba halitavuka miezi miwili tutakuwa tumekwisha kumalima kazi hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, mtusaidie nadhani kuna mahali sheria haijaka vizuri, kwa maana hizi zinazoitwa nyaraka za yule anayestaafu, kuna nyaraka anaombwa mstaafu ambazo kama ulipokea michango yake nyaraka hizo unazitaka za nini? Kwa mfano mtu amefanya kazi miaka 30, anataka mafao yake anaambiwa kalete barua yako ya ajira, kalete barua ya uthibitisho, michango yake imepokelewa na taarifa zipo, hizo taarifa zinatakiwa za kazi gani? (*Makofi*)

Nafikiri kwa sababu hilo lipo kwenye sheria na kanuni zetu ni muhimu sana kulifanya kazi, wastaafu wapewe bila kusumbuliwa maadamu michango yao ipo na majina yapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tumekuwa tukifanya uhakiki wa wastaafu kwenye mifuko hii, moja ya matatizo ambayo tumeyagundua ni hayo ambayo Mheshimiwa Naibu Spika umeayazungumza

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu wamekua wakisumbuliwa sana kuleta nyaraka na wakati mwininge mstaafu anadaiwa alete nyaraka za miaka 20 iliyopita na wakati amestaafu nyaraka hizo zikiwa kwenye Ofisi za Serikali, tumeshatoa maelekezo kwa mifuko yote na hasa sheria inasema wajibu wa kufuatilia michango na nyaraka ni wamifuko na siyo mstaafu mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kazi yetu kwa sasa ni kusimamia watendaji wa hii mifuko wanatekeleza maagizo hayo tuliyoyatoa na kama kutakuwa na mstaafu anasumbuliwa yeze sasa ndiyo haangaike na ma-file wakati ni wajibu wa mwajiri na wajibu wa mifuko, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tupeane taarifa na tutachukua

hatua kwa hao watendaji ambao hawazingatii huduma bora. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 130

Bajeti ya Barabara za Newala Vijijini

MHE. MAIMUNA S. MTANDA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya barabara za Newala Vijijini ambayo imetengewa fedha za kilometra 340 wakati zina mtandao wa barabara wa kilometra 960?

(b) Je, Serikali inatoa msaada gani wa dharula kwenye matengenezo ya barabara za vijijini vinavyozungukwa na milima au mito kama vile Mkongi - Nanganga, Mikumbi - Mpanyani, Namdimba - Chiwata, Mkoma - Chimenena na Miyuyu - Ndanda?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometra 960.04. Serikali imekuwa ikiongeza fedha za bajeti ya matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya Newala mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2019/2020,

shilingi milioni 939.27 zilitengwa kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zenyе urefu wa kilometra 343.86, mwaka wa fedha 2020/2021, shilingi milioni 976.88 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara zenyе urefu wa kilometra 320.38.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.056 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara zenyе urefu wa kilometra 277.35 na ujenzi wa mifereji yenye urefu wa kilometra 1.37.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 barabara ya Mkwiti - Lochino - Nyangao yenye urefu wa kilometra 11.1 imefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 84.78. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 barabara hii imetengewa shilingi milioni 56.32. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 87 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Maputi – Mikumbi – Miyuyu – Ndanda Kibaoni yenye urefu wa kilometra 17.5 ikiwa sehemu ya kipande cha Mlima Miyuyu – Ndanda na shilingi milioni 56 kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofи yenye urefu wa kilometra 3.5 ili iweze kuitika hadi Kijiji cha Lochino.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Wazir nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara Miyuyu - Ndanda kimekuwa kimetengewa fedha mara kwa mara za matengenezo ya kawaida, lakini fedha hizo hazitibu shida iliyoko kwenye mlima pale na barabara ile ni barabara ambayo inatumika kwa wagonjwa kutoka Wilaya za Newala na Tandahimba wanaopata rufaa kwenda Hospitali ya Ndanda. Hali ya pale ni mbaya, ni mlima kumbwa na korongo kubwa kiasi kwamba inahatarisha usalama kwa watumiaji wa barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata kauli ya Serikali. Ni lini itajenga kwa kiwango cha lami barabara ile hasa kipande kile ili wananchi wanaotumia hospitali ya Ndanda kama hospitali ya Rufaa waweze kupata urahisi wa kufika hospitalini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Jimbo la Newala Vijijini, zimesababisha athari kubwa sana ya barabara kukatika magari hayapiti, hata pipipiki zinapita kwa shida, kwa mfano barabara kutoka Malatu Shulen - Namkonda hadi Chitekete, barabara ya Maputi - Meta, barabara ya Likwaya Nambali, barabara ya Mtikwichini - Chikalule, barabara ya Mtikwichini - Lochino na Chikalule.

Mheshimiwa Naibu Spika, upi mpango wa Serikali wa kupeleka fedha kwa ajilli ya dharura ya kutengeneza barabara hizo ambazo kwa sasa hazipitiki? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge aliuliza eneo korofii la Mlima Miyuyu mpaka Ndanda na amesema kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha, lakini bahati mbaya tatizo hilo limekuwa halitatuliki, kwa hiyo, alikuwa anaiomba Serikali ni lini itajenga lami katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu peke ninachowezza kumuhakikishia ni kwamba kutokana na ombi aliloliletii na sisi Ofisi ya Rais - TAMISEMI tutakwenda tufanye tathimini na baada ya hapo tualeta majibu ya eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini sehemu ya pili barabara ambazo amejaribu kuzitaja Mheshimiwa Mbunge ambaye ninaamini anafanya kazi hii kwa nia njema ya kusaidia wananchi wake wa Jimbo la Newala, ameainisha maeneo mengi sana na kutaka mpango wa dharura na lenyewe nimuhakikishie kwamba Serikali tumesikia na kwa sababu katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha yakiwemo hayo maeneo ambayo ameyainisha, Iakini Serikali inaendelea na mchakato wa kutafuta vyanzo vingine.

Kwa hiyo kulingana na bajeti itakavyopatikana na sisi tutaakikisha kabisa kwamba tunatatua matatizo ya wananchi wa Newala na maeneo mengine ya Tanzania. Kwa hiyo, ahsante sana Mheshimiwa Mbunge tumepokea maombi yako na nikupongeze kwa kazi nzuri kwa wananchi wako, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 131

**Hitaji la Vitendea kazi – Kituo cha Afya
Mtii - Same Mashariki**

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vitendea kazi Kituo cha Afya Kata ya Mtii, Jimbo la Same Mashariki baada ya kukamilika kwa vyumba 12 vya Jengo la *OPD*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweka kumbukumbu sahihi kwanza naomba nianze kwa ufanuzi kwamba jengo linalojengwa eneo la Mtii ni zahanati na si kituo cha afya. (*Makof!*)

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati ya mpya inayojengwa kwa nguvu za wananchi, fedha za Mfuko wa Jimbo, wadau wa maendeelo pamoja na fedha za Halmashauri. Majengo yanayojengwa ni pamoja na Jengo la Wagonjwa wa Nje na Jengo la Huduma ya Kliniki ya Afya ya Mama na Mtoto ambayo tayari yamekamilika na ujenzi wa Jengo la Huduma za Uzazi unaendelea. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Same imepokea fedha shilingi milioni 150 iliyotengwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo Zahanati ya Mtii imepokea shilingi milioni 50 itakayotumika kukamilisha Jengo la Wazazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Mtii itakapokamilika itapatiwa usajili na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kuwekewa utaratibu wa kupatiwa vitendea kazi.

Aidha, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele cha ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya vilivyojengwa na kukarabatiwa na kote nchini, vikiwemo Vituo vya Afya vya Ndungu, Shengena na Kisiwani ambavyo vimepokea shilingi milioni 400 kila kimoja na Zahanati ya Kasapo iliyopokea shilingi milioni 154 vilivyoko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Same ambavyo tayari vimepokea fedha hizo na shughuli za ujenzi zinaendelea ujenzi na ukarabati wa vituo hivyo umekamilika na huduma sasa zinatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Same iweke kipaumbele kwa kutenga bajeti kwa kupitia mapato yake ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba nya zahanati mpya ya Mtii pindi itakapokamailika na kupatiwa usajili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza samahani maana niliona nisahishe, Naibu Waziri lakini kwa vile ameendelea haina neno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utata kutoka Serikalini *documents* tulizonazo nilizopewa nilipokuwa Mbunge wa Jimbo mwaka 2015 mpaka 2020 zilionesha kinachojengwa ni Kituo cha Afya, na hata ramani hii imetoka Wizara ya Afya na inaonesha *OPD* inayojengwa na wananchi wanajua hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe kwa vile kumekuwa na ubabaishaji mkubwa katika Wilaya ya Same Halmashauri ile, kwamba mambo yanabadilishiwa hewa *gear* zinabadilishiwa hewani nikuombe nikae na Wizara ili tuweze kujua kwamba hizi *documents* zimetoka wapi na nina ramani zote za jengo ambalo lilikuwa lijengwe Kituo cha Afya lakini sinazo.

Kwa hiyo, nikuombe tumalizie mjadala hapa ili niwasiliane na Wizara wao wanajua kwamba je tuwe tunaongea kwenye *same level* kwamba je tunazungumizia zahanati au Kituo cha Afya? Maana hata swali la nyongeza nkiuliza litakuwa *off sides* sana, halitaendana majibu ya Naibu Waziri. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana maombi yako Mheshimiwa Mbunge yamekubaliwa, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri utaonana na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum ili mjadili kuhusu hilo jambo. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru sana wananchi wa Kata ya Mtikwa kunipa kura nyalingi sana bila shuruti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuuliza swalii la nyongeza kwa kuwa jumatatu ya pasaka mimi na Naibu Waziri wa Afya tulikwenda kuiona zahanati hii ya Kata ya Mtii na kwa kuwa wananchi wale wamefanya jitihada, niliyeanza kujenga ile zahanati ni mimi na wananchi, sasa wananchi walichomililia Naibu Waziri wa Afya, wanaomba wajengewe nyumba ya Mganga.

Je, Serikali hamuoni kwamba wananchi wangu wamejitalidi sana kujenga zahanati ile wao wenye na Mbunge wao na Mbunge alipokuja aliweka kitu kidogo mkatusaidia kujenga nyumba ya mganga wa zahanati ile? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swalii hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):- Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Anne Kilango Malecela na wananchi wa Jimbo la Same Mashariki kwa kazi kubwa walioifanya kuanzaujenzi wa Zahanati ya Mtii, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge amekuwa karibu sana na wananchi, amefanya ziara pale na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na wameona kazi nzuri inayoendelea na wananchi wanatambua mchango mkubwa wa Serikali ambao unaendelea kutolewa katika ujenzi wa zahanati ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyojobu kwenye swalii la msingi

tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya Zahanati ya Mtii, lakini pamoja na kuweka bajeti kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mganga katika zahanati ile. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Njombe Mjini na sisi tuna Kituo cha Afya ambacho kina uhitaji wa wodi ya kibaba na wazazi na huduma ya upasuaji na Serikali ilishaonesha nia ya kutusaidia.

Swali, je, ni lini sasa shughuli ya ujenzi na ukarabati wa kituo cha afya cha muda mrefu sana Njombe Mjini utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Jimbo la Njombe Mjini kuna Kituo cha Afya cha Mji Mwema na cha siku nyingi ambacho kina uhitaji mkubwa wa miundombinu ya wodi ya akina baba akina mama lakini na wodi ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kwenda pia kuongeza miundombinu katika Vituo vyaa Afya na

nimuhakikishie kwamba Kituo cha Afya cha Mji Mwema katika Jimbo la Njombe Mjini nacho kitapewa kipaumbele.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Mheshimiwa Zuwena Athumani Bushiri Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swlai lake.

Na. 132

Kukamilika kwa Jengo la Mama na Mtoto - Hospitali ya Mawenzi

MHE. ZUENA A. BUSHIRI aliuliza:-

Je, lini Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Mawenzi litakamilika na kuanza kutoa huduma stahiki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbuge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la kuwahudumia mama na mtoto ambalo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 70. Mradi huo unagharimu jumla ya shilingi bilioni 10.5 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 5.3 kimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha dhilingi bilioni 57 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mawenzi ambayo imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kukamilisha

ujenzi na shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya vifaa na vifaatiba. Aidha, huduma zitaanza kutolewa baada ya kukamilika kwa ujenzi na ukamilishaji usimikaji wa vifaa ifikapo Januari, 2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuena Bushiri swali la nyongeza

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mawenzi ilianza kama zahanati mnamo mwaka 1920 ikapandishwa daraja ikawa Kituo cha Afya mwaka 1922, ikapandishwa daraja ikawa Hospitali ya Mkoa mwaka 1956, mwaka 2011 ikapanda daraja kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hospitali hii inahudumia Wilaya zote saba za Mkoa wa Kilimanjaro, lakini ina upungufu wa Madaktari Bingwa hususani upande wa wanawake.

Je, Serikali inasema nini kuhusu kuongeza madaktari bingwa wa Hospitali hii kwa sababu huduma stahiki wananchi wa Kilimanjaro hawazipati kutokana na ukosefu wa madaktari na madaktari bingwa?

Kutokana na miundombinu hii ilioanza tangu mwaka 1920 ni kweli kabisa hospitali ile imechoka, mazingira...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati na kujenga majengo ambayo yana hadhi ya kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake

mzuri sana hasa kwenye eneo la hospitali hiyo, lakini kwa ufuatiliaji wake mzuri hasa kwenye huduma ya akina mama na watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni kuhusu Madaktari Bingwa kwenye Hospitali ya Mkoa wa Mawenzi hospitali hiyo mpaka sasa ina *ma-specialist*, tisa lakini *specifically* idara anayoisema Mheshimiwa Mbunge ambayo inahitajika kuwa na Madaktari Bingwa wanne ina Daktari Bingwa mmoja. Kwa hiyo, ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge wakati tunajipanga kwa mwaka huu kwa maana ya ajira za mwaka huu Hospitali ya Mawenzi itakuwa mojawapo ya hospitali za kipumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sivyo tu kwamba kuna *ma-specialist* tisa, lakini kuna baadhi ya Idara kama Idara ya Mifupa ambayo halfanyi vizuri sana, tutaenda kufanya kazi kubwa kwenye kuboresha hasa kuweka kwenye vifaa, lakini kuelekeza utawala wa hospitali ili usimamie vizuri eneo hili liwe kufanya kupunguza rufaa kwenda KCMC.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pilli ni kuhusu miundombinu kwamba hospitali ni ya muda mrefu na kuna majengo ambayo yamechakaa na mengine kabisa hayafai kutumika. Ni kweli kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema na baada yeye kuja Wizarani, Mheshimiwa Waziri wa Afya alituma timu wiki mbili zilizopita, wameshakwenda Mawenzi na sasa wako kwenye hali ya kuangalia yale majengo ambayo hayafai kabisa na michoro imeanza kuchorwa ili kuja na mawazo ya namna gani tunaweza kuboresha hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini kuna suala la ardhi pembedi ya Hospitali ya Mawenzi kuna ardhi ya Manispaa ambayo tunaweza tukafikiria namna ya kushirikiana na Manispaa kama inawezekana, lakini ukiangalia ramani yamwaka 1959 Hospitali ya Mawenzi na ukiangalia mabadiliko ya 2009 utaona kuna maeneo fulani ya hospitali hiyo ambayo vilevile hayaonekani kwenye ramani nayo yatashughulikiwa kuhakikisha sasa tunaenda kuja na mkakati

ambao hospitali hiyo itaboreshwa vizuri sana, ahsante sana.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swali lake.

Na. 133

Mlipuko wa Magonjwa ya Nguruwe

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa mlipuko wa magonjwa ya nguruwe hayajitokezi mara kwa mara nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hivi karibuni kulijitokeza mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe katika mikoa kadhaa nchini na kusababisha hasara kwa wafugaji. Ugonjwa huu unaosababishwa na virusi, hauna chanjo wala tiba. Njia pekee za kudhibiti ugonjwa wa homa ya nguruwe ni kuzingatia kanuni bora za ufugaji wa nguruwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na wadau wengine inafanya jitihada za kudhibiti ugonjwa huu, jitihada hizo ni pamoja na:-

(i) Kuhimiza wafugaji kuacha kufuga nguruwe kwa njia huria;

- (ii) Kuzuia wageni kuingia kwenye mabanda ya nguruwe;
- (iii) Kuhimiza wafugaji wapulizie dawa za kuua virusi na kupe kwenye mabanda na kuweka dawa ya kuchovya kwenye milango ya mabanda;
- (iv) Kuweka katazo la kusafirisha nguruwe na mazao yake kutoka sehemu zenyen ugonjwa;
- (v) Kuhimiza wafugaji kutokuruhusu wachinjaji au wafanyabiashara kuingia katika mabanda na kuchagua nguruwe wa kununua;
- (vi) Kuepuke kulisha nguruwe mabaki ya vyakula kutoka kwenye mahoteli na migahawa;
- (vii) Kuacha kuchanganya nguruwe wageni na wenyeji kwenye banda moja; na
- (viii) Wafugaji kutoa taarifa za ugonjwa au vifo vya nguruwe pindi inapojoitokeza kwa mtaalamu wa mifugo aliye karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kuitia Wizara ni kuendelea kutoa elimu ya udhibiti kwa wadau wote katika mnyororo wa thamani, wakiwemo wafanyabiashara na wasafirishaji wa nguruwe pamoja na watoa huduma za afya ya mifugo. Kazi hii tunaendelea kuifanya kwa kuzingatia uhalisia katika kila eneo kwa wafugaji wakubwa na wadogo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo, naomba nipate nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, sekta ya nguruwe sasa imekuwa ikikuwa kwa kasi kubwa sana na hapa nchini na kwamba ufugaji wa nguruwe ni rahisi kidogo kuliko mifugo mingine kwa sababu wanatunzwa ndani ukilinganishwa na ng'ombe, sasa kumekuwa na *incentives* mbalimbali zinazotolewa kwenye mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye bidhaa zinazosaidia kwenye ufugaji wa nyuki, samaki, kuku ng'ombe na mifugo mingine zina nafuu ya kodi. Je, kwa sababu sekta hii nayo inahitaji kuboreshwa na kuwa ya kisasa zaidi Serikali haioni kuna haja ya kutoa *incentives* kwenye vifaa vinavyotumika kwenye ufugaji wa nguruwe kwenye eneo la kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na muingiliano mkubwa sana kwenye sekta ya nyama, huko utakutana na watu wa *NEMC* utakutana na watu wa *TBS*, ambao wanashughulika machinjio wengine usafirishaji, na wengine ubora wa nyama kitu ambacho kinasababisha mazao ya nyama kuwa na gharama kubwa sana ambayo Watanzania wengi hawawezi ku-*afford* kununua na kilo bei ya nyama ukiangalia katika mchanganuo wake gharama ya uununuzi inatokana mwingiliano huu wa mamlaka mbalimbali zinazosimamia suala la nyama sasa swali langu.

Sasa swali langu, Serikali haioni haja ya kuhamisha shughuli zote zinazofanywa na idara mbalimbali ili zikasimamiwe na Wizara na Mifugo ambayo yenyewe ndio yenyewe uwezo mkubwa sana wa kusimamia kutokana na utaalamu uliopo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Mifugo na Uvumi Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni juu ya *incentives* kwa ajili ya wafugaji wa nguruwe kama ambavyo wanapata wafugaji wengine. Naomba niichukue rai hii ya Mheshimiwa Mwambe ya kwamba Serikali tuitazame ufugaji wa nguruwe na kwa kuwa tuo kwenye kipindi cha bajeti jambo hili limekuja kwa wakati muafaka na Serikali tunalichukua, litatazamwa katika vikao vyetu kadri itakavyoonekana inafaa, wataalam pamoja nasi viongozi tutashauriana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ukuaji wa tasnia hii ya nguruwe inakwenda sambasamba na ukuaji wa mifugo mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ameuliza juu ya suala zima la muingiliano mkubwa wa taasisi mbalimbali za Serikali unaopelekea kupandisha bei ya nyama na mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu iliyopita Serikali ilifanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba tunaunganisha vyombo vyetu vinavyosimamia tasnia zetu hizi, kwa mfano baadhi ya mazao yatazamwe na moja tu katika taasisi, miaka michache iliyopita tuliamua kwa dhati kabisa kwamba *TMDA* itatazama vyakula na kwa upande wa mazao ya mifugo yatatazamwa na wataalam wenyewe wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie ya kwamba rai yako yakuondoa mgongano huu wa kitaasisi na la lenyewe tumelichukua kwa kusudio la kupunguza changamoto inayowapata wafanyabiashara wa mazao ya mifugo na wafugaji pia vilevile. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza

MHE. SEIF K. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo na milipuko ya magonjwa kwenye mifugo, nini mpango wa

Serikali wa kujenga majosho katika Wilaya ambazo zina mifugo mingi hususani Wilaya ya Igunga kutuwekea majosho kwenye mihada na vijiji? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA:Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Seif Gulamani, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga vyema katika kuhakikisha kwamba tunajenga majosho ya kutosha katika vijiji na Wilaya mbalimbali nchini. Katika mwaka huu tunaokwenda nao wa 2020/2021 Wilaya ya Igunga kwa maana ya Jimbo la Manonga ni mliongoni mwa maeneo yatakayopata fursa ya kujengewa majosho, tena utapata pale majosho mawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile habari njema kwa Waheshimiwa Wabunge wote; mkakati wa Serikali katika muda wa miaka hii mitano, baada ya kuwa tumefanikiwa sana katika zoezi letu la uogeshaji wa mifugo na kupunguza sana magonjwa yanayoambukizwa kupitia kupe, tutaendelea na zoezi hili la uogeshaji na kwa kujenga majosho ya kutosha. Tunataka kila kijiji ambacho kina wafugaji kipate joshio na kwa hiyo tunaomba sana mtuunge mkono katika kuhakikisha kwamba zoezi hili linafanikiwa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 134

Kupima na Kurasimisha Maeneo ya Miji

MHE. PRISCUS J. TARIMO aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kupima na kurasimisha maeneo yanayozunguka Mamlaka za Miji ili kuepuka kuendelea kuwa na makazi holela pamoja na kuweza kupeleka huduma za dharura kama *ambulance* na zimamoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba njibу swalı la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Sura ya 355 Fungu la 7(1), mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya nchini zina wajibu wa kupanga, kupima na kurasimisha maeneo yote yaliyo chini ya mamlaka zao. Pamoja na wajibu huo wa kisheria kwa mamlaka za upangaji, bado kasi ya upangaji na upimaji ardhi nchini imekuwa sio ya kuridhisha. Hivyo, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji pamoja na taasisi binafsi katika utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasi ndogo ya upangaji na upimaji, katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 Wizara yangu imeziwezesha mamlaka za upangaji 21 nchini kupanga na kupima viwanja vipatavyo 56,792 kwa gharama ya shilingi billioni 3.5. Lengo la kutoa fedha hizo ni kuziwezesha mamlaka za upangaji kuongeza wigo wa upatikanaji wa viwanja vilivyopangwa na kupimwa katika maeneo yao na kurasimisha makazi mijini. Pamoja na kupatiwa fedha hizo, jumla ya makazi yapatayo 735,047 yamerasimishwa nchini katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 katika Halmashauri 104 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yote yaliyopangwa, kupimwa na kurasimishwa, utengaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi ya umma umezingatiwa ili kuruhusu utoaji wa huduma za kijamii. Natoa rai kwa mamlaka za upangaji nchini kuhakikisha zinatenga fedha katika bajeti zao kila mwaka ili kuharakisha upangaji, upimaji ardhi na urasimishaji wa makazi katika maeneo yao. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Wizara, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Manispaa ya Moshi ndiyo manispaa ndogo zaalid Tanzania yenye kilometra za mraba 58; na kwa kuwa upanuzi wa makazi na shughuli za kiuchumi ambazo zinasababisha ukuaji wa mji ule zinakwenda kugusa mamlaka za sehemu nyingine ambazo watendaji wa Wilaya ile hawana mamlaka nazo.

Nini nafasi ya Serikali katika kurasimisha maeneo hayo kabla ujenzi holela haujaendelea?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Mabula, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Manispaa ya Moshi ina eneo dogo, na katika kupanuka kwake inabidi iguse na maeneo mengine ambayo yako nje ya utawala wa Manispaa ya Moshi. Lakini taratibu za Serikali ziko wazi, pale ambapo maeneo ya utawala yanatakiwa kuongezwa ama

kupunguzwa, taratibu lazima zifuatwe kuitia Wizara ya TAMISEMI ili kuweza kujua uhalali wa kuweza kuongeza eneo wawze kupata kama wanavyohitaji. Vinginevyo hawawezi kufanya zoezi katika eneo ambalo si la Manispaa, isipokuwa waliopo *Moshi DC* wanaweza wakafanya zoezi la urasimishaji na kupanga maeneo yao kutokana na sheria inayo...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji; Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 135

Kukamilisha Mradi wa Maji Kintinku – Lusilile Manyoni

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Kintinku – Lusilile ili wananchi wa vijiji 11 vya Kata za Chikuyu, Makutupora, Maweni na Kintinku waanze kupata maji safi na salama?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Kintinku-Lusilile ni mradi mkubwa ambao unatekelezwa kwa awamu nne na hadi mwezi Machi, 2021 utekelezaji wa awamu ya kwanza umefikia asilimia 90 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.085. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ufungaji wa mitambo ya kusukuma maji, ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji, tanki la kukusanya maji la lita 300,000 na ujenzi wa tanki la kuhifadhi na kusambaza maji la lita milioni mbili

na ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilometra 1.2. Aidha, vijiji vitatu vya Chikuyu, Mwiboo na Mbwasa vinatarajiwa kuanza kupata huduma ya maji mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia *RUWASA* imepanga kukamilisha usambazaji wa maji katika vijiji vyote 11 katika mwaka wa fedha 2021/22 na utahudumia wakazi zaidi ya 55,000.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu mradi umechukua muda mrefu sana, zaidi ya miaka kumi, kukamilika, na kwa kuwa Waziri ameahidi kwamba ndani ya huu mwaka mmoja huu mradi unakuja kukamilika; ninapenda kujua sasa Wizara inakuja na mikakati gani ndani ya huu mwaka mmoja kuhakikisha maji yanafika katika vijiji 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kwa kuwa huu mradi vilevile unanufaisha kata tatu ambazo zina miradi mikubwa ya kimkakati ukiwepo mradi wa ujenzi wa reli lakini vilevile na kituo cha afya. Je, Serikali haloni sasa kuna umuhimu wa haraka kupeleka maji katika Kata ya Kintinku na Maweni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri wangu kwa kazi kubwa na nzuri namna anavyojibu maswali yake, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara katika Mradi wa Kintiku-Lusilile, ni mradi ambaao umechukua muda mrefu

sana na mkandarasi alikuwa akidai kiasi cha pesa. Tumeweza kumlipa kiasi cha shilingi milioni 500, lakini pia tumepokea fedha shilingi bilioni 25, kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi. Nataka nimhakikishie mmoja wa wakandarasi ambao watalipwa fedha ni Mradi huu wa Kintiku-Lusilile. Kwa hiyo maelekezo ya Wizara na wakandarasi wote watakaopata fedha ni kuhakikisha wanakamilisha miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako nataka niliambie Bunge lako Tukufu jana Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo mahususi katika Wizara yetu ya Maji, na sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji tumeyapokea na tutayafanya kazi kikamilifu. Lakini naomba nitume salamu kwa wahandisi wa maji pamoja na wakandarasi; wakae mguu sawa, na sisi tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Haya, naona hotuba ya Mheshimiwa Rais Samia imeshaanza kufanyiwa kazi humu ndani.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 136

Ukarabati wa Uwanja wa Ndege – Same

MHE. DKT. DAVID M. DAVID Aliuliza:-

Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi huchangia Pato la Taifa kutokana na shughuli za utalii.

Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kuukarabati Uwanja wa Ndege wa Same Mjini ili ndege ndogo na za kati ziweze kutua kuleta watalii wa ndani na nje ya nchi katika Hifadhi ya Mkomazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushauri wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kuhusu ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Same, Serikali itaangalia uwezekano wa kukifanyia ukarabati kiwanja hicho kwa kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuongeza Pato la Taifa kuititia sekta ya utalii. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani kwamba majibu haya kidogo sijaridhika sana, lakini niseme ni mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, faru weusi pamoja na wanyama wengine wanapatikana katika Hifadhi za Taifa tatu tu katika nchi hii zikiwemo Serengeti, Ngorongoro pamoja na Hifadhi ya Mkomazi. Upande wa Kenya wana kiwanja cha ndege pale Tsavo, upande wa Kenya Hifadhi ya Tsavo ndiyo inayopakana na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, na hivyo wanapata watalii wengi kwa sababu wao wana kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile umbali wa kutoka Arusha na K/A ni mkubwa sana ukizingatia na uhitaji wa watalii kuja kuona faru weusi walioko kwenye *sanctuary* pale *Mkomazi National Park*. (*Makofii*)

Ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kukarabati Uwanja wa Ndege wa Same ili watalii hao waweze kufika kwa urahisi na kuongeza Pato la Taifa kama Mheshimiwa Rais alivyosema jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, ninaomba inapowezekana Mheshimiwa Waziri aje pale Same ili aweze kuona mazingira hayo ninayozungumzia, kwamba uwanja upo unahitaji marekebisho ili tuweze kukuza uchumi kuititia utalii. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta wazo zuri sana ambalo kimsingi siyo la Same Magharibi peke yake, hili ni jambo la Kitaifa.

Ninaomba nitumie nafasi hii kumuelekeza Katibu Mkuu Ujenzi na Uchukuzi, Sekta ya Uchukuzi, awatume wataalam wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege waende Same Magharibi wafanye tathmini, tuangalie *cost implication* ili kiwanja hiki kikarabatiwe mapema iwezakanavyo, fedha itakapopatikana kuitia watalii katika eneo hili itasaidia kuboresha hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya jana ya kuendeleza miradi mbalimbali ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kabla Bunge hili halijaisha naomba kibali cha Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, twende Sa me kwa sababu kuona ni kuamini, tushuhudie hali halisi na tuongeze maelekezo ya ziada. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana; Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 137

Ukosefu wa Usafiri Salama na Uhakika

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE aliuliza:-

Visiwa vilivyopo katika Ziwa Victoria, Wilayani Muleba havina usafiri salama na wa uhakika, na vilevile Bandari Ndogo ya Kyamkwikwi haina miundombinu stahili.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka kivuko ili kurahisisha usafiri kati ya Visiwa vilivyopo Ziwa Victoria na Miji ya Mwambao ya Ziwa hilo Wilayani Muleba?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu muhimu ikiwemo maghala ya kuhifadhiya bidhaa katika Bandari Ndogo ya Kyamkwikwi ili kuwavutia wafanyabiashara kutumia bandari hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Sekta ya Uchukuzi tayari imepeleka wataalam maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria, hususan Wilaya ya Muleba kufanya tathimini ya maeneo yanayofaa kuwekewa huduma ya usafiri wa vivuko. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Sekta

ya Ujenzi, imetenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maegesho ya Muleba – Ikuza na Ngara – Nyakiziba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali kwa kuuona umuhimu wa huduma hiyo kwa wananchi wa maeneo hayo, inaangalia uwezekano wa kuboresha huduma za usafiri zinazotolewa na Kivuko MV Chato II – Hapa Kazi Tu, kwa kuongeza njia (*route*) ya kutoka Chato hadi kwenye visiwa vinyavyoweza kufikiwa na kivuko hicho katika Wilaya ya Muleba.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) imekamilisha zoezi la utwaaji wa ardhi katika Bandari Ndogo ya Kyamkwikwi kwa lengo la kujenga miundombinu muhimu ili kuwavutia wafanyabiashara pamoja na kutoa huduma za usafiri wa kuelekea maeneo mengine ya Ziwa Victoria kupitia Bandari hiyo. Hadi sasa kazi ya kuainisha mahitaji ya miundombinu inayofaa kujengwa katika Bandari hiyo imekamilika. Miundombinu husika ni pamoja na ghala la kuhifadhi mizigo, jengo la kupumzikia abiria, kantini na chumba cha walinzi. Utekelezaji wa mradi huu unatarajia kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Charles Mwijage, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuwa umekamilisha kumlipa mtu fidia unapoweka pesa kwenye akaunti yake. Kwa nini sasa Serikali isiwalipe wananchi wa Kyamkwikwi kwa kuhakikisha pesa zinaingia kwenye akaunti zao kabla ya mwisho wa mwezi huu ili jibu la Mheshimiwa Waziri liweze kuwa sahihi? Hawa watu hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; tunapozungumza Bandari ya Kyamkwikwi tunamaanisha huduma kwa Visiwa nya Bumbile, Makibwa, Nyaburo, Kerebe na Gooziba. Sasa kwa nini Serikali isichukue maoni ya wananchi waliyoyatoa kwa Kepteni Mwita wa MV Clarias juu ya chombo muafaka cha kuweza kwenda katika hivyo visiwa nilivyovirejea? Kwa sababu unapozungumzia MV Chato, MV Chato haiwezi kupita kwenye mkondo wa Makibwa kuelekea Kerebe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI(MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu maswali mawilli ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuelekeze Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi atumie wataalam wake atueleze *statusya fidia* ya wananchi hawa, itakapofika Bunge la jioni Mheshimiwa Mbunge atapewa majibu sahihi ni lini wananchi wake watalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili Mheshimiwa Mbunge anasema ni kwa nini tusichukue maoni ya wananchi waliyotoa kwa Kepteni Mwita kama alivyotaja, ili yaweze kufanyiwa kazi kwa lengo kubwa la kuboresha huduma ya usafiri katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuyapokee maoni haya tuyafanyie kazi, yapitiwe na wataalam wetu tupate ushauri sanifu ili tuweze kutekeleza kama ambavyo tunapaswa kukidhi mahitaji ya wananchi. Kwa sababu lengo la Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi ni kuhudumia wananchi, tena wananchi wale amba wana uhitaji mkubwa hasa wa pale Muleba Kusini na Kaskazini.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tumalize swalii la mwisho, Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 138

Soko la Asali Nje ya Nchi

MHE. JACQUELINE K. ANDREA aliliza: -

Je, ni lini Serikali italiangalia zao la asali na kulitafutia soko la uhakika ndani na nje ya nchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, asali ni mojawapo ya mazao yanayozalishwa na nyuki, mazao mengine ni pamoja na nta, gundi ya nyuki, sumu ya nyuki, chavua na maziwa ya nyuki. Wizara imeendelea na jitihada za kutangaza mazao ya nyuki ya Tanzania kwa kushirikiana na *TANTRADE* kwenye mikutano mbalimbali ya kibashara, maonyesho, warsha na makongamano yanayofanyika ndani na nje ya nchi pamoja na Balozi zetu zilizopo katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa uzalishaji wa asili nchini ni wastani wa tani 30,400; sehemu kubwa ya asali hiyo zaidi ya asilimia 95 huuzwa katika soko la hapa nchini na asilimia tano huuzwa kwenye soko la nje kwenye nchi za Rwanda, Kenya, Burundi, Umoja wa Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Kiarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ukarabati pamoja na ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki katika Mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma na Geita ambavyo vitatumika kama soko la mazao ya nyuki. Serikali pia imeweka mfumo wa ufuatiliaji wa mazao ya nyuki katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao hayo kwa lengo la kuthibiti viwango vya ubora wa mazao ya nyuki pamoja na kufufua, kuendeleza na kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa ufugaji nyuki ili kuunganisha nguvu za uzalishaji pamoja na soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa soko la mazao ya nyuki kupitia mradi mpya wa kusaidia mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki utakaoteklezwa kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, swali la nyongeza.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na jitihada nzuri za Wizara inavyofanya kuzitangaza zao la asali nchini, lakini bado hatujafanya vizuri kwa masoko ya nje ambayo inapelekea wafanyabiashara wengi wa nchini wanashindwa kufanya vizuri kwa masoko ya nje hususan ni Mkoa wa Tabora na tukiangalia kinamama wengi wa Mkoa wa Tabora wamejikita kwenye uvunaji wa asali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara inakuja na mkakati upi kuhakikisha soko la nje la zao la asali linafanya vizuri kama ambavyo zao la asali linafanya vizuri ndani ya nchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, pamoja na jitihada nzuri zinazofanya na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuhakikisha zao la asali linaendelea kuwa na thamani, mpaka kupata wafadhili kutoka Umoja wa Ulaya.

Je, Wizara imeweka mikakati ipi na mipango madhubuti ya kutenga pesa kwa ajili ya kuhakikisha mradi huu walioweka kusaidiwa na Umoja wa Ulaya unaweza kuendelea hata kama mradi ule, hata kama wafadhali watachelewesha pesa au hawatoleta pesa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline, Mbunge wa Viti Maalum Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mbunge wa Viti Maalum Mkao wa Tabora Mheshimiwa Jacqueline kwa kuona umuhimu wa zao hili la asali. Ni kweli Tanzania tunafaidika kwa asilimia kubwa kwa soko hili la asali kuuza ndani na nje ya nchi. Mkakatiki wa Wizara na Serikali kwa ujumla ni kuhakikisha kwamba asali yetu inakuwa na ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kwa sasa hivi wizara inashikirikiana na Umoja wa Ulaya ikiwemo Ujerumanii kupeleka sampuli za kemikali za asali ambazo huwa zinachakatwa na kuangalia ubora wa asali ya Tanzania. Na kwa asilimia 90 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 tulipeleka asali yetu ya Tanzania na ikaonekana kwa asilimia 90 ni nzuri na inafaa kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania sasa itaanza kupeleka asali kwenye nchi za Ulaya na Marekani kwa kuwa tumekidhi vigezo vya viwango vya ubora wa asali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwenye mikakati ya kutenga fedha nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sasa tuna mkakati wa kuanzisha viwanda vitano. Viwanda vitatu tayari

vimeshajengwa na viwili tunakarabati. Lakini pia hii ni mwanzo wa kuhakikisha kwamba tayari tuna vyanzo vyetu sisi wenyewe bila kutegemea misaada mingine ambavyo vitawenza kukusanya asali yote nchini na itachakatwa kwenye viwanda hivi na kuhakikisha soko la ubora wa asali linapatikana na tunawenza kuza nje na ndani ya nchi. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Robert Maboto swali la nyongeza.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya *TANAPA* Kanda ya Magharibi yako Bunda; na kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Bunda ilitoa eneo kwa ajili ya kujenga ofisi zao za Kanda ya Magharibi. Je, ni lini *TANAPA* wataanza kujenga ofisi hizo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimshukuru Mheshimiwa Robert Maboto kwa swali lake hilo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* ina kanda nyingi nchi nzima na kila kanda inahitaji fedha ili tuweze kujenga miundombinu husika. Katika bajeti ambayo tutaileta mwaka huu tumeomba fedha kutoka Hazina ambazo ni mahsus kwa ajili ya kujenga na kuboresha miundombinu ikiwemo Ofisi ya Kanda ya *TANAPA* pale Bunda.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa muda wetu wa maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka kwa Serikali umekwisha. Nitaleta matangazo kwenu, lakini kabla ya matangazo nimuombe Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake wote humu ndani utafute namna tuanze yale mafunzo yetu. Tuanze mafunzo ya ili Wabunge wanapouliza maswali wawe

huru, asiwe anawaza kuna mtu mwagine atataka swalii la nyongeza. Namna yetu ya kuuliza maswali ndiyo inayoleta hizi changamoto. (*Makof!*)

Humu ndani kukiwa na Mbunge wa Jimbo fulani halafu wewe ukasema kwa niaba ya Jimbo fulani inaleta mtihani, lakini haya ni mambo ya kujifunza ambayo wapo Wabunge wanaouliza maswali ya jumla na hayaleti shida ya Wabunge wapo wangapi kutoka eneo fulani. Sasa tusije wenyewe badala ya kuwaaletea wananchi maendeleo tukawa wenyewe humu ndani tunakazi kila siku ya kuzima moto nani ameanzisha moto, nani anataka kuzima. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao wametufikia siku ya leo; wapo wageni ambao wapo, hapa wanasema Jukwaa la Spika lakini sioni wageni wao Jukwaa la Spika ambapo walitakiwa wawepo wageni kutoka *Guarant Trust Bank Tanzania Limited* ya Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Jubliry Adenigya na Mhandisi Mbaraka Hussein. Sijui wamekaa wapi, kama wataingia baadaye basi tutakuwa tumeshawatangaza. (*Makof!*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tutaanza na wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Mkundi ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Ukerewe, karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo ambao ni walimu na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma yaani *UDOMwakiongozwa* na Ndugu Erick Nganzi, karibuni sana. (*Makof!*)

Tunaye pia mgeni mmoja wa Mheshimiwa Elias John Kwandikwa ambaye ni rafiki yake kutoka Moshi Mjini na huyu ni Ndugu George Benson Kilenga, karibu sana. (*Makof!*)

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Amsabi Mrimi ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Serengeti

wakiongozwa na Ndugu Johnson Alphonce, karibuni sana.
(Makof)

Tunao wageni wawili wa Mheshimwa Edward Olelekaita ambao ni rafiki zake kutoka Chuo cha Kimataifa cha Mafunzo ya Maendeleo na Ushirikiano cha Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makof)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dodoma na huyu ni Abdallah Suleiman, karibu sana. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao lakini ninayo matangazo mengine; tangazo moja linatoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Ofisi yake imeshapokea nakala tete ya Hotuba ya Rais ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alioitoa jana na hotuba hii imeshatumwa kwenye mfumo wa Bunge Mtandao sanduku linaitwa Hotuba ya Rais. Kwa hiyo, ukienda kwenye hilo sanduku utaikuta Hotuba ya Mheshimiwa Rais alioitoa jana.

Lakini hata hivyo, Ofisi ya Bunge inampango wa kutengeneza vitabu vya hotuba hiyo na vitakapokuwa tayari Waheshimiwa Wabunge mtakabidhiwa. Ni hotuba ya muhimu sana sana kwa nchi yetu kwa sababu inaeleza mwelekeo wa Taifa hili katika awamu hii ya sita chini ya Rais wa kwanza mwanamke nchini Tanzania. *(Makof)*

Sisi huyu tunamuita Malkia wa Nguvu kama ambavyo msamiati huu umeshika kasi sana na niwapongeze *Clouds Media Group* kwa kuuanzisha, wamefanya kazi nzuri na nimeletewa ujumbe hapa sijui na Mbunge gani, kwamba kesho kuna mambo mazito *Mlimani City*, Malkia wa Nguvu atakuwa anapewa tuzo mbalimbali huko. Kwa hiyo, wale watakaokuwa Dar es Salaam wanakaribishwa hamna kiingilio. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine hili linatoka kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria Mashindano ya Kuhifadhi *Quran* Tukufu Kitaifa Uwanja wa Jamhuri Dodoma siku ya kesho tarehe 24 Aprili, 2021. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mashindano haya ni ya muhimu sana kwa sababu mshindi atakayepatikana kesho; kwanza atapewa nyumba, mshindi wa kwanza atakayekuwa ameweza kuhifadhi Juzu 30 atapewa nyumba. (*Makofi*)

Pamoja na kupewa nyumba anapata tiketi ya kwenda kushiriki Mashindano ya Kimataifa ambayo yatafanyika Jijini Dar es Salaam.

Kwa hiyo, ni mashindano ya muhimu sana na hapa hawajaambiwa Wabunge Waislamu ni Wabunge wote kwa sababu ukienda kule kuhudhuria unajifunza mambo mengi. Mimi huwa nahudhuria na ninajifunza mambo mengi naamini Waheshimiwa Wabunge mtapata fursa hiyo, kwa hiyo, mnaalikwa siku ya kesho Uwanja wa Jamhuri Dodoma. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Muda?

NAIBU SPIKA: Muda ni kuanzia saa mbili asubuhi na inatarajiwa kuisha saa saba mchana na Mashindano ya Kimataifa yatafanyika Dar es Salaam tarehe 2 Mei, 2021 kwa hiyo watakaokuwa kule pia wanaalikwa kabisa japo kuwa tangazo litakuja siku nyingine, ila ya kesho ni muhimu kwa sababu ndiyo atapatikana mshindi wa nchi hii. Mnakaribishwa sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Baada ya kuleta matangazo hayo kwenu tuendelee na ratiba iliyo mbele yetu sasa. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuaanza uchangiaji wa hotuba ambayo ilisomwa jana hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, lakini pia Mwenyekiti wa Kamati yetu ambayo inasimamia Ofisi hii alisoma hotuba yake.

Kwa hiyo, sasa tutaanza uchangiaji na nimeshaletewa majina hapa ya wachangiaji ambao tutakuwa nao. Tutaanza na Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye ajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hii bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Nianze kwa kuwashukuru watumishi, hawa watumishi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Charles Mwijage samahani kidogo, wachangiaji kutoka CCM, viongozi wa humu ndani wamesema mtachangia dakika saba na itapigwa kengele moja. Wachangiaji kutoka upande wa walio wachache wanachangia dakika kumi. Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru watumishi wa umma. Watumishi wa umma ndiyo wapishi wakuu, ndiyo wapishi wakuu wanaofanya mambo haya tunayoyaona. Mafanikio yote yanayosemwa sisi wanasiisa tunakuwa juu na bendera, lakini mpishi mkuu ni mtumishi wa umma. Nimewashukuru watumishi wa umma kama vile nilivyowashukuru wakulima na wafanyakazi waliotuwezesha kupata chakula cha kutosha kwa miaka mitano iliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora na utumishi ni sekta muhimu, ni sekta muhimu kama ambavyo zimeanishwa katika Mpango wa Tatu wa Dira ya Taifa na Lengo la Taifa la 2025. Katika Dira ya Taifa 2025 tunazungumzia utawala bora, lakini tunazungumzia amani, utulivu na mshikamano. Huwezi kuwa na utulivu na amani kama hauna utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wananchi wanaponna amani na mshikamano ina maana nchi hii ina utawala bora. Sitachukua muda kuzungumzia suala la utawala bora kwa sababu kila mtu anafaidi amani ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie utumishi, ninayo mapendekezo, mtumishi ukitaka kumpa motisha ili aweze kufanya kazi vizuri kuna mambo muhimu ya kuongelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mapendekezo, naiomba Wizara hii ibaini mahitaji ya watendaji ya watumishi tujue tunahitaji watumishi kiasi gani; sekta ya afya, watumishi kiasi gani; sekta ya elimu, kiasi gani; ugavi wa kila namna ili tukiwa tunajua watu tunaowahitaji basi tujue mapungufu yetu ni kiasi gani ili nchi hii tuweze kuwa na walimu wanaotakiwa, waganga wanaotakiwa ili wale waliopo waweze kupata motisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shule yenye mahitaji ya walimu kumi ukitaka kuwa-*demotivate* waliopo wapange wawili. Ni kama timu ya mpira, timu ya mpira ya watu kumi na mmoja ukitaka kuwa-*demotivate* weka wacheza mpira saba hawatafanya kazi. Kwa hiyo, pamoja na miradi yetu ambayo lazima iendelee, mradi kielelezo mwagine ni kuajiri wafanyakazi wanaotakiwa kila sekta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta za uzalishaji (*the productive sectors*) hatutaweza kuzalisha kwa tija kama hatutakuwa na wagani wanaotakiwa. Kumbe Wizara hii ndiyo inahusika na kutoa na kutoa vibali, Wizara hii ndiyo

inachakata, inachakata, inachakata ule mchakato mzima wa kuajiri kwa maneno mengine ndiyo waajiri wenyewe. Kwa hiyo, katika sehemu nzuri tunayopaswa kuingalia ni hii ya watumishi na imeandikwa wala sio mjadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote ili iendelee inahitaji watu. Unaweba kuwa na madini, unaweba kuwa maji na usiendelee, lakini ukiwa na watu mfano wa Japan, Japan hawana migodi lakini wameendelee kwa sababu wana watu. Ndiyo maana katika Dira ya Taifa ya 2025 lengo letu ni kuwa na watu walioelimika na wenye uchu wa kujifunza ambayo ni kazi ya ofisi hii ambayo tunajadili bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mambo madogo ya kuangalia ni msingi, kuna suala ambalo naungana na TAMISEMI wanaposema kwamba watakapoajiri watakuwa wanawapanga watu kwenye mikoa ambako wataweza kutumika na hawataondoka mpaka baada ya miaka mitatu.

Mimi nashauri kwamba kila mkoa upangiwe *quota* yake; wafanyakazi wangapi waende kule na mtu akubali kuwa anakwenda Rukwa, anakwenda Kagera, anakwenda Dodoma, anakwenda Dar es Salaam na hatatoka si pungufu ya miaka mitano. Hii itatuondolea hii kadhia waliyoisema watu wanakwenda kuchukua *check number*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hilo nitoe angalizo kuna haja ya kujenga jamii, hapa nazungumzia ndoa changa, haja ya kujenga jamii si busara wanandoa wachanga wenye miaka miwili/mitatu mpaka kumi bwana kukaa Tabora na bibi akakaa Tanga, hii itakuja kutuletea kujenga jamii ya ajabu ajabu. Kwa hiyo pamoja na kupanga watalaan zingatia msiwape kadhia hawa wanandoa, otherwise tutakuja kuzaa watoto, unakuja mtoto unarudi nyumbani mtoto anakuita mjomba. Sasa ina maana nyumbani kila siku walikuwa wanakuja wajomba. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la ustawi; ustawi wa nchi unapaswa kuwa na nguvu kazi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage hebu subiri kidogo. Walikuwa wanakuja wajomba, kwa hiyo ni upande mmoja tu ambao unahusika au hebu weka vizuri hilo eneo kidogo. (*Kicheko*)

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kinyume cha mjomba ni nini? Napenda nikiri kwamba kwetu ni kilometra 1,600 kutoka Pwani kwa hiyo Kiswahili kilichelewa kufika. Mimi najua madhara ya wajomba. Naomba kwa ruhusa yako hilo swali linishinde, nizungumze... (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Aah, ngoja ngoja, ngoja inabidi tuweke vizuri, labda, lazima uwelewe Malkia wa Nguvu siku hizi tunatunza umalkia kwa wivu kabisa. Eeh ukituambia sisi ndiyo tunaoleta wajomba na ninyi mnaleta mashangazi kwa hiyo lazima sentensi ziwe zinanyooka vizuri. Mama pia anaweza akarudi nyumbani akaitwa shangazi. (*Makofi*)

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunifundisha msamiati, kumbe kinyume cha mjomba ni shangazi. Napenda ni kiri tena kwamba Kiswahili mimi kwangu ni tatizo, kwa hiyo hoja yangu iko palepale, kwa hawa watu wenye ndoa changa ni vizuri wakakaa pale na sasa hivi kwa hali tuliyonayo Tanzania tunao wataalam wa kutosha.

Nizungumze kuimarisha sekta ya umma, jambo ninalopendekeza kwa Serikali; watumishi wa umma wanapoanza kazi *day one* ni muhimu Serikali kuwajengea mazingira na kuwaaminisha kwamba leo ni watumishi wa umma, kesho watakuwa watamishi au wadau wa sekta nyingine. Unapokuwa wewe ni mtumishi wa umma, ujue kesho utakuwa kwenye sekta nyingine ambayo ni sekta binafsi ukiwa mwajiri au mwajiriwa; kwa hiyo mazingira yako sasa uweze kujiandaa kwa kwenda sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lengo langu ni nini! Kama sekta ya umma itastawi watu waliopo nje sekta ya umma watajenga wivu wa kuingia katika sekta ya umma, lakini na

wa sekta umma sasa watajenga wivu na wataitendea sawia sekta binafsi. Watumishi wa umma wasiojua kwamba siku nyingine watakuwa watumishi wa sekta binafsi huwaangalia kwa jicho baya watu ambao ni wa sekta binafsi. Kwa hiyo, ukiwa umekaa kwenye sekta ya umma ujue ipo siku na wewe utakwenda kwenye sekta binafsi ukiwa mwajiriwa au ukiwa mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye. Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana ajiandae.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kukushukuru kwanza wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii adhimu, hasa tunavyotazamia kupiga hatua kubwa ya maendeleo katika nchi yetu.

Lakini vilevile nitumie fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, Waziri Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa; pamoja na Naibu wake Deogratius Ndejembii kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya hususani nikiakisi hotuba nzuri ambayo imewasilishwa jana hapa Bungeni. Kimsingi mambo mengi ambayo nilitamani kuyazungumza Mheshimiwa Rais ameyatolea maelekezo jana na nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana japo bado hatujaingia katika mjadala wa kuijadili hiyo hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze mambo machache kwa ajili kuendelea kujenga na kuimarisha utumishi wa umma katika nchi yetu. Jambo la kwanza, tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi katika sekta zote. Nitakupa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto hatuna kabisa *Engineerwa Ujenzi*. Hakuna *Engineer* wa Ujenzi kabisa, lakini tunapeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, tunapeleka fedha nyingi kwa ajili ya vituo vya afya na zahanati. Sasa unaweza kufikiria ni namna

gani au ni miujiza gani inatumika kwenda kusimamia ujenzi wa fedha zote hizo za Serikali ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri zetu ikiwa hatuna wataalam kabisa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio huyo tu, Halmashauri hiyo hiyo haina Mwanasheria wa Halmashauri, haina mkusanyaji mapato kwa maana *DT*, hatuna *treasurer* kabisa kwenye Halmashauri ile. Sasa unaweza kudhani namna gani tuna upungufu mkubwa wa watumishi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka kwenye uhaba huo wa watumishi ambao kimsingi inabidi kutumia nguvu ya ziada kama Taifa, pamoja na vipaumbele ambavyo vimepangwa katika miaka hii mitano, lakini tuwe na namna nzuri kubwa ya kuweza kuongeza na kujaza nafasi hizo za watumishi ili kusudi nguvu kubwa ambayo inawekwa hasa ya uwekezaji wa miradi na fedha nydingi iweze kuwa na tija kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya watumishi bado ni changamoto, lakini nashukuru limeshatolewa maelekezo, lakini nisitisize tu kwamba hakuna wajibu bila haki kama ambavyo mama jana amesema. Ili tuweze kupata watumishi waweze kuwajibika vizuri ni vyema tukatoa haki kwa watumishi hawa, kwa maana ya malimbikizo ya madeni, wanadai fedha nydingi za likizo, wanadai fedha nydingi za *overtime*, wanadai fedha watumishi wa umma kwa miaka mingi, sasa pawe na kusudio maalum la kulipa haya madeni ili tuweze kwenda nao vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitamani kulizungumza ni ushiriki wa watumishi kwenye uchaguzi, kwa maana ya ushiriki kwenye siasa. Ndugu zangu mtakumbuka mwaka jana wakati tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu, ndipo ulipoanza kutumika rasmi Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2015. Waraka ambao ulitoa maelekezo ni namna gani mtumishi wa umma anakwenda kugombea nafasi za kisiasa hasa ya Ubunge na Udiwani. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; Watanzania wote wanahaki ya kuchagua na kuchaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, mtumishi wa umma anayo haki ya kuwa na chama cha siasa, lakini anayo haki ya kuchagua na kuchaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa umma kwa mujibu sheria hiyohiyo, wamewekewa utaratibu wa namna gani wanaweza kwenda kuchagua na namna gani wanakwenda kuchaguliwa. Namna nzuri ambayo imewekwa kwa mujibu wa sheria ni kwamba, mtumishi ataomba likizo bila malipo kwa miezi miwili na baada ya miezi miwili kwa maana ya ndani ya mchakato huo wa uchaguzi, kama atakuwa ameteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenda kugombea kwenye jimbo au nafasi ambayo anakwenda kugombea maana nafasi yake pale itakuwa imekoma ile nafasi ya utumishi. Lakini wapo watumishi wa umma ambao mpaka sasa huu ni mwezi wa kumi wapo likizo ambayo hawajaiomba tena likizo ambayo haina mshahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunatengeneza *threat*, tunatengeneza uoga kwa watumishi wa umma kwamba wasishiriki kwenye hizi nafasi za kisiasa. Mwisho wa siku, leo tunajisifu ndani ya Bunge letu Tukufu tuna watu wa mchanganyiko tofauti tofauti, tuna wataalam aina tofauti tofauti, hata Mheshimiwa Rais anavyoamua kufanya uteuzi hapati shida, watu wapo wenyewe taaluma tofauti tofauti. Lakini kama tunatengeneza huu uoga kwa watumishi wa umma kwenda kushiriki uchaguzi, maana yake ni kwamba miaka ijayo, tusishangae tukawa na hao darasa la saba walio wengi zaidi kwenye Bunge hili au kwa sababu ya kukosa ile motisha na namna ambavyo wanaweza wakalindwa wakiwa kwenye utumishi wa umma watakavyokuwa na nia ya kwenda kugombea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2015 mtumishi wa umma ikitokea hajachaguliwa kwa maana hajabahatika kupata

nafasi yake anapaswa kurejea kwa kuomba kurejeshwa kwenye nafasi yake kwa mujibu wa waraka huo. Lakini kama hajapata nafasi ya kurejeshwa, anapaswa kulipwa mafao yake. (*Makof*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Husna Sekiboko kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kumpa taarifa mchangiaji. Anachangia vizuri anasema kwamba na....

MBUNGE FULANI: *Declare interest.*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu spika, *na-declare interest* kuwa mimi ni darasa la saba. Anasema kwamba humu ndani kuna watu wenye taaluma tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafasi ya Ubunge ilitajwa kwamba mgombea Ubunge awe anajua kusoma na kuandika na sisi darasa la saba tunajua kusoma na kuandika, kwa hiyo asitutishe kwamba ikitokea tumekuwa yaani wataalam wamepungua wamebaki darasa la saba, hata sisi tunao uwezo wa kuiongoza Serikali. Nakushuruku sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, huo huwa ni mjadala mrefu, lakini kimsingi hili jumba hili ni la wa wawakilishi.

Kwa hiyo, wananchi yule wanayemleta ndio wanayeona ndio anaweza kuwakilisha hoja zao, yaani hoja ni uwakilishi, ndio maana Rais anakuwa na nafasi zake akiona humu kwenye uwakilishi hakutoshi analeta wa kwake anawapa hizo nafasi.

Kwa hiyo, kila kundi lina umuhimu wake humu ndani na wale wanao wachagua wanajua wanampeleka nani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sekiboko malizia mchango wako.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu zimepungua naomba unilinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie hii hoja kwa kuiomba Serikali sasa, Wakurugenzi hao ni watumishi wa umma na hata kabla ya kuteuliwa kuwa wakurugenzi walitokea kwenye Kanuni za Utumishi wa Umma, na namna ya wao kuingia na kutoka wanasimamiwa na Kanuni za Kudumu za Umma na *Standing Order*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Makatibu Tawala wa Wilaya ambao nao ni watumishi wa umma *perse*, kuna Katibu Tawala wa Mkoa na wa Wilaya, kwa maana ya Makatibu Tawala. Sasa hao wote ningeomba Serikali kutizama namna nzuri ya ku-*handle* hili suala lao. Ni kweli waliomba ruhusa wakaenda kugombea, lakini waraka umesema ni miezi miwili huu ni mwezi wa kumi. Ni vyema sasa Serikali itakoa hatma ya hawa watu kwasababu pamoja na kwamba baadhi yao wanatafsirika kama wateule wa Mheshimiwa Rais, lakini wanashughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, atafuatia na Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na kwa sababu ya muda naomba niende moja kwa moja na nina hoja moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Mapinduzi *traditionally* ni Chama cha Wakulima na Wafanyakazi, ndio *base* yetu; ndio *social base* ya chama hiki. Na Serikali ya

Chama cha Mapinduzi ni muhimu sana, sana, ikashughulika na wafanyakazi wa nchi hii kama mtaji muhimu wa Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kuzungumzia jambo ambalo limezungumzwa na Wabunge kwa sehemu; lakini mimi nimeona nililet kwenye Wizara ya Utumishi. Jambo la haki na stahiki za walimu wa Tanzania. Nimeona nizungumzie hawa kwa sababu kwanza, ni karibia asilimia 70 ya watumishi wa umma wa nchi hii ni walimu, lakini ndio watu ambaao tumewakabidhi watoto wetu na vijana wetu kwa kuwalea na kuwafundisha kulitengeneza Taifa letu tunakokwenda. Kwa hiyo, ni kundi muhimu kabisa muhimu sana, lakini bahati mbaya Wizara ya Utumishi na Hazina wamekuwa wakitoa nyaraka na taratibu ambazo kwa namna moja ama nyingine zimekuwa hazilitendei haki kundi hili kubwa katika watumishi wa umma wa nchi yetu. Nyaraka hizi na taratibu ambazo zimekuwa zikitumika kwa mfano kwa walimu zimezaa makundi yafuatayo:-

Moja, kuna kundi la walimu ambaao walipewa barua za kupandishwa madaraja lakini stahiki zao hazikubadilika mpaka wakastaafu. Kwa hiyo mafao yao ya mwisho yameathirika sana na kundi hili lipo mtaani, kubwa! Wamepewa barua, stahiki zao hazikubadilika na hivyo mafao yao yameathirika kwasababu stahiki zao hazikubadilika.

Kundi la pili, walimu waliopandishwa madaraja kwa barua, lakini hakukuwa na mabadiliko kwenye stahiki zao kwa muda mrefu mpaka wamekutwa na barua zingine za kupandishwa madaraja wakati zile za awali hazikufanyiwa kazi. Kundi hili nalo lipo kubwa katika kada hii ya walimu.

Kundi la tatu, walimu ambaao wamepandishwa madaraja au vyeo kwa makaratsi, lakini mpaka leo wamebaki na maandishi ya pesa kwenye makaratsi lakini stahiki zao hajijaguswa.

Kundi la nne na hapo nataka niguse mifano tu, walimu ambaao walipandishwa madaraja kwa barua na hii nadhani

ilikuwa mwaka 2013. Wakakaa nazo bila ya mabadiliko ya stahiki zao, baada ya muda ukaandikwa waraka ukafuta, kule kupandishwa kwao madaraja na bila sababu ya msingi na mimi nadhani ni baada ya kuona kuna mlimbikizo mkubwa Serikali ikataka kukwepa deni hili ikaandika waraka wa kufuta waraka wake ambao uliwapandisha hawa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya madaraja na stahiki zao sio hisani ni haki zao. Hivi inavyoendeshwa, inalifanya jambo hili ligeuke kuwa ni hisani kuwapandisha madaraja na kuwapa stahiki zao. Hili jambo si sawa, hatuwatendei haki walimu wa nchi hii. Ni matumaini yangu nimesikia Wizara wanasema kwamba wanapandisha madaraja watu ni karibu 900. Lakini kupandisha huku madaraja kusisahau hawa ambao tayari wameshaathirika kwa sababu ya mfumo mbovu ambao tumeutumia. Nyaraka tunazozilandika kutoka Utumishi, zisigeuke kichaka cha kupora haki za watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ndio itainua Taifa hili, hili kundi ni kubwa sana kulifumbia macho na kuja tu na hoja tu ya kupandisha madaraja peke yake hakutafidia haki ambazo zimepotea za haya makundi na haya ni machache inawezekana yapo mengi sana na jambo hili limezungumzwa hapa. Sasa mapendekezo yangu, naiomba Serikali ikiwezekana iunde Tume Maalum iende ikachunguze ili wale ambao tayari wamekwishaathiriwa na huu mfumo tuwarekebishie mambo yao hata kama tutawalipa taratibu lakini haki yao isipotee kila mmoja apate haki yake. (*Makofii*)

Mimi ni matumaini yangu wizara wamepewa vijana wadogo zangu; na nina hakika watafanyakazi vizuri, Mheshimiwa Mchengerwa na mwenzake nina aamini mtakwenda kutendea haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimemsikia Mheshimiwa Rais, akizungumza suala la haki, jambo hili ni haki ya wafanyakazi ukiacha maslahi yao ya kupandisha mishahara, lakini hata hiki ambacho ni haki yao, nataka kuiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi; chama cha wakulima na wafanyakazi, twendeni tukatende haki kwenye suala la

stahiki za hawa wafanyakazi ambao tumewaacha, wanunung'unika na misahau Waheshimiwa Wabunge ndio hawa pia wamesimamia chaguzi zetu. Wamefanya kazi nzuri, wanafanya kazi nzuri ya kuwalea watoto wetu, hebu tusiache haki zao zikapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo unaajiriwa, ukiajiriwa kwa teknolojia ya leo, likiingizwa jina lako kwenye kwenye mfumo kuna haja gani tena ya kuanza kuhangaika na taarifa kule chini! Tayari kishaingizwa kwenye mfumo tunajua baada ya muda fulani nitastaafu.

Leo kuna watu wanastaafu wanakaa kule mpaka wanakuwa wanywa gongo! Kwa nini? Kwa sababu hamuwapi haki zao za kuondokea kwenye vituo vyao vya kazi. Kila siku lete *document* hii, lete *document* hii, na nikushukuru, Mheshimiwa Naibu Spika asubuhi umellzungumza jambo hili, jambo hili lina umiza, tumeanza kutumia utaratibu wa kuhakiki, utaratibu wa kutaka nyaraka kama kichaka cha kupora haki za watu. Hizi haki zao zisimamiwe wazipate. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele imeshagongwa.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Mrisho Gambo.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuwapongeza sana Waziri, Naibu Waziri wa Wizara hii ya Utumishi, Iakini kwanza niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu shupavu, Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana ametufundisha hapa, ametuelekeza masuala ya nidhamu na uwajibikaji katika kazi. Kwa hiyo, mengi yamezungumzwa kuhusiana na upungufu wa watumishi katika Halmashauri, Wizara naongeza na katika Balozi zetu. Kwa kweli eneo hili tuangalie, wakati mwingine, wakati tuna-*solve* suala upungufu tuangalie pia namna ya kutumia wanao-*volunteer*. Zipo idara zinaruhusu *volunteers* ambazo haziratibu nyaraka ambazo ni *confidential*, kule wanakoruhusu tuanze hata kutumia *volunteers*. Kuna wakati wananchi wetu wanakwenda katika ofisi unakuta ni muda wa kazi wakati mwingine maafisa hawapo ofisini. Jukumu la utumishi wa umma ni kuhudumia wananchi. Wananchi wanafika katika ofisi zetu, unakuta watu hawapo na wakati mwingine mwananchi anaulizwa, una *appointment*? Sasa hii *appointment* niiombee wapi? Sijapewa *email*, sijapewa *form* ya kujaza *appointment*.

Tunaomba watumishi wa umma sekta zote na taasisi tunapoimarisha utumishi wa umma maana yake utawezesha hata uwekezaji. Anapokuja mwekezaji anahitaji ardhi, maji, masuala ya umeme, vibali mbalimbali, tunaposema tunakwenda kwenye uchumi wa kati basi kitu ambacho kinaimarisha ni pamoja na *public service*. Huduma hizi za Serikali tunaomba sana tubadilike, *change of attitude*, tunavyofika katika ofisi zetu wananchi wakija wale ndiyo mabosi wetu na sio sisi ambao tuko utumishi ndiyo mabosi. Tuwapokee wananchi vizuri. Ni mbaya sana mwananchi ana shida katika ofisi fulani anauliza, je, kuna mtu unamfahamu? Niepeleke ofisi fulani, *no!* wananchi wanapoenda katika ofisi za Serikali, wasikilizwe, waelekezwe na waoneshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lazima tubadilike unaenda kwenye ofisi unaambiwa mhusika huyo hayupo. Sasa lazima tujue kama mhusika umetoka kwa ruhusa umemuachia nani maana hizi ofisi tumetoa dhamana na tumeahidi wananchi tutawahudumia, leteni kero, msiwe na wasiwasi, sasa tunapokwenda katika hizi ofisi iwe ni halmashauri, iwe ni mikoa, iwe ni wizara, taasisi yaani hapa lazima tubadilike, tuwahudumie wananchi kiasi ambacho kinastahili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba pia nilizungumzie, nipongeze sana *PCCB*, *PCCB* ina-fall chini ya Wizara hii wamefanya kazi kubwa sana. Wameokoa mabilioni katika uchunguzi, takriban bilioni 96 katika mifumo wameokoa takriban bilioni 11. Bado *PCCB* tunaomba mtusaidie katika miundo. Ni namna gani miundo hii kwanza tunaweza tukaokoa hizi fedha, lakini pia miundo mingi *PCCB* washauri iwe *transparent*. Upande wa *TASAF*, *PCCB* wamefuatilia masuala ya kaya na kuhakikisha maeneo yote kwamba hakuna kaya hewa, maana ziko kaya zingine zinaingia katika mfumo wa *TASAF* yamkini ni hewa.

Kwa hiyo, *PCCB* wafuutilie, kuhakikisha kwamba fedha tunazopeleka *TASAF* zinafika kwa walengwa kwa wakati unaostahili. Kwa hiyo, napongeza sana kazi nzuri, lakini bado kibarua cha kuboresha ili maendeleo yaweeze kufika kwa wananchi yafanyike kwa ufasha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Serikali Mtandao. Serikali Mtandao ni eneo muhimu sana, niombe Serikali Mtandao tuweke taarifa muhimu. Sasa hivi watu wengi kutokana na hii changamoto ya *Covid-19* mara nyingi sana wanatafuta taarifa katika mtandao. Kuna taarifa mbalimbali za Wizara mbalimbali; taarifa za masoko, bidhaa ambazo Tanzania tunauza katika Wizara zetu, kwa hiyo, wanapoingia wawekezaji na sisi wenyewe kupata taarifa fulani katika Wizara fulani tunaomba taarifa hizi ziwepo maana ni ngumu sana mwananchi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda Makao Makuu ya Wizara wakati taarifa zingine unaweza ukapata katika mitando.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa kupitia *e-government* tuzidi kuweka ushirikiano na mahusiano ya Wizara mbalimbali na balozi zetu. Wakati mwingine kunakuwa kuna maswali mbalimbali katika Balozi zetu wanahitaji taarifa. Kwa hiyo, *e-government* tuone ni namna gani tutaweza kujitahidi kuweka taarifa stahiki zinazopaswa katika mtandao. Iyiwe kwamba ah *website* haijawa *updated* tangu kipindi fulani. Katika eneo hili tuzidi sana kuboresha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kama tulivoambiwa nidhamu na uwajibikaji katika kazi ni suala zima la kupata mafunzo. Wakati umefika sasa watu wanaaojiriwa katika nafasi mbalimbali wapate mafunzo, *the do's and the don'ts*, maana sasa hivi wakati mwingine katika ajira zetu unakuta bado taratibu zingine za kuhudumia wananchi watu hawajapata kuzielewa ipasavyo.

Kwa hiyo, Chuo cha Utumishi wa Umma nakipongeza sana na Kamati tulifanya ziara pale ya masuala ya Serikali za Mitaa, imefanya kazi kubwa, nzuri lakini tuendelee kuomba watoe mafunzo kwa taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nalo ningependa kulizungumzia ni kuendelea kupoingeza ujenzi wa Ikulu ya Dodoma. Ujenzi huu wa Ikulu ya Dodoma ni muhimu sana. Kwa hiyo, ujenzi huu utakapokamiliika tuombe sana ujenzi wa Ikulu ya Dodoma uende sambamba na huduma. Maana tunaweza tukajenga vizuri sana, lakini ziwe ni zile huduma zinazopaswa kuwemo mle. Tunaita huduma za *first class*, hata Mheshimiwa wetu anavyofanya kazi Ikulu afanye kazi akipatiwa huduma za kutosha, stahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri, hili la watumishi kuwasikiliza wananchi ni la muhimu sana. Tunalamika hapa barabara ni mbaya, mtu ametoka atokako kasafiri siku nzima, afike mahali hana pa kulala anaambiwa huwezi kumuona. Ni muhimu watu tuwe na ule ubinadamu kwa sababu huyu anayesafiri angeweza kuwa ndugu yako, mzazi wako ni vile tu wewe una nafasi fulani. Kwa hiyo, msikilize. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jesca Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajandae.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi ninakwenda kujikita kwenye eneo moja tu, eneo la utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu na tunatambua kwamba utawala bora ndiyo nguzo muhimu sana kwenye mipango yoyote. Ukiangalia kwenye *sustainable development goals*, utawala bora ni nguzo muhimu. Ukiangalia kwenye Dira ya Taifa, utawala bora ni nguzo muhimu lakini hata ukiangalia kwenye mipango ambayo tunakuwa tunajadiliana humu ndani, haiwezi kutekelezeka kama eneo la utawala bora haliwezi kuwekewa nguvu inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni lazima ili kuweza kuboresha eneo la utawala bora tutafute vichocheo vikubwa ambavyo vinachochea na kuhamasisha utawala bora katika Taifa letu. Katika tafiti zangu ambazo nimekuwa nikizifanya na tafiti mbalimbali ambazo nimekuwa nikisisoma nimegundua kitu ambacho ni *very interesting*. Nimekuja kuona suala la utawala bora, tafiti nyangi zinaonesha wanawake wana mchango mkubwa sana kwenye *good governance* na sehemu hii napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Rais mwanamke wa kwanza katika Taifa letu, lakini kwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke *East Africa. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rekodi tulioiweka kama Taifa, tumeithibitishia dunia ya kwamba Taifa letu hatuna *doubt* wala *dispute* ya uwezo na umahiri wa mwanamke katika masuala ya uongozi. Ni ukweli usiopingika kwamba mama ameanza vizuri. Nampongeza na namuunga mkono kwenye jambo ambalo amelizungumzia jana la kuunga jitihada zake za nguvu kabisa kuwapa vipaumbele wanawake. *(Makof)*

Mimi nina ombi moja kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais, ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ambayo ilitumika kwenye kampeni 2020, ukiangalia ukurasa wa 281

Ibara ya 231(j) inasema hivi; Serikali ya CCM itabaini na kutekeleza mikakati ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika maamuzi na uongozi kwenye nyanja za kisasa na kiuchumi hadi kufikia 50 kwa 50. Na ***bold* hadi kufikia 50 kwa 50.**

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna wakati mwiningine sahihi ambao kama wanawake wa Taifa hili tunautegemea kama kipindi ambacho mama Samia Suluhu Hassan atakuwa madarakani kwa ajili ya kutekeleza jambo hili. Suala hili tusilitazame katika sura ya kisasa, suala hili tulitazame katika sura ya usimamizi wa masuala ya kiuchumi na masuala ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wamepimwa na wamethibitika kuonekana kuwa ni waadilifu na wana uwezo mkubwa sana kusimamia masuala mbalimbali katika Taifa letu. Lakini pia sisi hatutakuwa wa kwanza kufanya hivyo, nimesoma miaka mitano iliyopita Germany, nimeangalia sheria yao na ninayo hapa, Germany wametunga sheria, yaani kwa upande wao hilo suala halina mjadala. Uwakilishi wa wanawake *not less than 30 percent* kwenye mashirika yote ya umma, pamoja na *private sector*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hapa kwetu Tanzania wanawake wameonesha jithada kubwa sana katika kufanya shughuli zao. Nimesoma taarifa ya utafiti uliofanywa na *Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA)*; wanasema hivi, wanawake wa Tanzania ndiyo *lion share*, *I mean* ndiyo *majority share*, *I mean* ndio wamiliki wakuu wa biashara ndogo ndogo na biashara za kat. Wanawake hawa wanasimamia zaidi ya asilimia 95 ya idadi ya biashara zote Tanzania. Wanachangia zaidi ya asilimia 35 ya uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Naomba nitumie jukwa hili la Bunge lako Tukufu kumuomba Mheshimiwa Rais apambane huko aliko na sisi kama Wabunge kwa nafasi yetu tutamsaidia. Ninaomba kutoa taarifa, ninakusudia kuleta Muswada Binafsi Bungeni wa kutaka *not less than 30 percent* ya viongozi wa mashirika ya umma wawe wanawake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba taasisi zote zinazo-*deal*/na masuala haya waweze kunisaidia kwa ajili ya kupata *information* za kuweza ku-*package* hoja yangu ambayo nitakuja kuleta Muswada Binafsi. Lakini pia niwaombe na Waheshimiwa Wabunge wanaume watuunge mkono sana katika hili. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer Manyanya*.

TAARIFA

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, napenda kumpa taarifa ndogo tu Mheshimiwa Jesca kwamba kwa jinsi ambavyo ameweza kuinukuu llani ya Chama Cha Mapinduzi, kwa jinsi ambavyo ameweza kusikiliza vizuri hotuba ya Mheshimiwa Rais ya jana na kwa jinsi ambavyo anaendelea na mchango wake, kwa kweli naamini kama Kambi ya Upinzani itakuwa inaendelea kutoa michango *positive* na kuwa pamoja katika timu moja katika Bunge, mambo mengi ambayo tulikuwa tunayapanga yataendelea vizuri. (*Makofi*)

Kwa hiyo mimi nampongeza kwa *positivity*, uchanya wake katika mchango huu. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa, hiyo sio taarifa. Malizia mchango wako. (*Kicheko*)

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niendelee kwenye eneo lingine dogo la *transparency*. Unapozungumzia utawala bora suala la *transparency* haliepukiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* anisaidie. Sitaki sana kujua sababu gani iliwfanya mkajiondoa kwenye *OGP* (*Open Government*

Partnership). Wote tunajua hii *Open Government Partnership* wakati mmejiunga mwaka 2011 na bahati mbaya au nzuri sijajua ni kwa kusudi gani mkaja mkajitoa, mmepeleka barua yenu kule kwenye *committee* tarehe 29 Juni, 2017. Mmetaka kujiondoa na mmejiondoa kwenye umoja huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sisi kijiunga kwenye *Open Government Partnership* lilikuwa linawasaidia sana watafiti wa Taifa hili, lilikuwa linawasaidia sana *NGO's*, wasomi wa Taifa hili. Walikuwa wana uwezo wa kupata taarifa mbalimbali ambazo wanazihitaji kwa ajili ya kusaidia hata katika masuala haya ya kujadili bajeti, tulikuwa tuna uwezo wa kupata *references* ambazo zimefanywa na *researchers*, lakini pia hata wanafunzi wetu ambao wako shulen *OGP* imekuwa ikiwasaidia sana wao kupata taarifa na kuwasaidia katika masuala yao mbalimbali ya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais hebu turudi kwenye *OGP*, kuna tetesi ambazo nimezisikia kwamba mmejiondoa kwenye *Open Governance Partnership* kwa sababu kuna namna nyingine mmetafuta ya kutaka kutoa *information* zenu kuitia umoja fulani ambao uko Afrika, lakini *it's kind of* kutaka kufunika funika vitu hivi. Mimi ninaomba sana Serikali, turudi kwenye *OGP*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la uhuru wa vyama vyaya siasa. Katika Taifa letu mara nyingi sana tumekuwa tukishuhudia vyama vyaya siasa hususan vyama vyaya upinzani vimekuwa vikikosa fursa ya kufanya mikusanyiko ambayo kikatiba ipo kihalali kabisa.

Ninataka nimuombe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais katika suala hili hebu rekebishi hapa. Hivi vyama vina haki kabisa ya kikatiba ya kufanya mikutano ya hadhara. Vina haki ya kikatiba ya kukutana na wananchi na kueleza sera zao. (*Makof*)

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

TAARIFA

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu muongeaji asipotoshe, Mheshimiwa Rais jana amezungumza, anataka kukutana na vyama vyote vyaya siasa, wazungumze waone nini sasa wanaweza wakaendesha nchi yao pamoja. Haya masuala ya kwamba sijui vyama vimezuiwa kupiga nini, sijui kufanya mikutano, yanatokea wapi? Naomba nitoe Taarifa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasikitika sana kusema kwamba sijajua kama Mheshimiwa Mbunge ni kweli hafahamu au laa! Suala la kufanya mikutano ya siasa sio suala la Mheshimiwa Rais kutuambia, ni suala la Kikatiba ambalo linatakiwa lifanyike katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii tukianza kuiendesha kwa matamko na sio kwa kufuata misingi ya Kikatiba tutapotea. Ni muhimu sana ili Serikali iweze kuwa ni Serikali ambayo inazingatia utawala bora basi itoe fursa kwa vyama vyaya kisiasa kufanya mikutano yao.

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tulionao hiyo itakuwa Taarifa ya mwisho.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, taarifa inatokea upande ule. Mheshimiwa jitambulisse.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Francis Isack Mttinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji kwamba nchi yetu haijawahi kuzuia mikutano ya vyama, kilichokwuwa kinatakiwa ni kwamba kila mtu kwenye Jimbo lake akafanye mkutano. Kwa hiyo, anaposema kwamba tumewahi kuzuia mikutano, anapotosha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Kishoa, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei lakini niseme tu kwamba mimi nazungumzia vyama vyaa siasa sio mkutano wa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijajua kwa upande wenu hili ninyi mnalifanyaje, lakini sisi wa vyama vyaa upinzani tunakuwa tuna mikutano ya hadhara ambayo ni kama chama ambacho kinajumuisha viongozi wa chama wanakwenda kutangaza sera ya chama chao na wananchi wanapata elimu ili kuweza kupima chama gani ambacho kinafaa kushika madaraka.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bil akufuata utaratibu)

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa. Asipotoshe, aseme ukweli.

NAIBU SPIKA: Subiri, subiri.

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, mikutano ya vyama vyaa siasa huwa ni mikutano ambayo iko kwenye katiba zao. (*Makofi*)

Hiyo mikutano hufanyika kwa vipindi fulani na hiyo mikutano hata Chama cha Mapinduzi huwa ile mikutano sio ya hadhara. Kwa mfano tarehe 30 Aprili, 2021 Chama cha Mapinduzi kimetangaza kitakuwa na Mkutano Mkuu, Mkutano Mkuu unaenda kufanyika pale *JK Convention Centre*. Ule niyo utawenza kuita ni Mkutano wa CCM, lakini ameenda Rais mahali unasema huo ni Mkutano wa CCM, ule sio mkutano wa CCM, ni mkutano wa Rais. Mkutano wa Chama cha Mapinduzi ni kama huo tunaoenda kesho kutwa. Sasa ukisema mikutano ya vyama vya siasa imekatazwa, kuna chama kiliitisha mkutano halafu ukakatazwa?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Ngoja, tuelewane vizuri. Hata Katiba tuwe tunaisoma vizuri, leo naongea nikwiwa nimekataa. Hata Katiba tuisome vizuri. Katiba ikishaweka zile haki kule, imeweka na mipaka yake na usisome kifungu kimoja ukata kukisimamia hicho ukasahau kingine. Katiba yetu inazungumza haki nydingi sana. Ile haki ya kwako wewe haitakiwi kuzidi pua yako ili usiisumbue haki ya mtu mwingine.

Kwa hiyo lazima utaratibu ufuatwe na ndiyo maana Bunge letu hutunga sheria ili kuvikazia vile vifungu vya Katiba. Kwa hiyo, ukizungumza tu hivi jumla mtu anawaza kuna katazo labda liko mahali, hapana, tuelezane vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Jesca Kishoa malizia mchango wako.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki sana kubishana na Kiti chako, lakini niseme tu mimi ni mionganoni mwa wahanga wakubwa sana kwenye suala hili la mikutano ya hadhara.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hoja yangu.

NAIBU SPIKA: Haya, malizia sekunde 30. Naambiwa hapa muda wako umekwisha.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kusisitiza vyama vyaa siasa tunahitaji kupata uhuru wa kikatiba wa kufanya mikutano ya hadhara. Ni kwa muda mrefu sana na mimi nimekuwa ni muhanga katika eneo ambalo nilikuwa nikiwakilisha kama Mbunge wa Mkoa wa Singida kuanzia *term* ya Bunge lililopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikizuiliwa kufanya mikutano yangu ya hadhara na wananchi kwa sababu ambazo hazieleweki. Kuna wakati mwingine wamekuwa wakitoa sababu za kusema kwamba hali ya...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ahsante sana. Muda wako umekwisha.

Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile ajiandae.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kwenda kwenye hoja zangu moja kwa moja nakumbuka siku moja hapa Mheshimiwa Spika aliongea kauli ambayo ilinigusa sana, kuna jambo lilitokea Wabunge tukapiga makofi, akasema wakati mwingine Wabunge tunapiga makofi hata hatujui tunapiga makofi kwa jambo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo jambo linanikumbusha wakati wa kampeni nilivyokuwa Arusha Mjini, nilikwenda kufanya ziara kwenye viwanda viwili, Kiwanda cha A to Z na Kiwanda cha *Sunflag*. Wafanyakazi wale waliniuliza maswali ambayo kila siku nayakumbuka; kwanza walitaka niwahakikishie kwamba nitakapokwenda Bungeni sitakuwa Mbunge wa makofi na ndio hata kwa mambo ambayo

yanaumiza wananchi, la pili wakaniambia je, naweza kutoa hoja zenyé maslahi ya wananchi au nitakwenda kuunga kila kitu mkono hata kama kinaumiza wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakanikumbusha kwamba wanasema wana hasira sana na hoja ya kikokotoo. Kwa hiyo, na yenyewe pia walisema niweke kwenye maanani, lakini pia wakataka niweke kichwani kwangu changamoto iliyopo ya kima cha chini cha mshahara kati ya wafanyakazi wa sekta binafsi na wafanyakazi wa sekta ya umma ambapo wafanyakazi wa sekta binafsi wanaohusika na mambo ya kilimo na nguo kwenye viwanda, kima cha chini ni 100,000/= lakini wa Serikali ni 300,000/=. Kwa hiyo, hayo mambo ambayo nimesema leo niwakumbushe kwamba na mimi nayakumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwenye mambo mawili; jambo la kwanza nakumbuka Serikali yetu ya Awamu ya Tano ilifanya zoezi moja muhimu sana na zoezi nyeti sana, zoezi la kuhakiki vyeti vya watumishi wetu. Lilikuwa ni zoezi la lazima, lilikuwa ni zoezi ambalo linatusaidia kufanya usafi kwenye sekta nzima ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninakumbuka tarehe 7 Machi, 2018 ilitoka Taarifa ya mwisho ya Serikali ambayo ilituambia wafanyakazi 511,789 ambao ni sawasawa na asilimia 96.71 walikuwa ni wafanyakazi waliohakikiwa, lakini wafanyakazi 14,409 ambao ni sawasawa na asilimia 2.82 walikuwa ni wafanyakazi ambao walibainika wana vyeti *fake* na wafanyakazi 1,907 walikuwa ni wafanyakazi ambao walikuwa bado hawajapeleka uthibitisho wa vyeti vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ambayo nataka nijjenge hapa, pamoja na kuunga mkono zoezi la Serikali la kuwatambua watumishi wenye vyeti *fake* na kuchukua hatua stahiki, lakini lazima tukumbuke hawa watumishi walifanya kazi ya kuitumikia nchi hii. Hata masuala ambayo tunajivunia leo wao pia ni sehemu ya kazi ambayo tumeifanya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kujenga hoja kupitia Wizara yetu hii ya Utumishi ni vizuri sasa wafanyakazi hawa tukaangalia

utaratibu wa kuwapatia haki zao kwa sababu, wakati wanafanya kazi waliweza kukatwa fedha ambazo zikaenda NSSF, leo zile fedha zimekwenda kule zinamnufaisha nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wafanyakazi hawa wengine walipitisha muda wa kisheria, miaka 15, miaka 20 na kuendelea, walistahili pia kulipwa kiinua mgongo. Kwa hiyo, pamoja na Serikali kuwaondoa kazini nilikuwa naomba Serikali hii ya Awamu ya Sita ikaangalie jambo hili kwa jicho la huruma, ikawaangalie wananchi hawa wananchi 14,409 ambaao wana familia zinawategemea wakaweze kupata kiinua mgongo chao wakapate na mafao yao na baada ya hapo tuendelee sasa kuchukua watumishi wenye sifa. Maana sisi kama Serikali pia tulichangia kuingiza watumishi hawa kwa sababu waliingia kwa utaratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili niende kwenye mchakato mzima wa kuwapandisha vyeo watumishi na madaraja na mimi nakiri hotuba ya jana ya Mheshimiwa Rais imetupunguzia maneno kwa sababu watumishi wa umma walikuwa na kilio kikubwa sana. Watumishi wa umma toka mwaka 2015 walikuwa hawajapandishwa mishahara. Watumishi wa umma wamekuwa na matatizo mengi sana kwenye madaraja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la madaraja sio suala jepesi kama tunavyoliona. Mimi nakumbuka mwaka 2012/2013 wakati nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe kweye bajeti ya mwaka 2012/2013 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Korogwe Mji alisahau kuwaingiza watumishi kwenye mchakato wa kupanda vyeo, watumishi ambaao walijiriwa mwaka 2009. Matokeo yake ni kwamba wale TSC au kwa maana ya TSD huko zamani ambaao lazima kikao chao kikae kiweze kuwapitisha hakikuweza kukaa eti kwa sababu hakuna posho, watumishi wakakosa haki yao ya msingi ya kupanda madaraja na baadaye wakatakiwa waandike barua ya kuomba kupata daraja la mserereko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja yangu ni nini; lazima tuangalie vizuri mfumo wetu wa kuwapandisha

madaraja watumishi. Kwa sababu nimeambiwa taratibu ambazo zinafuatwa, taratibu ya kwanza tunaangalia bajeti. Mfano mwaka huu tumeajiri watu 800, uwezo wetu wa bajeti wa kupandisha ni watu 300, tunabakisha watu 500 ambao wao watakuja kupanda mwaka mwingine wa fedha. Kumbuka hawa wameanza kazi pamoja, huyu ana *TGS D* atatoka D atakwenda E, ambaye ameanza naye kazi pamoja atabaki kwenye *TDGS D* ile ile ambayo italeta manung'uniko na malalamiko makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeambiwa pia wanaangalia *tange* kwa maana ya *seniority list*, lakini pia wanaangalia na *OPRAS*. *OPRAS* ambayo ina changamoto nyingi inatakiwa kuwe na malengo, lakini pale kuwe na *resources*. Unakuta malengo yanakuwepo, lakini *resources* zinakuwa hazipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka niseme kwamba, changamoto ya madaraja ya watumishi ni kubwa tofauti na ambavyo tunaiona. Nilikuwa nataka niishauri Serikali ni vizuri sasa, kwa mapendekezo yangu, tukaunda tume au tukaunda timu maalum ambayo itafanya kazi ya kupitia changamoto za madaraja ya watumishi kwa miaka yote iliyokuwepo. Vinginevyo wale ambao wanaweza wakalalamika watapata *solution*, wale ambao hawawezi kuwafikia Serikali watabaki wanانung'unika na mwisho wa siku tunaanza kuwatupia mzigo Maafisa Utumishi wakati tunafahamu kwamba Afisa Utumishi hawezikupandisha nje ya bajeti na hawezikupandisha nje ya utaratibu wa Serikali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zimeisha?

NAIBU SPIKA: Ee, kengele ni moja kwa CCM mnachangia dakika saba.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, basi kwa sababu muda umeisha nilikuwa naomba pia, Serikali...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ajiandae.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kujikita kwa kuanzia kwenye maeneo mawili; eneo la upungufu wa watumishi pamoja na eneo la madeni, lakini kama muda utaniruhusu nitaongeza mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya upungufu wa watumishi imekuwa ni changamoto kubwa na ambayo imekuwepo Serikalini kwa muda mrefu sana. Mimi nimefanya kazi kama mtumishi wa umma kwa zaidi ya miaka 20 kabla sijawa Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini. Miaka yote ambayo nimehudumu kama Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri, kama Mhasibu *TANROADS*, kama Mkurugenzi katika Halmashauri, changamoto ya upungufu wa watumishi na madeni kwa watumishi imekuwa ni changamoto kubwa ambayo imesababisha kuwepo kwa hoja za *CAG* ambazo zimeshindikana kufungwa kwa sababu changamoto zimekuwa zikiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Halmashauri katika nchi yetu na idara mbalimbali za Serikali zimekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi kiasi kwamba baadhi ya majukumu yamekuwa yakishindwa kufanyika. Na niseme tu kwamba unapokuwa na upungufu mkubwa wa watumishi ni sawasawa na timu ya mpira ambayo inatakiwa kucheza wachezaji kumi na moja halafu unakuwa na wachezaji pungufu, hatutarajii timu ya namna hiyo iweze kushinda, ili timu iweze kushinda inatakiwa iwe na wachezaji kumi na moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba kumekuwa na hii changamoto hata katika Wilaya yangu ya Kilwa kumekuwa na changamoto hii kubwa, kuna baadhi ya zahanati zina watumishi mmoja-mmoja. Unaweza ukaona wale watumishi mmoja-mmoja wanaofanya kazi katika zahanati wanawezaje kufanya kazi wakati wanahitaji kuwa likizo, wakati fulani wanaumwa na kadhalika, lakini kuna zahanati moja kule katika Kata ya Kinjumbi, Kijiji cha Miyumbu ilikaa miaka tisa ikiwa inasubiri watumishi kwa sababu watumishi wachache. Mwaka jana ndio angalau tulipata mtumishi mmoja, lakini kuna zahanati katika Kijiji cha Bugo, Kata ya Chumo ina miaka zaidi ya mitano sasa hivi hajifunguliwa kwa sababu watumishi ni wachache, lakini leo tunacho Kituo cha Afya tunatarajia kukifungua hivi karibuni pale Somanga, tunafikiria, tunaumiza vichwa kwamba hali itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Serikali katika hili jambo, Wizara yetu ya Utumishi ililie maanani sambamba na suala la madeni ambalo nalo limekuwa ni shida. Madeni yamekuwa yakihakikiwa; katika utumishi wangu wa umma wa zaidi ya miaka 20 kila mwaka tumekuwa tukihakiki madeni; tunahakiki, tunahakiki, taarifa zinakuja watumishi kutoka Wizarani, Wizara za Kisekta zimekuwa zikija kuhakiki madeni, lakini mwisho wa siku madeni yanakuwa hayalipwi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna utitiri mkubwa, kuna kiasi kikubwa cha madeni kwa watumishi wetu kiasi kwamba inapunguza morali ya kufanya kazi kwa watumishi wetu, kwa hiyo, ningeomba hilo nalo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nikirudi kwenye suala la watumishi katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini kuna shule shikizi saba. Katika zile shule shikizi zote zinahudumiwa na walimu wa kujitolea ambaao wanalipwa viposho vidogo sana na wananchi baada ya kuwa wanachangia. Kwa hiyo, niseme kwamba, kwa kweli haya matatizo mawili ni matatizo makubwa hili la upungufu wa watumishi na madeni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora, niombe iandae mpango kazi maalum ili ndani ya miaka minne ijayo wakati tunakwenda kwenye uchaguzi wa mwaka 2025 basi tuhakikishe hii changamoto imekwisha ili tuzipunguzie Halmashauri zetu na idara zetu hii hoja ambayo inaweza ikafungwa, lakini vilevile tuweze kuwasaidia wananchi wetu wapate huduma inayotakiwa katika maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la michezo ya watumishi. Miaka mitano iliyopita kulikuwa na Sera ya Michezo, kulikuwa na Mashindano ya SHIMIWI kwa watumishi wa sekta ya umma, lakini kule kwenye Serikali za Mitaa pia kulikuwa na michezo inafanyika kwa watumishi ili kujenga afya bora, lakini vilevile kupambana na maradhi kama ya UKIMWI na changamoto nyingine za kiafya, lakini hata kwenye mashirika ya umma pia walikuwa na michezo yao wanafanya, lakini ndani ya miaka mitano iliyopita michezo hiyo tumekuwa hatuioni na niseme tu kwamba, nafahamu Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, ni mwanamichezo nimuombe kwa *interest* aliyonayo kwenye michezo, lakini vilevile katika kuboresha afya za watumishi wetu basi tuweze kurejesha ile michezo katika taasisi za umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kuna Mbunge mwenzangu amezungumza muda mfupi uliopita, kulikuwa na Wakurugenzi saba, *RAS* mmoja, pamoja na ma-*DAS* watatu walishiriki kwenye uchaguzi wa kura ya maoni mwaka 2010, lakini kwa masikitiko makubwa wale Wakurugenzi waliondolewa kwenye *payroll* ya Serikali na hatimaye mpaka leo hii hawajarudishwa, lakini nafahamu kwamba, wapo watumishi wengine wengi maelfu kwa maelfu walishiriki kwenye ule uchaguzi wa kura za maoni, walipotoka kwenye ule uchaguzi baada ya kuwa hawakupata nafasi ya kuendelea na uchaguzi uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 walirudishwa kazini baada ya kutoa taarifa kwamba, wametoka na hawakuvuka kwenye kura za maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara iwasaidie wale watumishi kumi na moja, *RAS* mmoja, ma-*DED* saba, pamoa na ma-*DAS* watatu ili waweze kuridishwa kazini na wapate haki zao za msingi. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Ndulane na Mheshimiwa Sekiboko, nafikiri ingeirahisishia Serikali kujua kama hawa walitokea kwenye utumishi. Mtakumbuka kuna teuzi zilifanywa ambazo ma-*DAS*na hao ma-*DED* mnasema sijuina ma-*RAS* walikuwa wanatoka huko watokako, sio watumishi wa umma. Sasa kama walichukuliwa nje ya utumishi wa umma, amepewa uteuzi, unataka sasa hapohapon kwa kuwa aliteuliwa basi apewe na ajira, arudi wapi sasa kama alikuwa ameteuliwa kutoka sehemu ambayo ye ye hakuwa mtumishi wa umma?

Nadhani lazima tuweze kutofautisha uliosema wamerejeshwa kazini; wewe mwenyewe umesema walikuwa watumishi wa umma, kwa hiyo, wamerudi kwenye nafasi zao. Sasa huyu Mkurugenzi kaenda, ilibidi ile nafasi ikae wazi imsubiri? Tuisaidie na sisi Serikali tunapotoa huu ushauri, hao waliteuliwa wakiwa wametoka wapi? Alikuwa Afisa Tarafa? Alikuwa Katibu sijui wa kitu gani? Lazima hayo yote yakae vizuri.

Kwa hiyo hata ninyi mnapoishauri Serikali ipelekeeni taarifa mahususi. Ukitaja tu hizi namba hata mimi mwenyewe hapa mbele ambaye ndio nasimamia kikao sielewi hao unaowaongelea walikuwa watumishi wakateuliwa kuwa Mkurugenzi, halafu ile nafasi yake ilibidi arudi sasa kwenda kwenye nafasi ipi sasa kama aliteuliwa kutoka sehemu nyine?

Kwa hiyo, nadhani tuisaidie Serikali tuipelekee hizo taarifa ili iwe rahisi kwao kufanya kazi hii michango yetu.

Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri sana ambayo kimsingi jana iliwasilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa sana ya baadhi ya hoja ambazo nilitaka kuzzungumza nadhani zimekuwa *coverd*, kwa hiyo ninawashukuru sana. Lakini ninaomba nzungumzie maeneo machache, la kwanza jana hapa amezungumza Waziri wetu wa TAMISEMI na ameonesha jinsi ambavyo atakwenda kuweka msukumo mkubwa kwenye watumishi waliopo kwenye kada ya TAMISEMI. Lakini nilitaka niongezee na nisisitize eneo moja, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri kwenda kutazama vyema mazingira ya ufanyaji kazi ya watumishi ambapo wapo kimsingi kwenye Utumishi na TAMISEMI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuititia ule Waraka wa Elimu Bure sote tulishuhudia jinsi ambavyo tultioa posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule pamoja na Waratibu wa Elimu Kata, lakini sasa hoja yangu ni nini, niwaomba mkatazame vizuri sana kuhusu watendaji wa kata kwenye nchi hii. Watendaji wa Kata, Maafisa Tarafa hata kwenye vijiji wao ndio viongozi kwenye maeneo yao, Watendaji wa Kata ndio Wakurugenzi kwenye maeneo yao, tumefanya kazi nzuri ya kuwawekea mazingira mazuri ya kazi wenzetu wa elimu na tunao mpango Maafisa wengine wa Ugani lakini bosi ambaye ni Mtendaji wa Kata ana hali gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ye ye ndiye anayesimamia madarasa, ye ye ndiye anayepeleka taarifa za Kata kwa Mkurugenzi ye ye ndiye anayekwenda kusimamia usafi huko, kimsingi hawa ndio wanaofanya kazi kubwa zaidi ya kumwakilisha Mkurugenzi kwenye maeneo yao. (*Makofi*)

Kwa hiyo hilo ningeomba pia liende sambamba na upande wa Maafisa Tarafa, kada hii huko nyuma kama alivyozungumza mchangiaji mmoja juzi ni kada ambayo kimsingi mionganoni mwao ndio tunateua Ma-DAS, tumeteua ma-*DED* na Ma-DC, lakini changamoto kubwa ipo kuanzia kwenye usafiri ofisi mpaka *incentive* zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Maafisa Tarafa walikuwa wanapata mishahara ya kiuongozi, baadaye ikaondolewa, ninaishauri sana ikiwezekana tutazame *package* maalum, maana hawa ndio wawakilishi wa Mkuu wa Wilaya kwenye maeneo yao. Vivyo hivyo kwa ma-DAS katika ofisi zao, utakuta *DAS* ni kiongozi mkubwa baada ya DC akitoka *DAS* wanasesma anakuja *DED*, lakini kwa mujibu wa *package* yake unaambiwa anastahili kupewa gari aina *saloon*, ni vyema tukahuisha mambo kama haya yaendane sambamba na wakati uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yapo mambo madogo ninayotaka kuyazungumzia, moja; kuna kitu kinaitwa kupanda cheo kwa mserereko, huko nyuma ilikuwepo, hii ni changamoto kubwa watumishi wetu wanayo sasa hivi. Utakuwa mtumishi alikuwa na haki ya kupanda cheo mwaka 2012 hakupanda, alikuwa na haki ya kupanda cheo mwaka 2016 hakupanda, pengine mwaka 2019 hakupanda, sasa anatakiwa apande cheo leo. Na pengine kutokupanda kwake cheo kipindi cha nyuma si makosa yake ni makosa ya mwajiri wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna m-punish yule mtumishi tumeweka mfumo mzuri kwamba kimsingi yule Afisa Utumishi au mwajiri ambaye hakufanya vile atachukuliwa hatua; je, stahiki ya mtu huyu, kwa hiyo niwaomba wenzetu wa Wizara sasa, wakalitazame jambo hili ni watumishi wangapi walistahili kupanda cheo lini kwa haki na kisha waweze kupatiwa stahiki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni *recategorization* hii ni kubadilishwa kada hapa kuna changamoto na kilio kikubwa sana kwa watumishi wetu,

utakuta mtumishi amesoma, ni mwalimu *diploma* akaanza kupanda cheo labda *TGSC* akapanda D akapanda hadi E baadaye amefika mshahara wa shilingi 1,200,000; sasa ameenda kusoma *degree* nyingine ya Utawala au yoyote ile, wakati wa kumbadilisha cheo kutoka kwenye yale aliyoysomea mambo ya ualimu kwenda huku kwenye utawala ambapo kimsingi mwajiri ameridhia kuna nafasi tunaanza kumpeleka akaanze kupata mshahara kwenye Utawala pale inapoanzia *entry point* yaani kwa mfano kama *HR* anatakiwa kuanza kulipwa labda *HR II* shilingi 700,000 huyu mtumishi alifika *level* ya ualimu ya kulipwa shilingi 1,200,000 anarudishwa kwenye *HR II*, ushauri wangu ni nini, tunaweza either *ku-maintain* ile *personal salary* au tukai-*quit* mshahara wa kule anapotoka *vis-a-vis* huko anakokwenda ili tuisiwavunje moyo hawa watumishi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nililokuwa nataka kulizungumzia pia kwa kidogo ni *issue* ya madai mbalimbali, kwa mfano nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aende akatazame madai ya wakufunzi wa Vyuo na Udhhibit Ubora, yako malalamiko ya watu ambao hawakupewa stahiki zao kwa zaidi ya pengine kuanzia mwaka 2018 kurudi nyuma, changamoto ni nini, wanastahili kitu gani? Kama wanastahili wapewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kuzungumzia kidogo kuhusiana na makundi maalum kwenye utumishi ambao kimsingi Wizara naomba ikasaidie kusimamia, hapa nazungumzia walimu, hapa nazungumzia *ma-nurse*, hapa nazungumzia madereva, yaani zile kada madereva, walinzi na wale wengine zile kada za chini kwenye *level* za Halmashauri wale wakubwa wanapata *per diem*, wanapata *overtime*, wanapata *extra duty*, wengine hawa anaweza kukaa kwenye utumishi wa umma, akafika hata miaka 10 hajawahi kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Agnesta Lambert ajiandae.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda na mimi nichangie hii hoja ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. mimi nitazungumza kwa uchache sana kwa habari ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo ambalo linafanya tasnia nzima ya Utawala Bora katika nchi yetu iwe na dosari kubwa sana sana. Kuna hizi sheria, hii ya *The Anti Money Laundering CAP 423* ya mwaka 2006 ambayo ilifanyiwa marekebisho na Bunge hili mwaka 2019, inajulikana kama Sheria ya Utakatishaji Fedha na hii Sheria ya *Economic and Organization Crime Act.* ambayo *CAP 200* ya mwaka 1984 ambayo pia ilifanyiwa marekebisho na Bunge hili mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Ugaidi ambazo zinahamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sheria tatu zinaifanya dhana ya utawala bora katika nchi yetu itiliwe maswali sana. Kwa mfano Bunge hili wakati linapitisha sheria hii au kufanya marekebisho sheria hii na sheria hii kufikia mahali kwamba haina dhamana kabisa, nia ya Bunge ilikuwa nzuri, lakini katika utekelezaji wake imeingia dosari nydingi sana, kuna watu wengi sana wapo ndani, wapo mahabusu maelfu ya watu kwa sababu ya hili suala la utakatishaji fedha, kubambikiziwa na watu wasio waaminifu katika vyombo vyetu vya dola na kwenye nchi yejote makini jambo hili haliwezi kuachiwa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtu anakwenda kwa mfanyakishara kukusanya mapato au kudai mapato au malimbikizo ya mapato anakwenda na *charge* kabisa anamwambia bwana usiponipa fedha kadhaa tayari nina hati hii hapa ninakuwekea *money laundering* au ninakuwekea *economic sabotage* kuna watu wengi sana wapo ndani, wapo mahabusu kwa sababu ya matumizi ya

mabaya ya hawa watu wasio waaminifu ambao tumewakabidhi kuitekeleza hii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo kwa mujibu wa takwimu kuna watu 1,701 ambao wako mahabusu kwa sababu ya ama kwa ajili ya *money laundering* au kwa sababu ya *economic sabotage* na kwa sababu hiyo nilikuwa nafikiri ni muhimu sana, kwakuwa kazi moja wapo ya Bunge letu ni kutunga sheria lakini na kufanya marekebisho sheria na kufuta baadhi ya sheria, haileti *sense* kwa nini mpaka leo wale Masheikh 23 wa Uamsho wa Zanzibar wapo ndani mpaka leo mahabusu, leo ni miaka tisa, haileti *sense* kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kuwaza ningkuwa mimi au angekuwa baba yangu, au angekuwa ndugu yangu ambaye mpaka leo miaka tisa yupo ndani, hajahukumiwa bado na haijulikani ana hatia au hana hatia. Itakuwaje baada ya miaka 20 huyu mtu mkagundua hana hatia, atalipwa nini *in-exchange* na miaka aliyopoteza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kwa kweli haliingii akilini kwanini hawa Masheikh 23 wa Uamsho wa Zanzibar wapo ndani mpaka leo kwa miaka tisa, lakini haitoshi kuna Masheikh 64 huko Arusha ambao nao wapo ndani kwa sababu ya hizi hizi Sheria za Ugaidi ambazo hazina dhamana kwa sababu ambazo hatuzielewi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashangaa kwa nini Masheikh tu wapo ndani kwa ajili ya Sheria za Ugaidi hakuna gaidi mwingine ambaye sio Sheikh? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri husika pamoja na Serikali kwa ujumla tuangalie kwa undani sana namna ya kuli-*handle* suala hili, kwa sababu sio sahihi Masheikh hawa wakawa ndani kwa muda wa miaka tisa, sisemi kwamba wana hatia au hawana hatia sijadili kosa lao, lakini ninachojadili ni kwamba basi wangehukumiwa basi ikajulikana. Wangehukumiwa wangejua wamebakiza miaka mitatu/miaka minne/miaka mitano/miaka sita. Lakini sasa

wapo ndani bila kujua watamaliza lini matatizo yao mimi nilikuwa naomba Wizara pamoja na *by-imprecation* Waziri wa hii Wizara ni Mheshimiwa Rais, na Mheshimiwa Rais wa nchi ni Rais wa nchi lakini pia ni Waziri wa hii Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba jambo hili lifanyiwe kazi, kuna watu wengi sana, rafiki yangu mmoja akanipigia simu akaniambia Askofu kuna watu wamekuja kwangu wananiambia ama niwape milioni 100 ama wanipe *money laundering*, nikamwambia wape haraka haraka utapata *money laundering* na utashindwa namna ya kutoka.

Nilikuwa nashauri sana sana kwa ajili ya kuondoa dorasi zinazotokana na kusemwaa kwamba Tanzania hatuna utawala bora, tuweze kuziangalia kwa makini hizi sheria, tuzi-revise na naomba sana rafiki yangu Mheshimiwa Mchengerwa ulifanyile kazi hii Masheikh hawa 23 na Masheikh hawa 64 ambao wapo ndani utafute namna ya kufanya, vinginevyo nitakuondolea shilingi kwenye bajeti yako. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mheshimiwa *Engineer Isack Kamwelwe* ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Utumishi na Utawala Bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninapenda tu niishauri Serikali yangu kwamba suala la watumishi wa umma kwenye Wizara ya Afya na Elimu ni muhimu sana, kwa sababu tunapozungumzia maendeleo ni lazima tuhakikishe kwamba wananchi wetu wana afya njema. Kwa hiyo, watumishi wamepungua sana kwenye maeneo hayo kwa hiyo wapelekwe watumishi wa kutosha na kwamba tumesikia juzi kwamba kuna ajira mpya ya kwenda kwenye maeneo hayo. Basi ajira hizo zifanywe kwa wepesi kwenye maeneo hayo (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia, tunazungumza suala la demokrasia katika nchi yetu, tunamshukuru Mungu sana nchi yetu imeendelea kuwa vizuri zaidi kwenye masuala ya demokrasia na ndio maana maendeleo yanazidi kupaa kwa kasi katika nchi yetu ya Tanzania. Niseme tu hapa mimi nitazungumzia kidogo kwenye suala la ukatili wa kijinsia. Kumekuwa na ukatili wa kijinsia hasa kwa Wabunge wa Viti Maalum wa vyama vyote tunapokuwa tunawajibika kwenye maeneo yetu kutekeleza wajibu wetu kama Wabunge wa Viti Maalum, tumekuwa tukinyanyapaliwa, tukinyanyaswa na Wabunge wenzetu wanaume kwa maana ya hofu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa pale ambapo Mbunge wa Viti Maalum anatoka Jimbo moja na Mbunge wa Jimbo hilo, wanakuwa na wasiwasi hofu yao ni kwamba Mbunge wa Viti Maalum akifanya kazi eneo hilo maana yake mwisho wa siku atapata *mileage* na kwamba anaweza akagombea Jimbo. Mimi niwaombe tu ndugu zetu Wabunge wenzetu kwamba sisi sote tunajenga nyumba moja mtupe nafasi tufanya kazi kwenye maeneo yote bila kutuwekea vipingamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii unyanyapaa huu sasa hivi umekuwa ukiota mizizi, tumekuwa tukitishiwa, tunaambiwa maneno makali na hata wakati mwingine kutudhoofisha ili tusiweze kufanya kazi. Niombe sana Mheshimiwa Rais jana ametoa hotuba nzuri sana, kwa hiyo niseme tu kwamba tunamsubiri mama yetu akabidhiwe kijiti kwenye chama, sisi kama Wabunge wa Viti Maalum tunaopitia Chama cha Mapinduzi tutakwenda kwake ili atusaidie namna gani tuweze kufanya kazi ili kukomesha huu unyanyapaa kwa Wabunge Wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye masuala ya biashara. Juzi juzi; ni wiki tatu tu baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tumesikia hotuba ya Mwenyekiti mmoja ambaye ana Mbunge mmoja wa chama chake ndani ya Bunge, lakini ana Wabunge 19 wa Viti Maalum akizungumzia kunyanyaswa na kufanyiwa vitu tofauti dhidi ya biashara zake. Sasa nataka

Watanzania watege masikio ninataka niwaeleze ukweli juu ya masuala mazima yanayohusiana na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu ile ameizungumza hadharani na amehutubia katika ..., kwanza inasikitisha sana muda mfupi tu baada ya Rais wetu kufariki badala ya kuja aeleze katika maelezo yake na masikitiko yake angeeleza hata baadhi ya kazi nzuri ambazo amezifanya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, badala yake ameeleza kinyume chake, lakini hatumshangai ni kwa sababu alikuwa anatetea tumbo lake. Niseme tu alieleza kwamba Serikali ilimfanyia ukatili wa kuzuia biashara zake na kuzifunga.

Mheshimiwa Spika, ukweli uko hivi, katika biashara yake ye ye zile biashara anazozifanya ni za urithi wa kifamilia, na kwa kuwa ni za urithi wa kifamilia ye ye amejimilishika kama za kwake na kwamba hatoi mrejesho kwa ndugu zake, kwa hiyo ndugu zake wakaenda mahakamani, walivyokwenda mahakamani wakataka haki itendeke. Mahakama ikatoa amri ya kufunga biashara zake ili asiendelee na biashara mpaka mgogoro utakapokwisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii anakuja anawadanganya Watanzania, anatafuta kuendelea kujipambanua kisiasa na wananchi wamwamini, hii si kweli na haikubaliki. Kwa hiyo, arudi akamalize mgogoro na familia yake asisingizie Serikali kwa imemnyanyasa na kumfungia biashara zake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuna jengo la Bilcanas lile jengo lilikuwa ni la Serikali la *National Housing*. Amekaa pale miaka na miaka halipi kodi anapenda vitu vya bure. Serikali ilipokuja kudai kodi analeta blaa blaa, Serikali iliyokuwa inaongozwa na Dkt. Magufuli ilikuwa haitaki blaa blaa na hata hii sasa inayoendeshwa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan nayo haitaki blaa blaa. Asiyelipa kodi akae pemberi. Kwa misingi hiyo... (*Makof*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani kuna Taarifa. Mheshimiwa Aida Khenani.

T A A R I F A

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji lakini pia niombe kiti chako kituongoze. Mimi ni Mbunge wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo - CHADEMA, kinachozunguzwa hapa ni Wizara ya Utumishi, kuzungumzia maisha ya mtu binafsi ndani ya Bunge ambaye hawezi kujibu, tena hazungumzii mambo ambayo yanayohusu mjadala uliopo anazungumza maisha yake binafsi, tuna Kanuni zetu niombe utaratibu wa kiti chako utuongoze. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Kwanza umesimama kwa Kanuni ya Taarifa, na Taarifa huwa anapewa mzungumzaji sio mwongozo wa kiti, lazima na wewe uwe umezitazama Kanuni vizuri. Na umesema vizuri hoja iliyopo mezani ni ya Utumishi na Utawala Bora, na Kanuni zetu zinaruhusu mtu ambaye alijadiliwa humu ndani kama anaona kile alichojadiliwa amevunjiwa heshima ama hakijawekwa kwa namna ambayo ni uhalisia, Kanuni zetu zinaruhusu namna yeye anavyoweza kuleta malalamiko. (*Makof*)

Sasa Mheshimiwa aliyekuwa anachangia, mimi huwa nasikiliza hapa kila neno linalozungumzwa nasikiliza, Mheshimiwa anayechangia anasema huyu aliyetajwa alisema hoja hizo kuonesha nchi hii haina utawala bora na hoja iliyoko mezani inahusu utawala bora. (*Makof*)

Kwa hiyo yupo sahihi kwa mchango wake, lakini kuhusu taarifa anazozisema kama kuna mtu humu ndani anafikiri anasema uongo asimame kwa kanuni inayosema kama Mbunge anazungumza uongo. Na kama yeye akisema uongo kuhusu huyo mtu Kanuni zetu zinaruhusu ataleta malalamiko yake kwa Mheshimiwa Spika utaratibu wa

kawaida utachukuliwa kama huko nyuma ambavyo imewahi kutokea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana bado dakika zangu sita naendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapinzani wamekuwa wakiitupia sana Serikali malalamiko juu ya matumizi ya fedha za umma, ni jambo jema, lakini tunapozungumza usawa na kuangalia namna ya uwasilishaji wa mambo yenye ni vizuri sasa wewe mwenyewe unayewasilisha jambo hilo ukajitazama kwanza, wanasema tazama kibanzi cha jicho lako kabla hujamuonesha mwenzako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa misingi hiyo nataka niseme Chama cha Demokrasia na Maendeleo tunataka watueleze miaka mitano iliyopita fedha za ruzuku wamefanya nini? Wamekuwa wakilipwa shilingi milioni 310 huyo Mwenyekiti huyo aseme shilingi milioni 310 kila mwezi, nimekokotoa vizuri nikapiga mara miezi 12 na mara miaka mitano nikakuta kwamba ni shilingi bilioni 18.6 ambazo chama hiki kimepelekewa pesa hiyo na kwamba katika utekelezaji wa majukumu yao dhidi ya ruzuku hii hawajajenga hata jengo moja ambalo lingewasaidia sasa kuonyesha taswira nzima ya chama chao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ikapelekea kwamba walishindwa kufanya uchaguzi kwa sababu hawakuwa na pesa, badala yake wakaja wakaanza kusema kwamba uchaguzi...

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: ...haukuwa wa haki haukuwa huru. Wewe ndugu yangu umekaa kwenye kiti tulia mambo yaendelee, wenzako wako nje huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme sasa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani subiri kidogo.

Mheshimiwa Aida Khenani umeshatoa Taarifa kwa Mbunge huyu tayari wakati anachangia, labda usimame kwa Kanuni nyingine. Umeshatoa taarifa kwa Mbunge huyu anayechangia, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe alipoona ameshafilisi kabisa chama chake akaamua kumsusua Tundu Lissu uchaguzi na kwamba sasa Tundu Lissu akawa anafanya peke yake, lakini ofisi hawana, lakini pia Mheshimiwa

Mheshimiwa Naibu Spika, bado dakika zangu tatu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa David Kihenzile anasema ameshamaliza kuongea, kwa hiyo huwezi kumpa Taarifa Mbunge ambaye ameshamaliza kuzungumza ahsante sana. Ahsante sana.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Ameshamaliza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani hamna Mbunge anatoa taarifa zaidi ya mara moja kwa mtu mmoja, tafadhalii. Mbunge unapotoa taarifa kwa Mbunge huwezi kuwa mnajibizana ninyi, ukishatoa taarifa umeshatoa mwambie jirani yako asimame ampe hiyo taarifa.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Umesema umemaliza Mheshimiwa ndiyo maana nimeikata ile taarifa nyingine kule ama nimesikia vibaya? Ulikuwa umemaliza au hapana?

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Alikuwa bado, bado hajamaliza Mheshimiwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimwa Wabunge, tusikilizane nazungumza na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani msimsaidie kujibu.

Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani nilizuia ile taarifa ya Mheshimiwa David Kihenzile nikifikiri umeshamaliza kuzungumza, si umeshasema unaunga mkono hoja. Mheshimiwa haya Mheshimiwa David Kihenzile.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika,

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa nilikuwa nataka kumpa Taarifa mzungumzaji kama viongozi wa chama fulani wametueleza mambo ya utawala bora kwa miaka mitano mfululizo na tumeshuhudia ndani ya chama kwa maelezo ullyotupatia. Nataka kumpa taarifa kuanzia sasa kwa kuwa pesa zimetumika zote hizo za ruzuku na hakuna chaguzi za ndani, wamekosa *legitimacyna moral authority* ya ku-question viongozi wa Serikali katika nchi hii kwamba hakuna utawala wa sheria. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nadhani wote tunazo Taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, ile taarifa ndiyo inayotuongoza kama huko kuna shida au hakuna shida. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani malizia.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Kwa hiyo, Mheshimiwa yule mwenye Mbunge mmoja wa Jimbo Bungeni humu alienda kununua matrektu mawili, hayo matrektu mawili hayajulikani yaliko mpaka leo hii. Lakini amekuwa akizungumza kwenye maelezo yake kwamba kulikuwa na dhambi na ubatili mkubwa sana kwenye utawala wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mama Samia; hii si kweli kwa sababu hawa watu kama ndivyo ina maana kwamba ubatili wao ni kujenga zahanati 1,900? Ubatili wao ni kujenga hospitali 400 zaidi? Ubatili wao ni kujenga flyover? Ubatili wao ni kununua ndege? Ubatili wao ni kujenga barabara? Haikubaliki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Nbu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnesta Lambert atafuatiwa na Mheshimiwa Isack Kamwelwe, Mheshimiwa Aloyce Kwezi ajiandae

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na mimi niende moja kwa moja katika mchango wangu. Nitakwenda kuanzia walikoishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu hususan Mheshimiwa Nape Nnauye.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inataka watumishi wa umma wapandishwe madaraja kila baada ya miaka mitatu, hiyo ndiyo sheria inavyotaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kumekuwepo na watendaji wa taasisi mbalimbali ikiwemo utumishi wa umma wamekuwa wakishusha nyaraka mbalimbali ambazo zinakinzana moja kwa moja na sheria hii ambayo nimeitaja awali na nyaraka hizi zimekuwa zikielekeza kwamba watumishi wapandishwe madaraja kila baada ya miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunaye Waziri husika Mheshimiwa Mchengerwa, ningependa atakapokuja ku-*wind up* atueleze ni kwa nini basi Wizara imeamua kukiuka Sheria hii ya Watumishi wa Umma kwa nini wameamua basi kukiuka sasa sheria hii na sasa wametengeneza nyaraka tofauti kabisa ambazo zinapingana na haki za watumishi wa umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nilivyosimama mbele yako wapo watumishi wengi ambao ni takribani miaka sita hawajapandishwa madaraja na nimesema kuna nyaraka ambayo inakinzana na sheria yenyewe ambayo inasema watumishi hawa wa umma wapandishwe madaraja ndani ya miaka mitano, lakini sasa hivi hata hilo ambalo haliendani na sheria wameshindwa kulitimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kwamba watumishi wa umma ndiyo kiungo pekee cha Serikali katika utekelezaji wote wa bajeti tunazopitisha, mipango yote ambayo tunaipima, tunaipanga, lakini maslahi yao yamekuwa hayaangaliwi. Kama jinsi ambavyo nimesema watu walipaswa kupandishwa madaraja miaka sita iliyopita na watumishi hawa wanaendelea kuchapa kazi na watumishi hawa wanaendelea kutarajiwa kwamba *wa-deliver* vizuri kulingana na taratibu za utumishi jinsi zinavyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unasema ukitaka kumtawala mtu unapaswa kuhakikisha anakula na kushiba. Ikiwa tunahitaji watumishi hawa wa umma waweze kufanya kazi kwa ufanisi hatuna budi kuangalia maslahi yao ikiwemo kupandishwa madaraja, ikiwemo kulipwa/kuongezewa mishahara, lakini pia ikiwepo kulipwa malimbikizo yote ambayo watumishi hawa wa umma wanayadai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Serikali kuhakikisha inatoa mafunzo kwa watumishi wa umma na mafunzo siyo *luxury*, siyo kwamba ni starehe, hapana, tunaishi katika dunia ambayo inakwenda kwa kasi, teknolojia zinakwenda kwa kasi. Ninavyosimama hapa mbele yako ni miaka sita imepita hakuna mafunzo yaliyofanywa kwa watumishi wa umma hawa. Lakini watumishi hawa tunategemea na kuwatarajia waweze ku-*deliver* kulingana na jinsi teknolojia inavyokwenda jambo hili haliwezekani na haliendani na uhalsia kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ufanyike utaratibu wa haraka wa kuhakikisha watumishi hao wa umma wanapatiwa mafunzo na siyo tu suala la kupatiwa mafunzo; watumishi wetu wanapaswa kupata *exposure*, mtumishi unakuta yupo kazini zaidi ya miaka sita, lakini hajawahi hata siku moja kwenda nje angalau kupata mafunzo au hata kupata *exposure* tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi dunia inavyokwenda lazima tukubali kwamba watumishi wetu

wanapaswa kwenda sambamba na *the way* dunia inavyokwenda kwa kasi.

Kwa hivyo basi, ushauri wangu kwa Serikali na hususan kwa Wizara husika waangalie uwezekano mkubwa sana wa kufuta hii *damage* ya kuwa na watumishi ambao takribani miaka sita hawajapata mafunzo na mwisho wa siku ndiyo maana tunawakuta Wakuu wa Wilaya mfano Mkuu wa Wilaya tu anakwenda kwenye eneo lake la kazi, anakutana na watumishi wale ambao wako chini yake, badala ya kuwaelekeza namna ya kufanya kazi, hata akikuta wamekosea kidogo mwisho wa siku anawachapa viboko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwengine tunaweza kudhani kwamba wanafanya makusudi, wakati mwengine hawajui hata wajibu wao, mwisho wa siku wanadhani hata kupiga viboko ni sehemu ya majukumu yao. Ndiyo maana nasema suala la mafunzo kwa watumishi wetu wa umma ni lazima na ni takwa la kisera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo upande wa utumishi tunatambua au niseme natambua kwamba zipo taratibu na kanuni zinazotongoza au zinazoongoza Wizara husika kuwajibisha watumishi wa umma pale ambapo wanakutwa na makosa mbalimbali. Lakini hivi ninavyoongea na wewe hapa kupitia Bunge lako Tukufu, wapo watumishi wengi ambao wamewekwa *bench* kwa masuala mazima ya nidhamu. Watumishi hawa wengine wamekaa zaidi ya miaka mitatu/minne mpaka mitano wako *bench* wanafamilia, wanatunza familia, wanapeleka watoto shule maisha yao yote yanategemeana na kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini watumishi hawa hawapewi hata ile nusu mshahara ambayo kikatiba kisheria na kikanuni unapokuwa umewekwa *bench*, haujakutwa na hatia lazima ulipwe nusu mshahara. Lakini mtumishi huyu yuko miaka minne na wakati yuko kazini alikopa, wote tunatambua mishahara ya watumishi wetu hawa siyo mikubwa, haiwezi ikawafanya wakaishi *comfortable*.

Kwa hiyo, watumishi hawa wamekuwa wakikopa walipokuwa kazini, wapeleke watoto shule, wale, walipe kodi za nyumba, wengine hata kujenga hawana uwezo wa kujenga. Lakini leo hii wamewekwa *bench* kwa takriban ya miaka minne hawapewi hata senti wanaishije. Je, unadhanu wale ambao wapo wanaendelea na kazi wanapokuwa wanaona yanayowapata hawa waliopo *bench* watashindwa kuchukua rushwa, kweli watakuwa ni waaminifu? Haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe kupitia Wizara na Mheshimiwa Mchengerwa nimekuwa chini ya uongozi wako ukiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba na Sheria, nakujua utendaji kazi wako naujua, *commitment* yako najua kwa Taifa hili, nikuombe chonde chonde uangalie ni namna gani sasa ya kwenda kufuatilia mambo haya wengine wamesimamishwa siyo kwa sababu wanamakosa, ni kwa sababu waliowasimamisha wana bifur tu ni kwa sababu wanawasimamisha wanadhani wanawezafanya chochote *as long as* wao wako kwenye madaraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ambalo nimelisema kuhusiana na Wakuu wa Mikoa Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wote tunatambua hawa ni wateule wa Mheshimiwa Rais. Unapokuwa mteule wa Mheshimiwa Rais, ukaenda huko chini katika majukumu yako ya kila siku unakwenda kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, sasa unapofika kule ukafanya vitu ambavyo haviendani na miongozo ambayo sisi wenyewe tulisaini kama watumishi kwamba tutakuwa na maadili, tutaongoza kwa kuongozwa na miongozo hii ya maadili, mwisho wa siku Serikali ambayo inasimamiwa na Mheshimwia Rais inapata taswira mbaya kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* natamani nisikie angalau unatoa tamko kwa Wakuu wa Wilaya, kwa Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi ukiwaelekeza namna ya kufanya wakati tunaandaa mafunzo ambayo nimeweza kuyasema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja lingine niombe au niseme ushauri kwa mambo yote ambayo nimeelezea hapa kuhusiana na watumishi wa umma, kwa mambo yote ambayo nimeeleza hapa hususiana na utawala bora, Mheshimiwa Waziri nikucombe mambo makuu matatu; la kwanza chonde chonde waangalie watumishi hawa wa umma ambao waliwekwa *bench* ambao mpaka sasa hivi wengine wamekimbia vijjini, vijjini na kwenyewe wamekuta matatizo ya wazazi wao hawawezi kabisa kujisaidia wao hata kusaidia familia zao, uchunguzi ufanyike haraka Mheshimiwa Waziri, ufanyike uchunguzi ambao hawana hatia warudi kazini na wakirudi kazini...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga ahsante sana.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sekunde nimalize ushauri kwa Serikali. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Utashauri kwa maandishi muda wetu hautoshelezi ahsante sana.

Mheshimiwa Isack *Engineer* Kamwelwe atafatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo ajiandae.

MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina hazina kubwa sana ya viongozi wetu wastaa fu ambao wamepita ngazi za juu, kuanzia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pamoja na Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Marais upande wa Jamhuri ya Muungano, lakini na Zanzibar; tunao Mawaziri Wakuu wastaafu, tunao Makamu wa Rais wastaafu, tunao *Ma-chief Secretary* wastaafu, lakini pia tunao mpaka Maspika na Naibu Maspika wastaafu. Hawa viongozi wetu ni hazina kubwa sana kwa nchi yetu. Ukienda kule Ulaya wenzetu wana Mabunge ya waliochaguliwa, lakini kuna Bunge ambalo wanaita kwa mfano kama Canada wanaita *The House of Queen* na Uingereza wanasema *The House of Lord*. Hili Bunge la pili linakuwa na wale viongozi wastaafu ambao walishatumikia zile nchi na kila muswada unapopitishwa na Bunge la waliochaguliwa hauwezi kupita moja kwa moja, lakini lazima uende ukapate ushauri kwanza kwa wale viongozi wastaafu ambao walishatumika katika zile nchi na kwa kufanya hivyo nchi inakwenda vizuri na utawala bora unakwenda vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, Ndugu yangu Mchengerwa jaribu kuliangalia hili na ikiwezekana kutengeneza mfumo rasmi katika nchi yetu ili tuweze kuwatumia hawa viongozi wetu wastaafu kwa sababu wanayohekima, wana busara nydingi na bado wanauzoefu mkubwa wanaweza wakatushauri hata katika ndani ya Bunge, hilo liliikuwa la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Jimbo langu na nimuombe sasa Mheshimiwa Waziri anisikilize pamoja na Naibu Waziri. Jimbo langu wananchi kwa kutumia Mfuko wa Jimbo pamoja na michango yao walijenga zahanati kumi kwenye hii miaka mitano iliyopita katika hizo zahanati kumi ni zahanati mbili mbili tu ndiyo ambazo zimefunguliwa, zahanati nane bado kwa sababu ya kukosa watumishi. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba hizi zahanati nane, mtakapo fanya ajira utuletee watumishi ili wananchi waendelee kufaidi jasho lao, wamejenga zahanati wenyewe lakini wanakosa huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nataka nizungumzie Shirika letu la Reli na nimpongeze sana

Mheshimiwa Rais jana katika hotuba yake amezungumza jinsi gani ambavyo Serikali imekarabati reli ya kutoka Tanga kwenda Kilimanjaro mpaka Arusha na baada ya kukarabati reli hiyo kumekuwa na manufaa makubwa, ajira zimeongezeka, lakini pia mzigo kutoka Tanga wa *cement* kupeleka Kilimanjaro na Arusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu *train* inavuta mabehewa kumi ya *cement* bei imepungua tofauti na kubeba na lori. Hoja yangu nini, ukarabati ule umefanywa na Watanzania, vijana wetu na waliofanya ngazi ya darasa la saba na kushuka chini. Vijana hawa ile reli ilikuwa imechoka sana wamefanya kazi nzuri, tulikuwa tuna mapendekezo kwamba hawa vijana wangefikiriwa kuajiriwa kama wanavyoajiriwa watu wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mfumo wetu wa ajira una sheria unasema kwamba hauwezi kuajiriwa mpaka awe amefika *form four*, ni *form four* gani ambaye atakuwa pigilia, ni *form six* gani ambaye atakubali kufanya ya pigilia, akakae kule kwenye magenge. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kama inashindikana basi hiyo sheria ifanyiwe *amendment* kwa kuletwa hapa Bungeni ili angalau tuweke tu hiyo kwamba ni *special* tuwaajiri hawa vijana, waendelee kutengeneza ile reli. Kwa sababu tukiacha itaharibika tena kama ilivyokuwa imeharibika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, na mimi nizungumzie kidogo suala la utawala bora, lakini kwa kusema nini maana ya nidhamu, nini maana ya heshima, kwa sababu nikichukulia mfano kwenye Halmashauri kumekuwa na tabia ya kuwahamisha watumishi hovyo hovyo kwa matakwa ya mtu mmoja anayeitwa Mkurugenzi, *transparentinakosekana*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nipo mtumishi niliwahi kwenda Canada, Montreal, ndiyo nilikokwenda kujifunzia kozi yangu ya *leadership*, nilichokigundua kule tulipewa semina kama wewe ni Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda, kiwanda kinazalisha vizuri na *marketing officer*

wanafanya kazi vizuri, yule Meneja wa Uzalishaji usimpandishe madaraka, usimpe cheo kwa kumpandisha madaraka ile *skill* aliyokua anafanya azalishe zaidi. Lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Aloyce Kwezi, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Contantino Mwakamo, Mheshimiwa Ally Kassinge, ajiandae.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri kwa uteuzi, Naibu Waziri nakupongeza watumishi wote wa Wizara hiyo ya Menejiment ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa kuangalia wananchi na watumishi walioko katika jimbo langu, Jimbo la Kaliua, pale tuna watumishi karibu 2,800; wamenituma watumishi hawa, natambua pamoja na watumishi wengine kwenye utumishi wetu kwenye nchi hii ya Tanzania wanaitaji kulipwa fedha zao kwa maana ya madai, madai haya mara ya mwisho imelipwa mwaka 2016; mwaka 2017 uhakiki umefanyika wa madai ya likizo, madai ya matibabu, madai ya uhamisho, madai ya mafunzo watumishi hawa hawajawahi kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumefanya uhakiki nchi nzima, lakini kulipa hatujawahi kuwalipa. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe watumishi hawa tuwarudishie morali yao ya kufanya kazi kwa kuhakikisha wamelipwa maslahi yao. (*Makofi*)

Niomba niongelee malimbikizo ya mishahara, hapa napo kuna changamoto kubwa sana, mtu amepanda daraja mwaka 2012, mwaka 2014 mchahara ukabadilika anadai

malimbikizo, sasa miaka hii yote malimbikizo bado hajalipwa, shida ni nini? Watumishi hawa tunawavunja mioyo, watumishi wamefanya kazi kubwa sana za kubadilisha maendeleo makubwa sana kwenye nchi yetu, hata kwenye jimbo langu bado wanaendelea kujenga hospitali, madarasa wanasiimamia wanafundisha watoto wetu, lakini kwa kweli morali ya watumishi inashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia watumishi hawa hata *increment* mara ya mwisho ni mwaka 2014 kupata *increment*, walikuwa wanapata kila Julai wanapata *increment* kwenye mshahara kunaongezeka fedha kidogo, wanaweza kukopa, sasa matokeo yake kule kwenye utumishi sasa hivi mimi naona kama hadhi ya watumishi wa umma imeshuka kidogo. Imeshuka kwa sababu watumishi wanakopa kuliko kiwango, napengine tumewadhibiti kupertia mfumo wa *Lawson* wa utumishi ambao upo kwamba wanakopa *one third*, lakini wanakwenda kukopa kwenye wakopeshaji bubu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakabidhi saa nyingine mpaka kadi zao benki, sasa tunakwendaje? Mimi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri waangalie sekta ya utumishi waiboreshi ipasavyo, na pengine kwa wale wastaifu sasa, hapa napo kuna shida, mstaifu anastaifu anadai malimbikizo hajalipwa, lakini kinachoumiza sana wastaifu unapostaifu unafatilia michango yako unakuta Wizara ya Fedha namuomba sana kaka yangu Mheshimiwa Mwingulu Nchemba watumishi unakuta hatukuchangia ipasavyo na ninyi pale mnachelewesha pelekeni zile fedha za wastaifu kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wastaifu hao waweze kulipwa fedha zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe umestaifu umefikisha miaka 60, umefikisha miaka 55 unakuta kuna *gap* kubwa sana huku nyuma, una miaka miwili kwamba hukuchangia, fedha yako haijaenda, anaanza kuzunguka huyu mzee, utumishi wa umma anatakiwa aone furaha ya kultitendea kazi Taifa lake, lakini hapa bado lipo shida. Niombe nashukuru sana wakati wanawasilisha TAMISEMI hapa

wakaongea kwamba tunaenda kuziangalia *RS* zile Sekretari za Mikoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namshauri Waziri wa Utumishi, shida iko hivi pale kwenye *RS* ili twende na utendaji mzuri watumishi wengine wa *RS* wamekuwa ni ma-junior hawajafikia kwenye *senior post*, hawajafikia kuwa waandamizi. Sasa mtu ajafikia kuwa mwandamizi kwenye Halmashauri kuna watu wana miaka zaidi ya kumi na tano, Maafisa Mipango, Maafisa Utumishi, Wakuu wa Idara, wenye sifa za kutosha kupanda kwenda *RS*, tumewaacha wale pemeni, tunaangalia *RS* mtumishi ana miaka miwili, anakuja kuongoza, ana mwongoza Afisa Mipango mwenye miaka 15. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kuna muda tulikuwa tunaona vichekesho kwa sababu wewe inabidi kumshauri sasa kwamba ndugu yangu hiki hapa kipo moja, mbili, tatu. Sasa ni nini hiyo *succession plan* iko wapi, maana yake mfumo wa kurithishana madaraka wale ambao wako *competent* kwenye *level* ya Halmashauri wapande kwenda Mikoani wale ma-senior. Sasa sisi tunaacha huku tunampa mtu wa miaka miwili anamwongoza mwenye miaka 20 yule kule ana *Ph.D* ana *Masters*, anafanya kazi vizuri, kwa nini tusichukuane yule tukapandisha wale ambao wanaanza *at least* ajifunze? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili linafanana, shida ambayo ilitukuta kwa Hayati ndio *succession plan* yenye hiyo, mama yupo *competent* kachukua nafasi pale, shida iko wapi? Kwa nini huku bado kuna *gap*? Kwa hiyo, nilikuwa nashauri tuangalie vizuri eneo hilo ili tuweze kwenda pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kikubwa zaidi ni kuboresha vitendea kazi, tunawasaidia Waratibu wa Elimu wa Kata pikipiki, tunasahau Watendaji wa Kata, Maafisa Tarafa. Sasa kwenye kata mkubwa wa kata ni Afisa Mtendaji wa Kata, sasa Afisa Mtendaji wa Kata pembeni hakuna *ka-incentive* kokote kwake, tumeangalia yaani chini yake kule

kuna mtu anapata posho ya madaraka, sasa kwa nini na wenyewe tusiwaangalie ili twende vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu kwenye sekta ya utumishi, nataka nichangie sehemu moja mahususi kweli kweli. Maana ukiangali Maafisa Kilimo wachache, hata kwenye jimbo langu ni hivyo hivyo, ukiangalia manesi wachache, ukiangalia sijui nini wachache. Lakini hebu twende kwenye *human resource allocation* tupange watumishi wetu vizuri, *centers* zina watumishi wamezidi. *Centers* kubwa zinawatumishi wamezidi, miji zimezidi, manispaa zimezidi, sijui wapi imezidii, kule unakuta mwalimu wawili, watatu. Ukiangalia sehemu fulani hakuna uwiano wako 40/50 sasa tunasaidia Taifa au tunakwendaje kwenye mfumo huo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiria tuwapange kwanza vizuri hao, lakini tuajiri watumishi wa kutosha kwenye sekta zetu. Afisa Ugani mmoja ana *control* kata mbili tunategemea kweli kilimo kiinuke hapa? Bado itakuwa ni changamoto. Utumishi niwashauri kingine, ikama zinaidhinishwa kila mwaka za kuajiri, tuna miaka hatujaajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Kassinge, Mheshimiwa Hassan Mtenga ajiandae.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kama walivyoanza wenzangu kuwapa shukrani Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazoendelea nazo hasa kwa kuanzia hotuba ya bajeti ambayo Waziri ameiwasilisha jana na ameonesha ni namna gani amejipanga na namna gani anayajua yaliyo ndani ya masuala ya utumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wameona na ameguswa na shida za watumishi na hii inaonesha ni kwa namna gani ndani humu Wabunge tumekuwa wawakilishi wa kweli wa wananchi kwa nafasi zote. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na michango mingi ambayo wengi wameisema na nisingependa sana niirudie kwa sababu itakuwa ni kula muda na watu wanatakiwa kuchangia, lakini nina maeneo machache ambayo na mimi nataka nianze kuzungumza. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la maslahi ya wastaaifu na hasa katika masuala mazima ya upatikanaji maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe niseme kwamba katika nchi hii sasa hivi na hata hususani kwenye jimbo langu kuna watumishi wengi wamestaifu, lakini shida hata kufungishwa mizigo kurudishwa imekuwa mtihani na umekuwa mtihani mkubwa sana na kulifuatilia jambo hili ukipeleka kwenye Ofisi ya Wizara ya Utumishi wanakuambia watumishi wengi wako kwa Mkurugenzi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima tukiri, humu ndani wote tumezungumza ni namna gani Halmashauri nydingi zimekuwa na mapato yawe madogo na ni namna gani Halmashauri zimekuwa na mzigoo mkubwa wa kuendesha shughuli za Halmashauri. Wanawezaje kuwasafirisha watumishi hawa na kuwarudisha makwao kwa sababu sehemu kubwa ya watumishi kwa sasa hivi kwenye nchi hii wanapatikana kwenye hizi Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeiomba Wizara ya Utumishi, jambo hili walitazame kwa kina, walichukue, walifanyie kazi, pamoja na kwamba majukumu hayo wameyaacha kwa Halmashauri, lakini vyema wakalifanya kazi wakawasaidia wakaja na mpango

unaoweza kusaidia kuondoa tatizo hili kwenye watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo wapo watumishi wamezungumza akiwepo Mheshimiwa Nape Nnauye alizungumza namna watumishi wanavyopata taabu kwenye maslahi na hasa hasa maslahi yao ya kustaafu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata wageni hapa, Naibu Waziri anafahamu, nililazimika kumtafuta anisaidie kujibu hoja zao. Watumishi wale walisahaulika kwenye bajeti, walikuwa wanastahili kupanda vyeo, lakini katika mazingira yasiyoyakueleweka wakasahafulika kupanda vyeo. Kwa bahati mbaya wakapewa wengine barua za kupanda vyeo vyao wale ambao walibahatika, lakini kilichotokea wamekosa mshahara haujabadilika, na wengi wa timu hii wamestaafu, wamekuja kwangu hapa mjini Dodoma, tumekwenda kwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha kwasababu wameshastaafu hawawezi kurekebishiwa zile haki zao, sasa watu hawa tunawasaidiaje? Na hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali ya kushughulikia matatizo na watu walikuwa na mazingira magumu. Ni kwa namna gani sasa sisi tunaona ni namna gani tunaweza tukawasaidia watu hawa, twende tukawatengeneze utaratibu maalum na ikiwezekana Waziri apite kwenye maeneo hayo, apate hayo makundi ambayo yana matatizo na hatimaye atengeneze mpango maalum uletwe kwenye Serikali tuwasaidie kuwatoa watu wale, kwa sababu hakika kabisa ni watu ambao wameitumikia Taifa hili, ni watu ambao wametengeneza mambo mengi kwenye nchi hii na kwa kweli leo wananyanyasika kupitiliza wakifuatilia madai yao pasipokuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kundi hilo nashukuru leo tumepata taarifa nzuri hapa kwamba kuna shida kwenye mifuko, watumishi wanastaafu, wanakwenda kufuatilia pesa zao kwenye mifuko, inaonekana kuna miaka katikati hapa

mwajiri hajapeleka makato, eti analazimishwa mtumishi yule kwamba kwanza akafuatilie makato yake, halafu yaje yajaziwe pale kwenye maeneo ambayo alikuwa hajamaliza halafu ndio aweze kulipwa. Hii kweli jamani lazima tuitazame kwa kina inawatesa watumishi wengi, na hivi tufikirie ingekuwa inatugusa sisi Wabunge tungekuwaje? Hebu tunaomba tufanyie kazi, Waziri amezungumza hapa kwamba lazima watu wale walipwe na ukitazama ndio sheria inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limepitisha sheria hapa tarehe 20 Oktoba, 2017 ya kuunganisha mifuko, hiyo sheria inasema majukumu ya kufuatilia makato, majukumu ya kupeleka makato kwenye mifuko, ni jambo la mifuko yenye na waajiri watajuana wenyewe, huyu mtumishi anatakiwa akistaafu akachukue hela yake aendelee na shughuli yake. Leo anatakiwa afanye kazi ya kufuatilia makato yake...

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakamo, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wake mzuri, kwa ajili ya rekodi tu nilikuwa nampa taarifa kwamba ile sheria ambayo tulunganisha ya mifuko haikuwa mwaka 2017 ilikuwa mwaka 2018.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakamo unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa sababu ni suala zima la kurekebisha taarifa wanaorekebisha taarifa watakuwa wamekaa nayo vizuri. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya ambayo nimeyazungumza kwenye eneo hili, lipo jambo moja ambalo naomba nilieleze kuna hizi nafasi mbili ambazo wenzangu wamezizungumza vizuri, kuna hawa wanaitwa Watendaji wa Kata, kuna hawa wanaitwa Watendaji wa Vijiiji.

Mheshimiwa Waziri mimi nakufahamu, na najua uchapakazi wako, nikuombe sana ndugu yangu hebu kada hii tuiangalie ni kada ambayo wengi wakizungumza hapa hawaizungumzi, lakini ndio wenyewe kazi ya kusimamia miradi, ndio wanaokusanya mapato kule, lakini ukionza ofisi zao, ukiona maslahi yao wanayolipwa wao, unashangaa kabisa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Spika ambao niliwatangaza lakini walikuwa kwenye mkutano, sasa niwatangaze; hawa ni wageni wawili kutoka *Guaranty Trust Bank of Tanzania* ya Jiji Dar es Salaam, na hawa Ndugu Jubril Adeniji karibu sana na Mhandisi Mbaraka karibuni sana. Hawa walikuwa wageni wa Mheshimiwa Spika, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa tunaendelea na michango, Mheshimiwa Ally Kassinge atafuatiwa na Mheshimiwa Mtenga, Mheshimiwa Abdullah Mwinyi ajiandae.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nianze kwa kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Lakini kwa upkee nianze kutambua changamoto za watumishi hususani kundi la walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni sehemu ya watumishi katika nchi hii lakini kama tunawasikiliza vizuri inaweza ikawa ni miongoni mwa kundi lenye changamoto nyingi zaidi ikiwemo kama ambavyo Wabunge wengine wamechangia kucheleweshwa kupandishwa kwa madaraja ikiwemo mapunjo baada ya kustaafu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina *case study* mbili naomba nizitaje; katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, kuna mwalimu anaitwa Mwalimu Hadija Salum Bugurumo alistaafu mwaka 2020; alistaafu akiwa na Daraja F, mshahara aliolipwa ni wa Daraja E, na kwa maana hiyo anadai mapunjo. Pia kuna mwalimu anaitwa Mwalimu Salma Khamis Kaisi, naye kadhalika alistaafu mwaka 2020 lakini alipandishwa daraja tangu mwaka 2017 na amelipwa mafao yake ya kustaafu kwa mapunjo bado wanaidai Serikali mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa hawa ni walimu wangu ambao wamenifundisha mimi shule ya msingi Mnazi Mmoja, Kilwa Masoko na wamesema mwanangu, mwanangu katusaidie kutusemea huko na hapa nawasemea, Serikali iwasikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia, kama ambavyo Wabunge wengine wamechangia kumekuwa na changamoto kubwa sana ya kupewa gharama za kusafirisha mizigo baada ya kustaafu. Walimu wangu wawili hawa ambao nimewataja kwa mfano tu kwa niaba ya wengine walio wengi nao pia wanakumbwa na kadhai hii hawajalipwa mizigo ya kustaafu bado. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya eneo hilo, nzungumzie pia mazingira ya ufundishaji kwa walimu. Kada zingine hapa Tanzania kumekuwa na namna fulani fulani hivi ya kufikiriwa kimotisha motisha zipo kada ambazo wanalipwa kinachoitwa *ration allowance*, zipo kada wanalipwa *on call allowance* kwa maana ya kada ya sekta ya afya, ambayo hiyo *on call allowance* kwa sababu ya ule muda wa ziada mtumishi wa sekta ya afya anapoitwa kwa ajili ya kwenda kutoa huduma. Lakini walimu hawajafikiriwa, huko nyuma tulipata kuambiwa kwamba kulikuwa na kitu kinachoitwa

teaching allowance na hii ilizingatia mazingira ya walimu yalivyokuwa magumu katika kuandaa somo lenyewe, kufundisha na kufuatilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ualimu hauishii kufundisha tu darasani unaandaa *scheme of work* ya mwaka mzima kama si kwa muhula mzima, ukitoka hapo unaanda *lesson plan*, ukitoka hapo unaandaa *lesson notes*, ukitoka hapo unashahihisha kazi na kufuatilia mwafunzi mmoja baada ya mwininge, lakini pia *work load* ni kubwa. Mwalimu anatakiwa afundishwe wanafunzi 40 mpaka 45 kwa darasa moja. Walimu wetu hawa wanafundisha wanafunzi mpaka 200 kwa darasa moja hii ni *work load* kubwa wafikiriwe na wao kupata *teaching allowance* wapate motisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la watumishi nitumie lugha kwamba wametelekezwa, hawa walikuwa ni watumishi waandamizi wakapata nafasi za kuteuliwa na mamlaka zao, mamlaka zao za uteuzi baada ya kuwaacha katika nafasi hizo hawajarudishwa bado katika utumishi wa umma na ndio maana nimetumia lugha ya wametelekezwa. (*Makofi*)

Naomba Ofisi ya Rais Utumishi iwafikirie watumishi hawa kwa sababu na wao ni watumishi kama watumishi wengine na wana haki ya kufikiriwa, hawajapata *pension* zao, hawajapata maslahi yao yoyote, wamebaki kama walivyo kama wakiwa ndani ya nchi yao, hii sio sawa Ofisi ya Rais iwafikirie hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niseme kwamba wale watumishi ambao waliflikia nafasi za uteuzi kama vile Wakurugenzi, Ma-DAS na wengine na wakaingia katika mchakato wa uchaguzi, baadhi hawakutoka katika sekta nje ya utumishi wa umma tunafahamu ambao wametoka katika utumishi wa umma na bado wameendelea kutelekezwa miezi tisa kama wenzangu wamezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa nina *case study* moja ya mtumishi ambaye alikuwa Mtendaji wa Kata

Manispaa ya Kinondoni na baadae akawa *DAS* - Mbeya na baadae akaenda kugombea mpaka leo hajarudishwa katika utumishi wa umma. Tunaomba Serikali iwafikirie hawa ili tusiandae kundi kubwa la huko mbele ya safari ambao watakuwa ni wa kuipinga Serikali ambayo kwa kweli walihitumikia kwa uadilifu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Hassan Mtenga atafuatiwa Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ajandae.

Nadhani Mheshimiwa Hassan Mtenga atakuwa ameenda msikitini, Mheshimiwa Abdullah Mwinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo na Mheshimiwa Florent Kyombo ajiandae.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia hidaya hii nami kusema maneno machache, cha msingi ningependa kuzungumza kuhusu mambo mawili; mchango wangu hautakuwa *specific*, mchango wangu ningependa uwe *general*. Na mambo makuu mawili ningependa kuyazungumza la kwanza ni amani, la pili ni utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amani hii ambayo tunajivunia sisi na kuna baadhi ya wenzetu ambao wanatuhusudu na amani yetu haikuja kwa bahati mbaya, imelelewa, ikatunzwa na hatimaye ikastawi mpaka hapa hii leo tukawa tunajivunia. Mwanzilishi wetu Baba wa Taifa aliitunza na kuilea hii amani kwa msingi mmoja mkuu msingi huo ni msingi wa utaifa. Baba wa Taifa kwa kipindi kikubwa sana cha awamu yake ya kwanza, nguvu nyingi sana za kifikra, za kifedha, aliziwekeza katika kujenga utaifa (*national unit and cohesion*) na alijenga hivyo kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhakikisha Serikali Kuu; pili, Serikali za Mitaa na tatu, Taasisi na Asasi za Kiserikali

zina sura ya kiutaifa. Hili jambo kwa kweli hatuwezi kulichukulia wepesi wa aina yoyote, ni zito mno, tukilega hapo hii amani ambayo tunajivunia inaweza ikapeperuka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Askofu Bagonza anasema; amani ni tunda la haki, na haki hii aliyoitenda Baba wa Taifa kuhakikisha kwamba taasisi zote, Serikali yenyewe ipo na sura ya kiutaifa ndio zao lake hii amani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Waziri naomba nikukumbushe hili somo la kihistoria na sina shaka yoyote utorialichukua kwa umakini na katika uboreshaji wenu wa taasisi zote za ndani mtazingatia sura ya kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maana gani sura ya Kitaifa? Mheshimiwa baba wa Taifa alichukia ukabila, alichukia udini na alihakikisha taasisi za Kimuungano zina sura ya Kimuungano (*national cohesion*). Hili ni jambo la msingi sana hili amani idumu na itamalaki kama hivi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ningependa kuzungumzia suala la utawala bora. Tumejichagulia sisi kama nchi kuendesha nchi yetu kwa misingi ya kidemokrasia, Serikali ya watu, kwa ajili yao na inayowatumikia wao (*Government of the people, by the people, for the people*) huu ndio mfumo wetu. Sisi tulibahatiika kuwa viongozi tunadhamana hii ya muda mfupi tu na tupo hapa kwa ajili yao, tumejiwekea misingi ya utawala bora pasiwe na uonevu wa aina yoyote, tuwe tunalinda hii misingi iwalinde watu, hii misingi ilinde mali zao na misingi hii ilinde utu wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo basi ningependa kuona sheria ambazo zimetoka nje ya mlolongo huu, nje ya mfumo wa utawala bora ziletwe na tuzirekebishe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, imefika dakika saba?

NAIBU SPIKA: Tayari ahsante sana.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Londo karibu tutamalizia na Mheshimiwa Francis, halafu Mheshimiwa Naibu Waziri ujiandae.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kukushukuru kwa kitie chako kuniona walau niwe mionganoni mwa wachingiaji wa hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mimi naomba nichangie maeneo mawili; moja umuhimu wa dhamana ya utumishi katika Serikali yetu, lakini la pili nakisi ya imani ya wananchi wetu katika utumishi wa umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunapozungumzia utumishi ni dhana ambayo inahitaji tafsiri mpya na hasa ukizingatia katika Taifa ambalo sekta binafsi imeajiri watu wengi ambao wanautumikia umma kiasi ambacho tafsiri ya utumishi umma inakosa maana ama inayumba yumba hapa katikati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta watu wengi katika sekta binafsi wanatumikia umma kuliko watumishi wenyewe, utakuta watu wanapata shida katika ofisi ya umma kiasi ambacho wanapata huduma bora zaidi ambazo zilikuwa zinapaswa kubebwa na ofisi ya umma katika taasisi binafsi. Na ndio maana mfumuko huu wa mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yanahudumia watu yamechukua sana majukumu ya watumishi wetu Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba watu ambao wanaomba ajira Serikalini na wale ambao

watumishi walipoko Serikalini wajue dhamana waliyonayo, kwamba wao ndio kioo cha Serikali wanapoenda kuhudumia watu wao ndi Serikali, mwananchi anapofika katika ofisi ya umma kwenda kuomba ama kusiliza shida yake yule ndio Serikali, na dhamana hii ni ya muda ni lazima watumishi wetu wafahamu kwamba hatma ya nchi yetu ipo mikononi mwa mtumishi wa umma. Lakini watumishi hawa wanahitaji pia maandalizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya USEMI ya Utawala na Serikali za Mitaa kilio kikubwa cha Chuo cha Utumishi pale Magogoni ni kwamba hawana wanafunzi wa kutosha ambao ni watumishi wa Serikali. Wanafunzi wengi ambao wanasoma katika chuo hiki wanalipiwa na wazazi na wengine wanatoka majumbani. Tunapoteza lengo la msingi la chuo hiki kuwanoa na kuwafundisha watumishi wa Serikali hili kuboresha utumishi wao kwa umma wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ambalo nilikuwa naomba kuchangia ni dhana ya uzalendo; kwa wenzetu kazi za kujitolea ndio msingi wa uzalendo katika Taifa lao. Sisi hapa pia tuna vijana wengi ambao wanajitolea kwenye sekta mbalimbali hasa elimu, lakini vijana hawa ajira inapotoka miongozo ya utumishi haiwatambui. Sasa ni wakati, wakati tunaboresha teknolojia, watu sasa hivi wana *apply* kazi kwa mitandao tuwe na vigezo vya kuangalia vijana ambao wanajitolea katika mazingira mbalimbali na kujitolea kuwe sehemu ya mahitaji ama sehemu ya masharti ya watu ambao wanaweza wakapata *added advantage* pale wanapoomba kazi Serikalini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wana malalamiko mengi hasa watumishi wa umma, kuna wengi ambao walismamishwa kinyume cha sheria wakati ule wa mjadala wa yeti *fake* na wafanyakazi hewa na baadae wakarejeshwa kwenye ajira zao. Lakini naomba kuchukua nafasi hii kuwasikitika mpaka sasa wengine hawajalipwa malimbikizo yao na wengine waliachishwa kazi barua zimetoka za kuwarudisha kazini, hawarejeshwa kazini mpaka

sasa hivi. Nilikuwa naomba kutumia nafasi hii kutoa rai kwa ndugu zetu wa Utumishi, kuona ni jinsi gani wanaenda kuhakikisha kwamba wale watumishi ambao waliondolewa kimakosa basi wahakikishe kwamba malimbikizo yao ya mishahara yanaenda kurejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linazungumzia suala malimbikizo ya mshahara ni watumishi wale wahanga 2,000 wa Ilovo. Wakati tunabinafsisha mashirika ya umma, kuna Watanzania wengi waliachishwa kazi na malimbikizo yao mpaka leo hawajalipwa na wengine walilipwa pungufu na hawajui mahali pakwenda kulalamika PSRC wanasema watalipwa na mwajiri, mwajiri anasema watalipwa na Hazina. Kwa hiyo watu hawa bado wana kilio kikubwa naomba sana Wizara ya Utumishi iwaangalie hasa hawa wahanga 2,000 kule Ilovo ambao mpaka sasa hivi wana kesi mahakamani lakini kuna wengine ambao hawana kesi mahakamani wanaagaikia malipo yao.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora ajiandae.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi, niungane na wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Deo Ndejemb, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais.

Naomba niongee machache kwa sababu ya muda, lakini pia niwaombe Mheshimiwa Waziri na Naibu wake

naona ni vijana ambao wana kesho nyingi njema na hivyo wakichukua fursa hii ya kupata ushauri na kuiboresha Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora basi tutakuwa na watumishi wenyewe hali ya kazi na hivyo malengo mahususi ya nchi yetu yataweza kufikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua nitatoa *case study* katika *local government* na najua mwongozo ambao unasimamia maadili ya utumishi wa umma ni Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 yaani *Standing Order of 2009*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujikita kwenye fursa sawa kwa watumishi wote. Halmashauri inazo Idara 18 baada ya moja ambayo ilikuwa Idara ya Maji kutolewa na kuanzishwa Taasisi ya RUWASA. Lakini katika maeneo hayo watumishi wote hawahudumiwi sawa na kanuni za utumishi wa umma. tunaona katika *OC* inayopelekwa katika Halmashauri hizo suala la *leave*, suala la likizo zime-concentrate katika baadhi ya idara na idara hizo ni Idara ya Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Afya na huko hazitoshii lakini idara zote zilizobaki hakuna mtumishi anayeweza kukuambia kwamba nilishawahi kulipwa hela ya likizo, hakuna mtumishi anayeweza kukuambia kwamba nilishawahi kulipwa hela ya kusafirisha mizigo kurudi kwetu kutoka kwenye *OC*. Na idara hizo nyingine *OC* inaenda shilingi milioni moja Idara ya Kilimo, Idara ya Mifugo, Idara ya Mazingira, Idara ya Mipango. Niombe Wizara iangalie kwa sababu yeye ndio baba, mama wa watumishi wote na *Standing Orders*sasa ya mwaka 2009 iweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la *OPRAS*, mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais jana ni kama alifungua kifua changu na kunifanya nipumue vizuri baada ya kuiona pia *OPRAS*ni tathmini ya utendaji kazi ya watumishi kwamba haiko vizuri inatakiwa iboreshwa. Najua kutakuwa na *forum* mahususi kwa ajili ya kuchangia vizuri, lakini niombe kushauri tunazo taasisi za Serikali, mimi nishawahi kuwa mtumishi wa *TFDA* leo ni *TMDA* ili boresha ile *OPRAS* tukaingia kwenye *TASA - TFDA Staff Appraisal* ambayo ilikuwa kwa kweli

inatumika hata kumpata mfanyakazi bora wa Mei Mosi anapatikana kupitia hiyo. Lakini leo *OPRA*Shai po na Mei Mosi mtumishi bora anapatikana kwa zamu, kwamba tupeane zamu, sijui ni nani maaarufu zaidi naomba kwa hiyo niombe sana iweze kuboreshwa kama Mheshimiwa Rais alivyoshauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nilitaka kushauri kwenye suala la uhamisho. Tumekuwa na utaratibu wa kuhamisha watumishi na tumepewa maelekezo kwamba watumishi wahame kadri inavyowezekana, lakini niombe *chain of command*, *chain* ya mawasiliano ya viongozi wetu izingatiwe, yule ambaye tumemkasimu kusimamia watumishi katika eneo lake basi *m-consult* hata kidogo, leo unakuta Halmashauri imetumia fedha kumuhamisha mwalimu kwa gharama wa sayansi, amefika hapo barua inatoka Utumishi au inatoka TAMISEMI bila taarifa Mkurugenzi kujua. Tunaiweka Serikali katika gharama kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe *chain of command* mamlaka haipingwi, lakini wasiliana na wale wanaokusaidia kusimamia watumishi kule chini. mtaongea lugha moja na tunajua kwamba kila mtumishi atapata haki yake ya kuhama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho niungane na hoja ya Mheshimiwa Husna Sekiboko na Mheshimiwa Ndulane, ni watumishi ambao walikuwa watumishi wakaenda kugombea katika nafasi za siasa. Katika eneo hili lilikuwa na ukakasi na *grievance* nyingi sana, mimi niwaombe Wizara hii ilifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *post* nyingine ni *political post* akimaliza anapewa *gratuityyake*, anafungasha, anaondoka, lakini *post* nyingine kama walivyosema za Wakurugenzi na watumishi wengine zilikuwa ni za kiutumishi, wamepewa ajira, wamethibitisa kazini na walipoondoka walitakiwa sasa wapangiwe vituo vingine na hii tumeiona, hata kipindi cha nyuma wapo Ma-RAS ambao walitolewa kazini, wapo Wakurugenzi walitolewa kazini, lakini

walipangiwa *RS*, wapo wanafanya kazi na taasisi nyingine za Serikali wengine wameletwa katika Wizara zenu. Kwa hiyo, tuombe hao wenzetu ambao wapo mtaani, wanazurura hawajui la kufanya, niombe sasa Wizara ifanyie kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimeshalitolea Mwongozo jambo hilo tukikaa hapa tunawazungumzia watu ambao hatuna taarifa zao mahsus, hata mimi kama mwongoza kikao inanipa wakati mgumu sana, kwa sababu mtu akitaka akaajiriwe maana yake yeye ndio ajira yake hiyo pengine ya kwanza. Wapo watu ambao wameteuliwa kutoka sehemu mbalimbali yaani kwa mfano niseme kuna Wakili mahali ameteuliwa kuwa Mkurugenzi mahali hajawahi kuajiriwa, alikuwa kwenye *law firm* yake huko akateuliwa kuwa Mkurugenzi, baada ya kuwa Mkurugenzi akaamua agombee nafasi ya kisasa, kwenda kugombea imeshindikana, unataka Serikali imuajiri kwa ngazi ipi sasa? Kwa sababu hajawahi kuajiriwa, aliteuliwa kutokea kwenye *law firm* yake kwenda kuwa Mkurugenzi. Mifano kama ipo ambayo hawa walikuwa watumishi nimeshalitolea Mwongozo; ipelekeni Serikalini waweze kuifanyia kazi. Kwa sababu mkileta hapa hatuna taarifa, mimi mwenyewe sina hizo taarifa za *DAS* yupi aliondolewa wapi na alikuwa nani kabla hajawa *DAS*, sina.

Kwa hiyo, hata wao hapa tukisema tunataka atakapokuja ku-*wind up* aseme hili na hili, nadhani kwa sababu tumeshalitolea mwongozo, pelekeni hiyo orodha na hao watu walikuwa akina nani kabla ya kwenda kugombea. Maana tuisijekuwa tunailazimisha Serikali kuajiri watu kwa sababu tu walipata fursa ya kuteuliwa, hapana, tutakuwa hatutoi ushauri ulio sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda sasa kwa Mheshimiwa George Malima, atafuatia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora na tutamalizia na mtoa

hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. (*Makofii*)

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa sababu ya kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nataka niwapongeze sana kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia katika Taasisi ya TAKUKURU. Taasisi hii inafanya kazi nzuri kwa ajili ya kupambana na rushwa na mambo ya ujisadi katika nchi yetu. Lakini katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri alikuwa amesema Taasisi moja ya *Transparency International* ilitupa alama ya 38; hii ni ishara kwamba bado tuna kazi kubwa ya kufanya kwa ajili ya kupambana na vitendo hihi vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ninapenda kutoa ushauri kwa Serikali, TAKUKURU ijkite sana kwenye utafiti, tuangalie sana vyanzo vya rushwa viko maeneo gani na kusema kweli maeneo mengi ambayo yana shida ya rushwa ni yale ambayo yanatoa huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, tufanye utafiti wa kutosha, tujue na kubaini maeneo ambayo yana mianya ya rushwa ili kabla ya kuanza kukimbizana na mla rushwa mmoja mmoja tupambane kwanza na kuziba hiyo mianya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wale wananchi wenyewe uzalendo ambao wanatoa taarifa sahihi zinazosaidia kupambana na vitendo vya rushwa. Najua taarifa hizi zinatolewa katika mazingira ya usiri mkubwa. Lakini ninashauri wawe *motivated* katika mazingira hayo hayo ya usiri ili waendelee kusaidia katika kupambana na vita ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kuhusu *TASAF* - Mpango wa Kusaidia Kaya Maskini. Mpango huu pia umeendelea vizuri na hasa kule jimboni kwangu vijiji vingi vimepata mpango huu. Lakini naomba sana katika

Jimbo la Mpwapwa bado kuna vijiji 22 havijaingia katika huu Mpango wa Kusaidia Kaya Maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitoe ushauri, bado kuna malalamiko madogo madogo kwamba utaratibu mzima wa kutambua kaya maskini bado una kasoro ndogo ndogo. Wale walengwa wanaotakiwa kufaidika na mpango huu hawatambuliwi, matokeo yake unakuta kaya ambayo inapata huduma hii haina sifa ya kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo maana yake kuna wimbo la rushwa hapo limegubika, maana sioni mantiki ya mtu kwenda kuona kwa sababu utaratibu ni kwamba lazima maafisa wafike wakaone kaya ile ina hali gani ya kiuchumi. Sasa kama umekuta ina unafuu wa kiuchumi kwa nini uiandike katika orodha ya kaya maskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hilo ni jambo ambalo tunaomba Wizara iendelee kupambana nalo. Tunapenda sana watu wetu wale ambaao kwa kweli wanahitaji msaada huu basi wanufaikie na msaada huu, badala ya kunufaika watu wasiohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze juu ya uongozi; katika bajeti ya TAMISEMI, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walichangia juu ya migogoro inayoendelea katika maeneo yetu. Unakuta *DED* hapatani na Mkuu wa Wilaya, hapatani na mwenyekiti wa Halmashauri. Mimi nafikiri haya yote yanatokana na ukweli kwamba wanapoteuliwa hawapewi semina ili wajue wajibu wao. Matokeo yake mtu ana-overlap mpaka kwenye kazi ya mtu mwingine halafu kunakuwa hakuna maelewano ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ule utaratibu wa semina elekezi mimi naomba urudishwe ili watu wakipata uteuzi au wakiajiriwa kwenye nafasi fulani basi apewe maelekezo namna ya kuenenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deogratius Ndejembia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake nyingi ambazo anaendelea kutujalia sisi waja wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwa sababu ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza tangu Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, afanye mabadiliko katika Baraza la Mawaziri na kunibakisha mimi katika nafasi yangu nikiwa nahudumu katika ofisi yake, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana na kumuahidi sitomuangusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru sana wanajimbo wa Jimbo langu la Chamwino ambaao wameendelea kuwa na imani nami na tumeendelea kuwa wote pamoja katika kutatua changamoto mbalimbali za Wanachamwino. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini siyo kwa umuhimu, naomba niwashukuru Wabunge wote 19 ambaao wamechangia katika hotuba yetu iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hapa ya bajeti yetu ya Ofisi yetu ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja mbalimbali ambazo zimeletwa na Wabunge hapa tumezipokea na nyingi ni hoja ambazo zimejikita katika kuboresha maslahi ya watumishi wetu wa umma ambaao ndio *engine* ya Serikali yetu, watumishi wa umma ndio ambaao wanatoa huduma kwa wananchi wetu ambaao wengi wao ni maskini katika Taifa letu hili la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutambua hilo, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 imeboresha

maslahi ya watumishi wa Serikali kwa kulipa malimbikizo ya madeni ya mishahara kwa watumishi zaidi ya 34,676 ambayo yana jumla ya thamani ya shilingi 69,077,261,014 katika mwaka wa fedha huu 2020/2021. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako kwamba madeni ya *arrears* za mishahara yapo ambayo yalifanyiwa uhakiki na yamelipwa mwezi Novemba, 2020 na kuna madeni vilevile ya *arrears* ambayo yalifanyiwa uhakiki na yamelipwa mwezi uliopita, mwezi Machi, 2021na hivi tunavyozungumza kuna madeni mengine ambayo tayari yanafanyiwa uchambuzi na uhakiki na yatakwenda kulipwa muda si mrefu tayari yakimaliza uhakiki katika Ofisi ya Utumishi na kupelekwa kwa wenzetu kule Hazina yataweza kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna hoja ambazo zimeletwa hapa na Waheshimiwa Wabunge ya kuzungumzia masuala ya *OPRAS* ambayo ni *Open Performance Appraisal System* ambayo ipo kwa watumishi wa umma. Huu ni mkataba wa ufanyaji kazi baina ya mtumishi na mwajiri wake. Sasa hapa kumekuwa kuna changamoto kidogo, na kama mlivyomsikia Mheshimiwa Rais jana, naye alilizungumzia. Changamoto ni kwamba watumishi wetu wengi wamekuwa wakifanya udanganyifu katika mfumo huu. Kwa maana taarifa za mwaka juzi, mwaka jana, ndizo hizo hizo ata-copy na ku-paste na kubadili tu tarehe bila hata ya kujipima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukimuuliza mtumishi huyu kwamba hivi wewe kuanzia Januari mwaka jana mpaka Januari, 2021, kuna kipi ulichochangia katika eneo lako la kazi cha kuweza kuleta matokeo chanya ambayo ni faida kwa wananchi wetu wa Tanzania? Ukiuliza swali hilo unaweza ukakuta majibu hayaeleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunakwenda kubadili mfumo huu na kuweka utaratibu ambao utakuwa ni rahisi sana kwa mtumishi tangu anaingia katika utumishi wa umma na anapoendelea katika ukuaji wake wa utumishi, basi tuweze ku-evaluate performance yake kwa njia rahisi zaidi

kwa maana *immediate supervisor* awe ana uwezo wa kuweka *comment*, lakini vilevile mwajiri mkuu awe ana uwezo wa kuweka *comment* katika *performance* ya mtumishi huyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhakikisha ya kwamba hakuna udanganyifu. Kuwe kuna utaratibu wa kuwa na *work plan* ambayo itatoholewa kutoka kwenye *strategic plan* ya taasisi yenye we ili tuweze kujua huyu mtendaji ametusaidia vipi kuweza kufikia malengo yaliyowekwa na taasisi husika, ndipo tutaweza kujua pia kwamba hawa watumishi, je, anastahili kupanda daraja, je, anastahili kupanda mshahara, je, kile anacholipwa na Serikali ni sahihi au amepunjwa au anatakiwa kuongezwa kwa sababu ya tija ya kazi yake anayoifanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tunakwenda kulifanya kazi na kuhakikisha kwamba *OPRAS* hii inabadilika na kuwa yenye tija katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi pia wamezungumzia suala la kuwawezesha watumishi wetu kwa kuwafanya *training* mbalimbali na kuwapa mafunzo kuweza kujua kazi zao ziko vipi na mafunzo mengine ambayo ni ya *on the job training*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili tumegundua kwamba kuna changamoto moja; tuna Chuo cha Utumishi wa Umma, lakini chuo hiki waajiri wengi wamekuwa hawatengi mafungu au fedha za kuweza kupeleka watumishi wao kuweza kufanyiwa mafunzo ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtu ametoka chuo fulani lakini akiingia kwenye utumishi wa umma lazima afunzwe apewe *etiquette* za utumishi wa umma na aweze kuendana nao katika miaka yake yote ya utumishi. Hili ninaamini muda si mrefu Waheshimiwa Wabunge mtaona mabadiliko makubwa sana kwenye hili. Tunataka kuwe na *uniformity* katika utumishi wa umma, kwamba watu wanavyo-behave akiwa mtaani na akiwa kazini, basi mtu akimuangalia

aweze kufahamu kwamba huyu ni mtumishi wa umma.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia suala zima la Uwezeshaji wa Kaya Maskini (*TASAF*). Mpango huu kiukweli umesadnia watu wengi, kaya nyingi ambazo hazikuwa na uhakika wa mlo hata mmoja katika kaya zao, lakini leo hii zimekuwa zina uhakika wa milo mitatu na kaya nyingine zimekwenda hata kuboresha maisha ya kuwa na biashara, kuwa na mifugo, kulima kilimo kilicho bora na kadhalika. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwahakikishie Wabunge, kaya zilizokuwepo kwenye *TASAF III, Phase One* zilikuwa ni kaya milioni moja Tanzania nzima. Sasa tunakwenda kuwa na kaya 1,400,000 katika nchi nzima, ambapo vijiji viliyvoachwa mpaka ifikapo mwezi Julai, 2021, vijiji vyote katika nchi yetu vitakuwa vinapokea *TASAF*. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika suala hili ninaomba sana ushirikishwaji wa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, mshiriki sana katika kutoa elimu kwa wnanachi wetu kwamba *TASAF* si jambo endelevu, *TASAF* imekuja kwa sababu ya kukuwezesha wewe kukutoa katika hali moja na kukuweka katika hali nyingine ya maisha yako. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumekuwa na upotoshwaji unaendelea, wanaelezana watu huko kwamba ukiboresha maisha yako watakutoa kwenye Mpango wa *TASAF*. Lengo la *TASAF* ndio wakutoe, lakini ukiwa umeboresha maisha yako. Kama walikukuta huna mbuzi basi uwe una mbuzi watano, una kuku kumi, una bata ishirini na una nyumba bora, ndilo lengo la Mpango wa *TASAF*. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwisho wa siku ukibaki kwenye mpango huu kwa muda mrefu, siku mpango huu unapokuja kuisha tutakuwa tumetengeneza tatizo kubwa zaidi badala ya mpango huu ulipofika. Mpango huu lazima Waheshimiwa Wabunge twende majimboni mwetu tutoe

elimu kwamba umekuja kuwasaidia kuboresha maisha yao na siyo kuwa tegemezi wa mpango huu katika maisha yao yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa Malima, ametoka kumalizia hapa na amezungumzia utaratibu wa kupata kaya hizi maskini. Nilifahamishe Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu ni kwamba unakwenda kwenye mukutano wa kijiji na mukutano wa kijiji ndiyo unatambua kaya zile maskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto imekuwa kwamba katika wale wananchi wa eneo husika kuna watu ambao wana *status* fulani katika kijiji. Wale watu wanaogopeka na wanawekwa kwenye mpango na wakiwa kwenye mpango watu wanaogopa kusema kwa kuogopa akisema anaweza akachukuliwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine nyingi tumezichukua na Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Mchengerwa naye atazizungumzia. Lakini nyingi tulizozichukua tutazitafutia majibu na kuzijibu kwa maandishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimuite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, uje uhitimishe hoja yako.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwiningi wa rehema, kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kufikia mwisho wa mjadala wetu wa bajeti yetu hii wa ofisi yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo aliyojatoa siku ya jana kuhusu masuala yanayohusu ofisi yangu wakati akililutubia Bunge lako Tukufu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa maelekezo yake tumeyapokea, tumeyaelewa, tutayazingatia na kuyafanya kazi kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia uniruhusu niwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kuunga mkono hoja niliyowasilisha jana katika Bunge lako Tukufu. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuweza kuchangia kwa sababu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha hoja, naomba kusisitiza kuwa ofisi yangu na taasisi zote zilizo chini yangu tumejipanga vizuri kutekeleza yale yote tunayoyapanga kuyafanya kazi mwaka ujao wa fedha ili kuiwezesha Serikali kufikia malengo yake ya kukuza uchumi na ustawi wa Watanzania. Ninatambua umuhimu wa mchango wenu katika jitihada za kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, lakini pia maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyonadiwa katika uchaguzi uliopita, lakini pia Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026) na Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa siku ya jana katika Bunge lako hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vita dhidi ya rushwa, tumeendelea kujidhatiti na kukabiliana na vitendo vya rushwa nchini, hali ambayo imeongeza nidhamu, uadilifu na matumizi bora ya madaraka na fedha za umma. Mafanikio ya juhudhi zetu yamedhihirishwa na taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Kazi iliyombele yetu ni kuhifadhi mafanikio hayo na kuongeza juhudhi ili kutokomeza rushwa na ujisadi nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo hayo tumejipanga vyema kuandaa na kutekeleza mkakati mpya wa mapambano dhidi ya rushwa hapa nchini utakaozingatia changamoto zinazojitokeza sasa. Vilevile tunakusudia kuongeza ufahamu kwa wnanachi kuhusu masuala ya rushwa, kuboresha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa na kuimarisha utendaji wa Taasisi yetu hii ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wanyonge, ofisi yangu itaendelea kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa MKURABITA ili manufaa yake yawafikie wananchi wengi zaidi. Wakati huo huo, tutaendelea kusimamia maadili na mwenendo wa watumishi wa umma, uwe ni mwema na uendane na miongozo mbalimbali ya watumishi wa umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, tutaendelea kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuboresha na kuimarisha usalama wa mifumo ya Serikali ili iweze kubadilisha taarifa tunazopata. Matumaini yetu ni kuwa hatua hii itaongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi yangu itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa kubuni sera, kanuni, na sheria za uendeshaji wa shughuli za utumishi wa umma na kuwajengea uwezo watumishi waweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo tutaendelea kulinda haki za watumishi wa umma kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Aidha, tutahakikisha kuwa ngazi za mishahara na madaraja ya watumishi yanapandishwa kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais siku ya jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda kuona watumishi wanalipwa stahiki zao kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo. Stahiki za mtumishi ni haki yake mtumishi husika

na siyo huruma, ni *right*, siyo *privilege* kama ambavyo nimikuwa nikisisitiza mara kwa mara. Tunataka kuondoa kero za kimaslahi zinazowakabili watumishi wa umma na uonevu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nitaweka utaratibu wa kupokea malalamiko ya watumishi na nitachukua hatua kali za kinidhamu kwa wale wote watakaoshindwa kuwahudumia watumishi na wananchi kwa ujumla. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi yangu itaendelea kuratibu, kusimamia, na kukuza jithada za Serikali, Serikali mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na viwango vya miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi zote za umma hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutoa maoni yao na pengine lazima nikiri kwamba maoni tumeyapokea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja chache ambazo pengine ningependa kuzitolea ufanuzi. Kuna hoja hii ambayo imezungumzwa sana kuhusu Idadi ya Wakurugenzi saba, Ma-DAS pamoja na Ma-RAS ambao walikwenda kwenye kugombea kwenye nafasi mbalimbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii kama Wizara tumeipokea. Kama ambavyo nimesema Rais wetu amejikita katika kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa kila Mtanzania.

Kwa hiyo tutalichukua jambo hili tutakwenda kulifanya kazi kama kutakuwa na mtumishi ambaye pengine alikuwa Mkurugenzi, alikuwa *RAS* au alikuwa *DAS* na alikwenda kugombea na kama alifuata taratibu zote ambazo zinatakiwa za kisheria na kikanuni zilizowekwa basi mtumishi yule kama haki yake itamtaka arejeshwe kazini, atarejeshwa kazini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kwa sababu tunatambua kwamba wapo watumishi ambao tayari walirejeshwa kazini na jukumu la Serikali hii kuhakikisha kwamba inafanya kazi zake kuondosha *double standard*, kwa hiyo tutalichukua jambo hili, tutakwenda kulifanyia kazi kwa wale watumishi ambao wana haki ya kurejeshwa kazini watarejeshwa kazini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe na kama kuna Mbunge ye yeyote Mheshimiwa Mbunge ye yeyote anataarifa au watumishi hawa wapo basi wafike ofisini kwangu ili tuweze kuititia taarifa zao na yule mweye haki ya kurejeshwa kazini atarejeshwa kazini. Kwa sababu huu ndiyo msimamo wa Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba inatenda haki kwa wakati ili kila mmoja wetu aweze kupata haki zake stahiki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu suala hili la upandishwaji wa madaraja limezungumzwa kwa kina sana. Naomba niseme kwamba tumeziagiza Taasisi na Maafisa Utumishi wote nchini kuhakikisha kwamba wanatuletea taarifa za watumishi wote katika maeneo yao. Tayari wizara yangu imekwishatenga nafasi za upandishwaji wa madaraja. Kwa sasa tunao watumishi zaidi ya 91,841 ambao wataigharimu Serikali zaidi ya shillingi 73,402,166.926. Kwa hiyo, tumejipanga kuhakikisha kwamba tunawapandisha madaraja watumishi kwa mikakati ambayo tumejiwekea sisi wenyewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu hili suala la ajira mpya tayari Wizara yangu imejipanga kuhakikisha kwamba tutatoa ajira mpya 40,737 ambazo zitawagawinyika katika kada mbalimbali za utumishi wa umma. Tunazo ajira za elimu ambazo tunategemea kuzingataza hivi karibuni, ajira 9,667 na katika sekta ya afya tunategemea kutangaza ajira 10,467 na hivi karibuni tutatangaza ajira 2,116 za afya tukisubiri taarifa ya bajeti ambayo tutatangaza ajira zitakazopungua kutokana na hizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika sekta ya kilimo tutatangaza ajira 1,046 kulingana na bajeti tutakayoipata. Katika sekta ya mifugo ajira 758, katika uvuvi 175, katika polisi 1,346 na katika magereza ni ajira 427. Jeshi la Zimamoto ni ajira 510, uhamiaji ajira 404, hospitali na mashirika ya kidini na hiari 1,486 na ajira nyinginezo ni 13,192. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwatulize Waheshimiwa Wabunge watambue kwamba Serikali yao ya Awamu ya Sita imejipanga kuhakikisha kwamba tunakwenda kupunguza maeneo ambayo tunajua yanachangomoto nyingi za ajira katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mahusiano kati ya Ma-RC, Ma-DC, na Ma-DAS hili nimelizungumza kwa kina kabisa. Ni vyema kila mtumishi wa umma akatambua kwamba mtumishi yeote wa umma hapa nchini yupo chini ya Wizara ya Ofisi yetu. Wizara hii ambayo inasimamia nidhamu za watumishi wote wa umma, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe Ma-RC, Ma-DC na Naibu Wakurugenzi na wale wote wanaoangukia kwenye Wizara hii kujikita katika kuhakikisha kwamba wanalinda viapo vyao ambavyo wamekula mbele ya Mheshimiwa Rais. Lakini pia nichukue fursa hii kuwataka viongozi wote wa Chuo cha Uongozi kujipanga vyema katika kuhakikisha kwamba wanatoa semina kwa viongozi wote wa umma ambao wanaangukia katika nafasi ya Naibu Wakurugenzi, Wakurugenzi, Ma-RC, Ma-DC na viongozi wengine wote wa umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili suala la utolewaji wa nyaraka, suala hili nimelizungumza kwa kina. Ofisi yangu itakwenda kujipanga, tutakwenda kupertia nyaraka zote, zile nyaraka ambazo tunaona zimetolewa na zinakiuka sheria nyaraka hizo zote hizo tutazifuta. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, lakini naamini kwa kipindi ambacho

nimekaa katika ofisi hii binafsi sijaona nyaraka ambayo imetolewa imekiuka sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama kuna taarifa ya nyaraka yoyote ambayo imetolewa na inakiuka sheria tutakwenda kujipanga na kuhakikisha kwamba nyaraka hiyo tunaiondosha na kuifuta ili sasa kwa namna ile ile ya misingi ya tasfiri ya sheria tunakuwa na Katiba, tuna sheria, tuna kanuni pamoja na miongozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafuu ya muda ninaomba sasa pamoja na michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge iliyotolewa ninaomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofi*)

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na taratibu zetu na watu wanaweza kuwa wanaona saa saba kamili imeshafika kwa mujibu wa Kanuni ya 34(2) ambayo haiitaji niwahoji tutamalizia shughuli zilizopo mbele yetu.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Kamati ya Matumizi.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 32 - OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UΤΑΛΑΒΑ ΒΟΡΑ

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*.....Sh.12,505,350,800

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenyε mshahara wa Waziri na hapa nimeletewa majina ya Wabunge ambao wanahitaji ufanuzi kwenye sehemu hii. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na maelezo mazuri na ufanuzi na hitimisho la Mheshimiwa Waziri, lakini pia kwa kuzingatia hotuba nzuri, hotuba bora na hotuba ya matumaini aliyoitao Mheshimiwa Rais siku ya jana, ambayo kiukweli imewafanya watanzania na hasa watumishi wa umma jana wamelala wakiwa na raha na wakiwa na matumaini makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba jambo hili la nyongeza la mishahara kwa watumishi wa umma wanachukua na kwenda kulifanyika kazi. Sina mashaka sana na uwezo wa Mheshimiwa Waziri, lakini kwa kuwa jambo limekuwa ni la muda mrefu, nataka kupata kauli ya Serikali, ni lini jambo hili linakwenda kufanyika ili kuangalia maslahi ya watumishi wa umma kwenye nchi yetu? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, mtoha hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UΤΑΛΑΒΑ ΒΟΡΑ: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kabisa kwamba Serikali Awamu ya Sita imejipanga kusikiliza haki za watumishi wa umma na baada ya Mheshimiwa Rais siku ya jana kutoa hotuba yake yenye matumaini kwa watumishi wa umma ninaimani kubwa sana kwamba jambo hili litakwenda kufanyiwa kazi na Serikali na

niwatie moyo watumishi wa umma kwamba Serikali yao ya Awamu ya Sita imejipanga kuhakikisha kwamba tunalinda na kutetea maslahi ya watumishi wa umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hili kama ambavyo Mheshimiwa Rais amelizungumza kwa ufasaha ninadhani kabisa kwamba hakuna Mtanzania mwingine mwenye uwezo wa kulizungumza kwa ufasaha zaidi kama ambavyo Mheshimiwa Rais amelisema siku ya jana. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati jambo hili linafanyiwa kazi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnzava naona umesimama.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri niseme tu kama alivyosema Mheshimiwa Rais jana kwamba watumishi tunapowapa wajibu wa kufanya kazi pia wanastahili kupata haki yao, wajibu unaendana na haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa tunayo matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Rais, kwa kuwa tuna matumaini makubwa sanana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na hakika jambo hili litakwenda kufanyika tunaomba mkalishughuhulikie ili tuwasaidie watumishi ndani ya nchi yetu. Nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa swali lilikuwa limeuliza lini, nadhani nidhahiri Mheshimiwa Rais kwa namna alivyositisiza jambo hili jana na Mheshimiwa Waziri katika majibu yake hapa nadhani tuwape muda. Sasa hivi ndiyo tunapitisha bajeti ili waende mengine wakayafanye sasa hivi, mengine watakuwa wanaenda nayo. Lakini la muhimu ni kwamba hilo jambo lifanyiwe kazi kwa haraka ndiyo la muhimu.

Mheshimiwa Janejelly Ntate.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na bajeti nzuri, lakini mimi napenda kujua kwa kuwa Sera ya Utumishi wa Umma inataka uwepo utawala bora kwa Wakuu wa Idara, Ma-DC na Ma-RC kuwatendea kwa heshima watumishi wanaowaongoza, mfano wanapokuwa wamekosea. Kwa mfano kuwaweka ndani, kuwakaripia mbele ya wale wengine wanaowaongoza. Ni nini tamko la Serikali kuhusu suala hili? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo; ni kwamba watumishi wote wa umma iwe kwenye ngazi za teuzi, iwe kwenye kazi za idara na kadhalika ni lazima wazingatie utawala bora kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni na miongozo mbalimbali iliyokuwepo katika utumishi wa umma na wakifuata hivyo wakati wote tunaamini kwamba migongano kazini haitokuwepo. Kwa hiyo, tuwaase wote huko waliokuwa *field* kwamba wafuate sheria, taratibu, kanuni na miongozo waliyonayo kwenye kazi zao na waheshimiane na bila kuvuka mipaka ya kazi yao tunaamini mambo yote yatakuwa sawa. Nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janejelly naona ameelewa, lakini tamko hilo ni la msingi sana sana, kwa sababu viongozi wanapodhalilishana linakuwa sio jambo jema. Halafu wanadhalilishana mbele ya wale wanaowaongoza wote halafu kesho unataka wamskilize huyu uliyemdhaliishaa. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ni jambo jema kabisa kwa hilo tamko lilitotoka lakini tuombe linapotokea basi mtafute namna ya kushughulika nalo ili lisitokee tena sehemu nyingine. Kama ni hapa Bungeni mnasema, semeni hapa hapa ili mtu ajue kwamba kule kesi yangu walau imeisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Agnesta Lambert.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na maelezo au ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri lakini nikiri kwamba sijaridhika kwa upande wa waraka ambao niliongelea pale awali katika mchango wangu.

Mheshimiwa Waziri amesema kwamba watakwenda kupekua pekua ili kuona kama kuna hizo nyaraka ambazo zimeshushwa huko chini ambazo kimsingi zinahatarisha au zinaminya kabisa zile haki za watumishi wa umma na zinakinzana moja kwa moja na sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama tunavyofahamu hakuna Waraka wowote unaopaswa kuwa juu ya sheria. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri aje moja moja na *commitment* ya Serikali kwa sababu waraka upo, upo unatumika na inatumika.

Sasa Waziri aje na *commitment* ya moja kwa moja kwamba baada ya kutoka hapa na kwa kuwa namwambia kwamba huo waraka upo basi aende moja moja aje na *commitment* ya kwamba anakwenda kufuta huo waraka. Na Mheshimiwa...

MWENYEKITI: Sawa, sasa ngoja tuelewane vizuri, tuelewane vizuri Mheshimiwa. Huo waraka Mheshimiwa Waziri amerudia tena hilo jambo hapa wakati akihitimisha hoja, kwamba huo waraka ye ye haufahamu kama upo, hizo waraka zilizopo zote zimefuata sheria anazozifahamu ye ye, sasa wewe kwa sababu unasema aje na..., yaani aseme ama aje na kauli ya Serikali kuhusu waraka huo ambao haujui. (*Kicheko*)

Labda mimi niseme hivi, huo waraka ambao unakinzana na sheria wewe mpelekee kwa sababu sasa mimi ndiyo naagiza. Wewe mpelekee huo waraka halafu ukimpelekea utaniambia mimi ili nimpe maelekezo ya nini cha kufanya kwa sababu ye ye haujui hata akisema hapa kwamba nitaufanyia kazi haufahamu. Lakini wewe kwa sababu unaufahamu na unasema upo nadhani ni muhimu

wewe kuuchukua huo waraka kumpelekeia ili awe na uhakika anajisemea kwenye waraka gani. Sekunde moja malizia.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, niseme tu kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba atakwenda kutafuta naomba niwe na imani naye nikiamini kwamba anakwenda kutafuta na baada ya kuupata basi ataufanya kazi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Sasa kazi, Mheshimiwa Waziri sawa yeye anaenda kutafuta, lakini wewe ulionao mahsusimpe mpelekeetili usimpe kazi ngumu ikapita muda mrefu ukasema Waziri hajaupata, yeye mpaka sasa hivi hana. Kwa hiyo Mheshimiwa Agnesta utampelekeia. Ahsante sana. Tumalizie na Mheshimiwa Neema Mwandabila. (*Kicheko*)

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na niseme tu ningependa kupata ufanuzi wa Serikali kwa masuala haya ambayo nitaenda kuyasema.

Kwa kuwa watumishi wa nchi hii wana haki sawa katika Serikali yao hii na kwa kuwa wote wanajenga nchi moja ya Jamhuri Muungano wa Tanzania, kumekuwa na watumishi wa kada moja katika *section* tofauti kwa maana wengine unakuta wanapewa wapo kwenye Wakala wa Serikali wakati wengine wapo katika *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wamekuwa wakipewa malipo tofauti *but the same* kada, na unakuta watu waliopo kwenye Wakala wa Serikali wanapewa malipo makubwa kuliko watu waliopokatika *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia watumishi hawa hawa katika Idara moja *let saylabda* kwenye Wizara ya Afya nichukulie mfano Wizara ya Afya kwa sababu nimekuwa mtumishi huko. Watu wote wapo Wizara ya Afya, wote wapo hospitali, nichukulie mfano wa Maafisa Lishe na Maafisa Ustawi wa Jamii, wamekuwa wanapata mshahara *scale* nyiningine...

MWENYEKITI: Fupisha maelezo, kengele imeshagonga huku, kwa sababu muda huu huwa unaenda kwenye hoja moja mahsusi.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hoja yangu ipo hapa kwa nini Maafisa Lishe na Maafisa Ustawi wa Jamii wanamshahara wa *TGS* badala ya *TGHS* wakati wote wanafanya katika Wizara moja ya Afya? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.
(*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ningependa kumjibu, Mheshimiwa Mbunge kwamba utofauti wa mishahara unatokana na miundo tuliyonayo kati ya Wizara na Wizara na kati ya Taasisi na Taasisi. Lakini hoja yake pia ni ya msingi sisi kama Wizara tutakwenda kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kazi kubwa ya kwenda kufanya, tunakwenda kupitia miundo yote ya taasisi mbalimbali ili kuondoa ile adha ambayo inatokea sasa watumishi wengi kutaka kuhamza kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutakwenda kujipanga vizuri kama wizara mimi na timu yangu, tutakwenda kukaa na kupitia miundo hii na tutaangalia utaratibu mzuri wa kutumia ili kila Mtanzania, mfanyakazi katika sekta ya umma waweze kufanya kazi vyema na tutaangalia pia na mambo mengine na tunaamini kwamba itakwenda kusaidia katika Utumishi wa Umma. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tunashukuru kwa majibu hayo mazuri lakini naamini hayakusudii kuwafanya watu wote wafanane kwa sababu kazi na majukumu pia huwa zinatofautiana. Kwa hiyo, naamini katika mambo mnayoenda kuangalia mnaenda kuangalia na hilo pia.

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio waliokuwa wameomba kupata ufanuzi sasa nawahoji Fungu linaafikiwa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Katibu hapa ananiambia bado dakika kumi, kwa hiyo, tunaenda kwenye utaratibu wa *guillotine*.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida; Fungu 33 - Ofisi ya Rais - Sekretarieti...

MWENYEKITI: Anza na Fungu 32 kwa sababu ulikuwa umeshaanza kulitaja. Taja zile ulizotaja.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

FUNGU 32 – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i> | Sh.12,505,350,800 |
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> | Sh. 427,631,700 |
| Kifungu 1003 - <i>Government Communication Unit</i> | Sh. 224,164,000 |
| Kifungu 1004 - <i>Procurement Management Unit</i> | Sh. 262,670,000 |
| Kifungu 1005 - <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 245,915,500 |
| Kifungu 1006 - <i>Planning Division</i> | Sh. 467,155,500 |
| Kifungu 1007 - <i>Legal Services Unit</i> | Sh.141,519,000 |
| Kifungu 2001 - <i>Policy Development Division</i> | Sh. 718,356,745 |
| Kifungu 2002 - <i>Management Services Division</i> | Sh. 630,168,900 |
| Kifungu 2003 - <i>Establishment Division</i> | Sh. 857,090,000 |
| Kifungu 2004 - <i>Ethic Promotion Division</i> | Sh. 464,513,110 |

Kifungu 2005 - *Human Capital Management*
Division.....Sh. 1,270,064,500
Kifungu 2006 - *Performance Contracting*.....Sh. 423,864,000
Kifungu 3001 - *Human Resources Development*
Division.....Sh. 6,169,455,400
Kifungu 3004 - *Division of Salary and Remuneration*Sh. 530,776,045
Kifungu 4002 - *Management Information System Division*.....Sh. 8,128,539,800

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 04 – IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*..... Sh.1,166,924,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh.140,978,000
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.....Sh. 79,340,000
Kifungu 1004 - *Information and Communication Technology Unit*.....Sh.141,444,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*.....Sh.400,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*.....Sh.99.030.000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*..Sh.900,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit*....Sh. 87,544,000
Kifungu 4001 - *Archive Management Division*....Sh.223,956,000
Kifungu 4002 - *Records Management Division*....Sh.349,736,000
Kifungu 4003 - *Records Centre Division*.....Sh.164,510,000
Kifungu 4004 - *The Founders of the Nation Centre Division*.....Sh.116,256,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 20 – IKULU

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 24,557,764,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 30 – OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*.....Sh. 460,000,839,000

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 766,928,000

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh. 912,293,000

Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 531,495,000

Kifungu 1005 - *Information and Communication Technology Unit*.....Sh. 292,310,000

Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.....Sh. 509,360,000

Kifungu 2001 - *Cabinet Secretariat*.....Sh. 2,851,616,000

Kifungu 2002 - *Government Communication*.....Sh. 370,970,000

Kifungu 2003 - *Good Governance*.....Sh. 990,066,000

Kifungu 2004 - *Public Service Appeal*.....Sh. 696,040,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 33 – OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI VIONGOZI WA UMMA

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*.....Sh.1,815,612,760

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 417,454,440

Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.....Sh. 289,736,000

Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh.138,618,952

Kifungu 1005 - *Procurement and Management Unit*.....Sh. 284,856,000

Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*.....Sh.197,400,000
Kifungu 1007 - *Information and Communication Technology Unit*.....Sh. 257,968,000
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*.....Sh. 148,968,000
Kifungu 2001 - *Public Leaders Ethics Enforcement Division*.....Sh. 392,854,000
Kifungu 2002 - *Public Leaders Ethics Promotion Division*.....Sh. 414,180,000
Kifungu 2004 - *Zonal Office - Northern Zone*.....Sh. 286,328,648
Kifungu 2005 - *Zonal Office - Southern Zone*.....Sh. 281,592,200
Kifungu 2006 - *Zonal Office - Central Zone*.....Sh. 392,240,000
Kifungu 2007 - *Zonal Office - Eastern Zone*.....Sh. 375,684,000
Kifungu 2008 - *Zonal Office - Southern Highlands*.....Sh. 376,124,000
Kifungu 2009 - *Zonal Office - Lake Zone*.....Sh. 432,540,000
Kifungu 2010 - *Zonal Office - Western Zone*.....Sh. 257,598,000
Kifungu 2011 - *Zonal Office - Dar es Salaam*.....Sh. 607,166,000

(Vifungu vilivytajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 67 – OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*.....Sh.1,438,254,725
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 98,034,000
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.....Sh.86,588,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh. 87,968,395
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*.....Sh.85,110,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.....Sh.103,758,485
Kifungu 1007 - *Management Information Systems Unit*.....Sh. 267,508,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 77,330,000

Kifungu 2001 - *Recruitment Management*
Division.....Sh. 782,498,395
Kifungu 2002 - *QualityControl*.....Sh.361,721,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 94 – OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management* Sh.1,859,725,673
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 306,874,814
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.....Sh. 371,735,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 93,534,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*.....Sh.100,888,000
Kifungu 1006 - *Legal Services Unit*.....Sh. 217,918,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*.....Sh.126,128,000
Kifungu 1008 - *Information and Communication Technology Unit*.....Sh.143,961,682
Kifungu 1009 - *Guidelines Formulation Dissemination and Research*.....Sh. 237,958,000
Kifungu 2006 - *Appeals and Complains Department*.....Sh.1,032,125,831
Kifungu 2007 - *HR Standards and Compliance Department*.....Sh. 809,985,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 04 – IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

Kifungu 4001 - *Archive Management Division*...Sh.1,275,000,000
Kifungu 4002 - *Records Management Division*....Sh.725,000,000
(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**FUNGU 30 - OFISI YA RAIS SEKRETARIETI YA BARAZA LA
MAWAZIRI**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh.171,858,401,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 32 – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 - *Administration and Human
Resource Management*.....Sh. 2,000,000,000

Kifungu 2002 - *Management Services
Division*.....Sh.132,000,000

Kifungu 2005 - *Human Capital
Management Division*.....Sh.200,000,000

Kifungu 2006 - *Performance Contracting*.....Sh.150,000,000

Kifungu3001 - *HR Development Division*.....Sh. 150,000,000

Kifungu 4002 – *Management Information
System Division*.....Sh.5,018,000,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 – SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI
WA UMMA**

Kifungu 1001 - *Administration and Human
Resource Management*.....Sh.1,000,000,000

Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and
Evaluation Unit*.....Sh. 534,000,000

Kifungu 1004 - *Government Communication
Unit*.....Sh. 60,000,000

Kifungu 1007 – *Information and Communication
Technology Unit*.....Sh. 0

Kifungu 2001 - *Public Leaders Ethics
Enforcement Division*.....Sh. 59,620,00

Kifungu 2002 - *Public Leaders Ethics
Promotion Division*.....Sh. 21,100,000

Kifungu 2004 - *Zonal Office - Northern Zone*.....Sh. 14,145,000
Kifungu 2005 - *Zonal Office - Southern Zone*.....Sh.25,241,000
Kifungu 2006 - *Zonal Office- Central Zone*.....Sh. 25,241,000
Kifungu 2007 - *Zonal Office- Eastern Zone*.....Sh. 25,241,000
Kifungu 2008 - *Zonal Office- Southern Highlands*.....Sh. 25,241,000
Kifungu 2009 - *Zonal Office- Lake Zone*.....Sh.12,050,00
Kifungu 2010 - *Zonal Office- Western Zone*.....Sh.16,140,000
Kifungu 2011 - *Zonal Office-Dar es Salaam*.....Sh.31,981,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa taratibu zetu sasa nitawahoji.

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote kuwapongeza sana, sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote ambao nao wapo hapa, kwanza kwa kupokea michango ya Wabunge na kusikiliza ushauri wa Kamati yetu ya Bunge inayoshughulikia ofisi hii. Lakini pia kwa kupokea mawazo ya Wabunge humu ndani na hawa Wabunge mwisho wake kuridhika na maelezo ya upande wa Serikali na kuitisha bajeti hii, ninawapongeza sana. *(Makof)*

Kwa kuwa Bunge limesharidhia, kile ambacho mlikuwa mmekiomba, hakuna hata shillingi iliyopungua, tunaamini yale yote mliyoyaahidi kwamba mnakwenda kuyafanya basi mnakwenda kuyatekeleza kwa ukamilifu wake kama ambavyo Bunge limefanya kwa sehemu yake. Sisi tunawakia kila kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu na utekelezaji wa yale yote ambayo mmewaaahidi Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba mnakwenda kuyatekeleza. Tunawatakia kila kheri. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja hapa, mnatangaziwa kwamba kutakuwa na Kongamano la Miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar litakalofanyika siku ya Jumatatu, tarehe 26 Aprili, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Chimwaga, Dodoma kuanzia saa tatu asubuhi. Mgeni rasmi katika Kongamano hilo atakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge wote mtakaoshiriki kongamano hilo mnaombwa kujiorodhesha katika eneo la mapokezi ili usafiri uweze kutayarishwa kwa ajili ya kuwatoa hapa na kuwapeleka Chimwaga ili msipate taabu kwenda huko na magari yenu. Kwa hiyo, mnawenza kujiandikisha leo halafu siku ya tarehe 26 Aprili, 2021 kwa kuwa tukio linaanza

saa tatu basi pale mapokezi mtashauriwa muda gani mfike ili muweze kuelekea huko kumsikiliza Mheshimiwa Makamu wa Rais wetu ambaye kama Mheshimiwa Spika alivyokuwa anasema alikuwa Mbunge mwenzetu hapa, ni muhimu kwenda huko tukasherehekee hiyo siku yetu ya Muungano tukiwa pamoja naye. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, na mimi niwatakie sherehe njema za Muungano, tuendelee kukumbua waasisi wetu wa Taifa hili ambaao ndio walituunganisha tumekuwa wamoja, tumekuwa nchi moja na mara zote tunasisitiza tuendeleze umoja huo. Nawatakia kila la kheri katika hiyo siku ya tarehe 26 Aprili, 2021.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumanne, tarehe 27 Aprili, 2021 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.33 Usiku Bunge lillahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 27 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*